# PRAGMATIKI YA KIHISISHI CHA KISWAHILI

**TASNIFU**

**YA**

**ADELAIDE KHAVAI**

**TASNIFU ILIYOTOLEWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**APRILI, 2017**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo chochote.

______________________________________________________

ADELAIDE KHAVAI C50/23538/2013

Tasnifu hii imewasilishwa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi.

______________________________________________________

DAKTARI ALICE NYAMBURA MWIHAKI

______________________________________________________

DAKTARI LEONARD CHACHA MWITA

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mwandani wangu Georgiads Mboya,

na mabinti zangu wapendwa,

Anastasia Ndendwa, Alice Mueni na Juliet Ngina.

## SHUKRANI

Katika kuwasilisha tasnifu hii, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote ambao kwa njia moja au nyingine walinisaidia kabla na hata wakati wa kuitayarisha kazi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, uzima na nguvu za kuweza kuitekeleza hadi mwisho. Namshukuru sana Rabuka kwa vyote nilivyo navyo. Safari hii ilikuwa ndefu lakini Mungu alikuwa nami na kunipa nguvu za kuweza kuimaliza. Jina lake liinuliwe na kutukuzwa.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu wapendwa, Dkt. Mwihaki na Dkt. Chacha kwa ulezi, ushauri, uelekezi na wema wenu. Mmeninoa na kunilainisha katika usomi. Ningependa mfahamu ya kwamba nisingeweza kufika hapa bila nyinyi. Mungu na ambariki sana pamoja na familia zenu. Asanteni sana.

Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili chuoni: Dkt. Wafula, Dkt. Ngugi, Prof. Mbaabu, Prof King’ei, Prof. Ndungo, Dkt. Osore, Dkt. Onyango, Dkt. Masinde, Mwl. Mudhune, Dkt. Gakuo, Dkt. Arege, Mwl. Gathenji, na Dkt. Maitaria. Mlinielimisha kwa mengi na kuniongezea ujuzi. Shukrani za dhati kwenu nyote. Namshukuru Bi. Ngesu wa Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya University kwa kulihariri pendekezo langu. Asante sana kwa maelekezo na mashauri yako, Mungu akubariki.

Kwa mume wangu Georgiads, natoa shukrani zangu za dhati kwa mapenzi yako, ushauri na uvumilivu nilipokuwa masomoni. Ulinifaa wakati huu wote na unaendelea kunifaa. Kwangu ulikuwa tegemeo kwa hali na mali. Ulinipa moyo wa kuanza na kuendelea

kusoma, na kunihimiza kila wakati kutia bidii. Uliwatunza wana wetu wakati nilikuwa masomoni. Asante sana mpenzi. Mungu na akuzidishie neema na baraka zake.

Nawashukuru wanangu Ndendwa, Mueni na Ngina kwa mapenzi yenu na uvumilivu wakati mlipokuwa na mama mwanafunzi. Asanteni kwa kunihimiza kutia bidii na kuniomba kushindana nanyi masomoni. Himizo lenu lilinipa moyo wa kuendelea na kuleta nyumbani matokeo mazuri. Kongole kwa kazi nzuri, Mungu na amwezeshe kusoma zaidi ili muweze kumpiku mama yenu.

Wazazi wangu, marehemu John Amalemba na Juliana Amalemba nawashukuru kwa kunileta katika ulimwengu huu, kunilea na kunielekeza katika maadili. Shukrani pia ziwaendee shangazi wapendwa mtawa Jane Amache na marehemu Rufina Wamboi kwa kuchukua nafasi ya baba ya kunielimisha na kunipa mwanga maishani. Mbarikiwe sana. Shemeji Stans asante kwa kunipa moyo wa kuendelea. Mavyaa na bavyaa asanteni kwa yote mliyonifanyia nilipokuwa masomoni.

Mwisho, nawashukuru wanafunzi wenzangu chuoni katika Idara ya Kiswahili: Lucy, Tabitha, Christine, Judy, Grace, Phoebe, Kibet, Koskei, Kehongo, Winny, Wambua, Elizabeth, Rebecca na Juma kwa ushirikiano wenu masomoni. Bila kumsahau Doris, rafiki yangu wa karibu ambaye tulisaidiana na kushirikana kwa mengi, Mungu na ambariki sana. Shukrani zangu pia ziwaendee wote walionifaa katika kazi hii, asanteni sana. Alhamdullihai!

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchanganua **Pragmatiki ya Kihisishi cha Kiswahili** kwa madhumuni ya kubainisha maumbo na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili. Kihisishi hutumika katika mawasiliano ya kila siku ya watu kuonyesha hisia mbalimbali. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu ikisaidiwa na nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo. Data ya utafiti ilikusanywa kupitia kwa mbinu za usomaji, uchunzaji na mahojiano. Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa kihisishi cha Kiswahili kina maumbo ya aina tatu: maumbo ya kifonolojia, maumbo ya kimofolojia, na maumbo ya kisintaksia. Kihisishi cha Kiswahili kimedhihirisha matumizi mbalimbali kupitia kwa amali za: uarifu, ujamilishi, unafsishi, uliwazi, utendezi, ukalimizi, na uchangamshaji. Matumizi haya ya vihisishi yameonyesha kuwa vihisishi ni muhimu katika Kiswahili na katika lugha zote kwa jumla. Matokeo ya utafiti pia yamedhihirisha kuwa muktadha wa mawasiliano ni muhimu katika kufafanua matumizi ya kihisishi. Tasnifu ya utafiti imepangwa katika sura nne: utangulizi, umbo katika kihisishi cha Kiswahili, matumizi ya kihisishi cha Kiswahili na hitimisho. Matokeo ya utafiti yana nafasi ya kutumika katika ufunzaji na ujifunzaji wa vihisishi katika hatua mbalimbali za elimu na pia kwa watafiti wa baadaye.

## ABSTRACT

This research investigated **The Pragmatics of Kiswahili Interjection** with the aim of distinguishing the forms and functions of the Kiswahili interjection. Interjections are very essential in the day to day communication because they express emotions. The study was guided by Critical Discourse Analysis theory and the Systemic Functional Grammar theory. The data for the study was obtained through literature reviews, interviews and observational methods. The research findings show that the Kiswahili interjection consists of three forms: phonological forms, morphological forms and syntactic forms. In addition, the Kiswahili interjection exhibits different functions through various language functions: informative function, social contact function, expression function, alleviation of anxiety function, control function, role related function and stimulation function. These functions illustrate that interjections are very crucial not only in Kiswahili but in all languages. The study also identified that context influences the interpretation of the meaning of interjections during communiction. This project report is structured in four chapters: introduction, forms of the Kiswahili interjection, functions of the Kiswahili interjection and the conclusión. We believe that the research report will be useful in the teaching and learning of Kiswahili interjections at various levels of education and also to the future researchers.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Kihisishi** | Neno linaloonyesha hisia za msemaji. |
| **Kishazi huru** | Sentensi sahili. |
| **Matini** | Kipashio cha mfululizo wa usemi ambacho huwakilishwa kwa matamshi au maandishi. |
| **Pragmatiki** | Taaluma inayoshughulika na maana kulingana na muktadha wa mawasiliano. |
| **Sarufi Amilishi Mfumo** | Nadharia ya sarufi inayotazama lugha kama mfumo wa maana unaowakilishwa katika matini za kisarufi. |
| **Uchanganuzi Usemi Jadilifu** | Nadharia ya kiisimujamii inayozingatia hoja kuwa lugha hutegemea mahusiano ya watu katika jamii. |
| **Ufasili** | Mchakato wa matumizi ya lugha ambao matini huelezewa na wanajamii. |
| **Usemi** | Ni tamko la lugha ambalo ni tendo la mawasiliano lenye muundo wa uamilifu. |

## ORODHA YA VIFUPISHO

**EAEP** East African Educational Publishers

**JKF** Jomo Kenyatta Foundation

**KIE** Kenya Institute of Education

**KV** Konsonanti Vokali

**SAM** Sarufi Amilishi Mfumo

**TUMK** Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya

**TUKI** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**UUJ** Uchanganuzi Usemi Jadilifu

**UK** United Kingdom

**YALIYOMO**

Mada ya Utafiti………………………………………………………………………….....i
Ikirari........................................................................................................................ ii
Tabaruku ................................................................................................................. iii
Shukrani ................................................................................................................. iv
Ikisiri ....................................................................................................................... vi
Abstract…………………………………………………………………………….vii
Ufafanuzi wa Istilahi............................................................................................. viii
Orodha ya Vifupisho............................................................................................... ix
Orodha ya Yaliyomo…………………………………………………………….... x
Orodha ya Majedwali ............................................................................................ xiii
**SURAYA KWANZA**:**UTANGULIZI**.......................................................................... 1
1.0 Usuli Wa Utafiti ................................................................................................... 1
1.1 Swala La Utafiti ................................................................................................... 5
1.3 Maswali Ya Utafiti................................................................................................ 7
1.4 Malengo Ya Utafiti ............................................................................................... 7
1.5 Upeo Na Mipaka Ya Utafiti ................................................................................. 7
1.6 Sababu Za Kuchagua Mada .................................................................................. 9
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada............................................................................. 11
1.7.1 Tafiti Bayana Kuhusu Kihisishi Katika Lugha Zingine ..................................... 11
1.7.2 Tafiti Bayana Kuhusu Kihisishi Cha Kiswahili................................................. 15
1.8 Misingi Ya Nadharia .......................................................................................... 17
1.8.1 Uchanganuzi Usemi Jadilifu ............................................................................. 17
1.8.1.1 Muundo Wa Usemi ......................................................................................... 18
1.8.1.2 Mbinu Za Uchanganuzi.................................................................................... 20
1.8.2 Sarufi Amilishi Mfumo ...................................................................................... 20
1.8.2.1 Muundo Wa Sarufi........................................................................................... 21
1.8.2.2 Amali Za Maana .............................................................................................. 22
1.8.2.3 Amali Za Kishazi ............................................................................................. 23
1.9 Mbinu Za Utafiti ................................................................................................ 25
1.9.1 Eneo La Utafiti.................................................................................................. 25
1.9.2 Sampuli Na Usampulishaji ................................................................................ 26
1.9.3 Mbinu Za Kukusanya Data ................................................................................ 27
1.9.4 Vifaa Vya Utafiti................................................................................................ 28

1.9.5 Maadili Ya Utafiti ........ 28
1.9.6 Uchanganuzi Wa Data ........ 29
1.9.7 Uwasilishaji Wa Matokeo ........ 30
**SURA YA PILI: MAUMBO YA KIHISISHI CHA KISWAHILI ........ 31**
2.0 Utangulizi ........ 31
2.1 Maumbo Ya Kifonolojia ........ 31
2.1.1 Umbo La Silabi Moja ........ 32
2.1.1.1 Umbo La Konsonanti Vokali ........ 32
2.1.1.2 Umbo La Vokali Pekee ........ 33
2.1.1.3 Umbo La Konsonanti Silabi ........ 35
2.1.2 Umbo La Silabi Nyingi ........ 36
2.1.3 Umbo La Kiarudhi ........ 40
2.2 Maumbo Ya Kimofolojia ........ 43
2.2.1 Umbo La Mofimu Moja ........ 44
2.2.2 Umbo La Mofimu Moja Ambatano ........ 45
2.2.3 Umbo La Mofimu Mbili ........ 46
2.2.4 Umbo La Mofimu Changamano ........ 49
2.3 Maumbo Ya Kisintaksia ........ 51
2.3.1 Umbo La Kundi La Maneno ........ 51
2.3.2 Kihisishi Cha Vijenzi Viwili ........ 53
2.4 Hitimisho ........ 56
**SURA YA TATU:MATUMIZI YA KIHISISHI CHA KISWAHILI ........ 57**
3.0 Utangulizi ........ 57
3.1 Uarifu ........ 59
3.1.1 Vihisishi Vya Kukubali ........ 59
3.1.2 Vihisishi Vya Kukataa ........ 64
3.1.3 Vihisishi Vya Kutaka Taarifa ........ 67
3.2 Ujamilishi ........ 68
3.2.1 Kihisishi Cha Kubisha ........ 69
3.2.2 Vihisishi Vya Kukaribisha ........ 69
3.2.3 Vihisishi Vya Salamu ........ 71
3.2.4 Vihisishi Vya Kuita ........ 75
3.2.5 Vihisishi Vya Kuitika ........ 77
3.2.6 Vihisishi Vya Shukrani ........ 81

3.2.7 Vihisishi Vya Maagano ........ 82
3.2.8 Vihisishi Vya Samahani ........ 84
3.2.9 Vihisishi Vya Pongezi ........ 87
3.3 Unafsishi ........ 89
3.3.1 Vihisishi Vya Mshangao ........ 89
3.3.2 Vihisishi Vya Kusihi ........ 96
3.3.3 Vihisishi Vya Dharau ........ 97
3.3.4 Vihisishi Vya Mshtuko ........ 101
3.3.5 Vihisishi Vya Majuto ........ 102
3.4 Uliwazi ........ 103
3.4.1.Vihisishi vya Kufariji........102
3.5 Ukalimizi ........ 106
3.5.1 Vihisishi Vya Kuapa ........ 107
3.5.2 Vihisishi Vya Dua ........ 108
3.6 Utendezi ........ 114
3.6.1 Vihisishi Vya Kutuliza ........ 114
3.6.2 Vihisishi Vya Kuamrisha ........ 117
3.7 Uchangamshaji ........ 118
3.7.1 Vihisishi Vya Kutanguliza Hadithi ........ 118
3.7.2 Vihisishi Vya Kushangilia ........ 119
3.8 Hitimisho ........ 120
**SURA YA NNE:HITIMISHO ........ 122**
4.0 Utangulizi ........ 122
4.1 Matokeo Ya Utafiti ........ 125
4.2 Mahitimisho Ya Utafiti ........ 129
4.3 Mapendekezo Kuhusu Utafiti Zaidi ........ 130
**Marejeleo ........ 132**
Kiambatisho A:Data Ya Utafiti........137
Kiambatisho B: Kiongozi Cha Mahojiano ........ 167
Kiambatisho C: Vibali Vya Utafiti ........ 168

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 2.1 Vihisishi vya Konsonanti Vokali……………………………………………33

Jedwali 2.2 Vihisishi vya Vokali Pekee…………………………………………………..34

Jedwali 2.3 Vihisishi vya Konsonanti Silabi.…………………………………………..35

Jedwali 2.4 Vihisishi vya Silabi Mbili……………………………………………………37

Jedwali 2.5 Vihisishi vya Silabi Tatu……………………………………………………..38

Jedwali 2.6 Vihisishi vya Silabi Nne……………………………………………………...38

Jedwali 2.7 Aina za Kidatu………………………………………………………………..41

Jedwali 2.8 Vihisishi vyenye Wakaa……………………………………………………...42

Jedwali 2.9 Vihisishi vya Mofimu Moja Sahili…………………………………………...44

Jedwali 2.10 Umbo la Mofimu Moja Ambatano…………………………………………...45

Jedwali 2.11 Vihisishi vyenye Viambishi Awali…………………………………………..46

Jedwali 2.12 Vihisishi vyenye Viambishi Tamati…………………………………………47

Jedwali 2.13 Vihisishi vya Mofimu Mbili kutokana na Uunganishaji…………………..48

Jedwali 2.14 Vihisishi vya Mofimu Changamano…………………………………………50

Jedwali 2.15 Vihisishi vya Kundi la Maneno………………………………………………52

Jedwali 2.16 Kihisishi cha Maamkizi………………………………………………………54

Jedwali 2.17 Dhihirisho la Kishazi kama Uwakilishi……………………………………55

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Utafiti

Katika lugha ya Kiswahili, kama ilivyo katika lugha zingine za ulimwengu, kuna aina ya maneno ambayo hutumika kudhihirisha hisia za binadamu. Maneno haya huitwa vihisishi, na ni muhimu katika mawasiliano ya watu ya kila siku. Utafiti huu unahusu Pragmatiki na ulidhamiria kuchangia katika uelewaji zaidi wa kihisishi cha Kiswahili. Sura hii inaweka msingi wa tasnifu, kuanzia usuli wa utafiti hadi mbinu za utafiti.

Kwa mujibu wa Nerlich na Clarke (1997), pragmatiki inakisiwa kuwa ina asili yake katika falsafa ya lugha, na hasa kazi za wataalamu wanne: Charles Sanders Peirce (1839-1914), William James (1842-1910), John Dewey (1859- 1952), na John Langshaw Austin (1911-1961). Falsafa ya lugha hujishughulisha na nadharia za maana, matumizi ya lugha, utambuzi wa lugha, na uhusiano kati ya lugha na hali halisi ya maisha.

Matumizi ya kisasa ya neno pragmatiki yanahusishwa na mwanafalsafa Charles Morris, aliyeandika mwaka wa 1938 kuhusiana na umbo la kijumla la taaluma ya semiotiki (Levinson 1983). Semiotiki ni taaluma inayoangalia lugha sawa na mfumo wa ishara unaowasilisha maana, na huegemea tanzu tatu za kisarufi: sintaksia, semantiki na pragmatiki. Sintaksia inashughulika na uhusiano kati ya ishara na ishara nyingine, huku semantiki ikionyesha uhusiano kati ya ishara na maana. Pragmatiki nayo inashughulikia uhusiano kati ya ishara na msemaji. Baada ya Morris, pragmatiki imeendelezwa na wataalamu mbalimbali. Hivi leo, pragmatiki ni taaluma inayojisimamia.

Pragmatiki ya kisasa ni taaluma inayoshughulika na maana kulingana na muktadha wa mawasiliano (Levinson 1983, Leech 1983, Yule 1996, na Huang 2007). Taaluma ya pragmatiki husisitiza dhamira ya msemaji, ikirejelea uhusiano wa maana na msemaji. Pragmatiki huchanganua usemi katika miktadha ya mawasiliano na hushughulikia mada msingi sita: maana awali, maana dokezi, maana dhamirifu, deksia, matendo ya usemi, na urejeshi penyezi. Kama amali ya urejeshi penyezi, pragmatiki huhakiki ujumbe unaodhamiriwa na usemi na basi hujihusisha na jinsi ambavyo msemaji huitumia lugha katika muktadha wa mawasiliano. Matumizi lugha kimawasiliano huhusika pakubwa tunapochanganua kihisishi.

Kihisishi ni neno ambalo hutumiwa katika usemaji na linaloonyesha hisia za msemaji kama vile: furaha, mshangao, hasira, uchungu, maumivu, au mshtuko mkali (TUKI 2013). Vihisishi hutokea mara nyingi wakati msemaji anapokumbwa na tukio linalosababisha hisia kwa mfano, msemaji anaposhtuka atasema *"Lo!"* Ama akihisi uchungu atasema *"Mama we!* Mbali na kuonyesha hisia, kihisishi pia hutoa maana kulingana na muktadha kinamotumiwa. Kihisishi huwa hakina uhusiano wa kisarufi na kategoria zingine za maneno na huwa na uhusiano mdogo sana wa kisarufi na sentensi ambamo hujitokeza.

Kihisishi huwakilishwa kimaandishi kwa alama ya hisi (!) ambayo hubainisha sifa ya tonisho. Katika mazungumzo, kihisishi hutamkwa kwa tonisho mahususi ili kutoa maana maalumu (www.reference.com/browse/ interjection). Dhana ya tonisho inarejelea ruwaza

za kidatu katika kishazi. Ruwaza za kidatu kwa hivyo, ndizo hutofautisha dhima za kihisishi.

Kwa kawaida kihisishi hakina maana moja lakini huwa na dhima nyingi, na maana yake hutegemea muktadha ambamo kinajitokeza (Corver 2010). Kihisishi ni muhimu katika isimu kwa sababu hupatikana wakati lugha inapokua na kuwa sehemu ya umilisi lugha. Msisitizo umo katika hali ya kupatikana kwa kategoria ya kihisishi katika lugha za ulimwengu. Mtoto mchanga anayejifunza lugha anaweza kutambua vihisishi katika sauti anazozisikia, kulingana na mazingira ya matumizi.

Kwa jinsi maneno mengine kama vile: *ng'ombe, kiti,* na *mti* yanavyotambulika kama vipengele vya kiisimu vyenye maana, ndivyo vilivyo vihisishi kama: *Lo! Aka!* na *Ewe!* Kihisishi hudhihirisha hisia za wahusika katika mazungumzo. Kama ilivyo katika lugha kwa jumla, kihisishi hutumika kama kioo cha mfumo wetu wa hisi. Baadhi ya vihisishi husisitiza hali ya kihisia ya msemaji.

Dhana ya kihisishi imekuwepo katika Sarufi Mapokeo tangu karne ya tano kabla ya Kristo, kwa mujibu wa wanafalsafa wa Kiyunani (Lyons 1968 na Ameka 1992a). Wanafalsafa wa Kiyunani walikichukulia kihisishi kuwa kategoria ndogo ya vielezi kwa sababu iliaminika kuwa vihisishi 'vingeamua' kitenzi hata kama kitenzi hicho kinaeleweka. Wanasarufi wa Kilatini walikuwa wa kwanza kuchukulia kihisishi kama kategoria ya maneno inayojisimamia. Jambo hili liliwawezesha kuhifadhi kategoria nane

za maneno zilizobainishwa na Wayunani, na ambazo zilikuwa nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi, kihusishi, kiunganishi, na kihisishi.

Mwanasarufi maarufu wa Kilatini, kwa jina Priscian, alikieleza kihisishi kama kategoria ya maneno inayoonyesha hisia (Ameka 1992a). Baadhi ya Wamodiste kama Martin wa Dacia na Thomas wa Erfurt walishikilia msimamo wa Wayunani lakini wakasisitiza zaidi uhusiano wa kihisishi na kitenzi. Wamodiste wengine kama Boethius wa Dacia wanasema kwamba kwa kawaida kihisishi si neno, ila ni kiashiria tu cha hisi za akili.

Wamodiste ni wanasarufi wa karne ya kumi na tatu hadi kumi na nne, ambao walijaribu kuzua kategoria za sarufi kutoka kwa kategoria za kimantiki, kiepistemolojia na kimetafizikia (Lyons 1968). Wanasarufi hao walizua kategoria hizi baada ya kutiwa moyo na kanuni za kisayansi. Mitazamo ya Wamodiste, na Wanamapokeo kwa jumla, inaashiria mtafaruku kuhusu dhana ya kihisishi. Mtafaruku kuhusu maana na umuhimu wa kihisishi umeendelea katika sarufi ya kisasa.

Tafiti nyingi zinazopatikana zimerejelea uchanganuzi wa kihisishi cha Kiingereza na baadhi ya lugha kama vile Kituruki na Kiq'eqchi' Maya (Ameka 1992b, Kockelman 2003, Büyükkantarcioğlu**2006 na Nguyen 2011). Mahitimisho ya tafiti husika yanaafikiana kuwa ingawa kihisishi ni muhimu katika lugha, kimepuuzwa kwa muda mrefu katika isimu. Matatizo kuhusu kihisishi pia yanajidhihirisha katika Kiswahili, kuashiria umuhimu wa utafiti.

## 1.1 Swala la Utafiti

Dhana ya kihisishi inahusika katika mtaala wa Kiswahili nchini. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (TUMK) awali ilijulikana kama Taasisi ya Elimu ya Kenya (Kenya Institute of Education. (KIE) huchapisha silabasi za shule za msingi, upili na vyuo vya walimu. Katika silabasi ya Kiswahili ya shule za msingi (KIE 2002a) na shule za upili (KIE 2002b) nchini, kihisishi cha Kiswahili hutazamwa kama mojawapo wa kategoria za maneno. Mwelekeo wa KIE na sasa TUMK, unaashiria kuwa kihisishi cha Kiswahili kimepewa umuhimu katika mtaala wa elimu nchini.

Ijapokuwa kihisishi kimepewa nafasi katika mtaala wa elimu, utafiti wa awali umeonyesha kuwa hakijachukuliwa kwa umuhimu mkubwa shuleni ikilinganishwa na kategoria zingine za maneno kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, viwakilishi na vielezi (Waihiga 1999, na Waihiga na Wamitila 2003). Vitabu vya sarufi ya Kiswahili havitoi mifano na mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi ili kuelewa zaidi maana mbalimbali zinazojitokeza na ambazo mara nyingi hukanganya. Waandishi mbalimbali wa vitabu vya sarufi ya Kiswahili wanakipa kihisihi nafasi ndogo na wengine hawakirejelei kabisa (Waihiga 1999, Waihiga na Wamitila 2003, Mumbo, Ngamia, Maneno na Mogambi 2004, Habwe na Karanja 2004, Njogu, Mwihaki na Buliba 2006, na Matei 2008). Hali hii imepelekea vihisishi vingine vya Kiswahili kupotea au kutumika kwa nadra sana. Fauka ya hayo, dhana ya kihisishi ina matatizo kwa sababu maana zake hukanganya kama inavyodhihirika katika baadhi ya maandishi.

Jina la kihisishi cha Kiswahili linakanganya. Waandishi wengine kama Ndalu (1997), Kihore, Massamba na Msanjila (2003) wanatumia neno kiingizi naye Mbaabu (1992) anatumia kishangao badala ya kihisishi. Jina kiingizi limekitwa sana katika msingi wa mpangilio ambapo kihisishi huja kabla ya sentensi inayofuata. Jina la kihisishi linafaa zaidi, kwa kuzingatia kuwa jina hilo limekitwa zaidi katika maana ambapo linahusu hisia mbalimbali.

Kama ilivyo katika lugha kwa jumla, kihisishi cha Kiswahili ni muhimu katika mawasiliano ya kila siku (Tazama §1.1). Vihisishi vya Kiswahili hufanya mawasiliano yaimarike na kuvutia. Vihisishi pia hufanikisha mawasiliano kwa kupunguza maelezo marefu ambayo mara nyingi hutolewa tu kwa neno moja.

Tafiti za kihisishi cha Kiswahili zinazopatikana zimechunguza kihisishi cha Kiswahili kama mawasiliano ya kitamaduni, ugumu wa kutenganisha matumizi ya lugha, na matumizi ya ishara katika vihisishi na sifa za vihisishi (Eastman 1983 na 1992, na Yahya-Othamn 1998). Tafiti hizi za kihisishi cha Kiswahili zilifanywa kwa ujumla bila mitazamo ya kinadharia. Utafiti huu kwa hivyo ulifanywa kwa kuegemezwa katika Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu ambayo ilishirikiana na Sarufi Amilishi Mfumo. Hali hii ilituongoza katika kukifanyia kihisishi cha Kiswahili utafiti zaidi ili kuangaza kanuni za matumizi na hasa kanuni za kipragmatiki, pamoja na kujibu maswali ya utafiti.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti kuhusu kihisishi cha Kiswahili uliongozwa na maswali matatu:

1. Kihisishi cha Kiswahili kina umbo gani?
2. Kihisishi cha Kiswahili kina matumizi gani?
3. Uchanganuzi Usemi Jadilifu una utoshelevu gani wa kubainisha kihisishi cha Kiswahili?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Kulingana na maswali, utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo matatu:

1. Kuchanganua umbo la kihisishi cha Kiswahili.
2. Kujadili matumizi ya kihisishi cha Kiswahili.
3. Kutathmini utoshelevu wa nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu katika kubainisha kihisishi cha Kiswahili.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kihisishi cha Kiswahili kinaweza kushughulikiwa katika taaluma mbalimbali za kiisimu na hasa isimujamii, isimu linganishi, isimu tafsiri, isimu matini, na isimu jumulifu. Utafiti huu ulijikita katika taaluma ya isimu jumulifu (sarufi), kwa kujihusisha na pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili bila kuchunguza tanzu zile zingine za kisarufi. Tanzu za fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki hazikurejelewa moja kwa moja isipokuwa pale ambapo zilihitajika katika kuangazia pragmatiki ya kihisishi kwa utoshelevu zaidi. Uchanganuzi

wa kipragmatiki ulitegemea hoja kuwa, kihisishi hurejelea matumizi ambayo hueleweka kwa ubora zaidi katika muktadha wa mawasiliano (Eastman 1983). Kimsingi, kihisishi hakiwezi kueleweka bila kurejelea muktadha wa matumizi.

Kama ilivyodokezwa katika usuli wa utafiti (Tazama §1.1), pragmatiki hushughulika na aina mbalimbali za maana: maana awali, maana dokezi, na maana dhamirifu. Pamoja na aina mbalimbali za maana, mada zingine ni deksia na matendo ya usemi. Mada hizi zote za pragmatiki zinatangamana na kuhusiana, na kwa hivyo zilizingatiwa katika utafiti wa kihisishi cha Kiswahili.

Utafiti pia ulirejelea nafasi ya tonisho katika kihisishi cha Kiswahili. Tonisho ni sifa ya kifonetiki inayorejelea ruwaza za kidatu katika ngazi ya kishazi. Tonisho vilevile hudhihirisha dhima ya kisintaksia na dhima ya kipragmatiki. Dhima ya kipragmatiki ya tonisho ilitumika katika kusawiri maumbo ya kihisishi pamoja na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili.

Kihisishi huonyesha uamilifu wa lugha wa jinsi watu huwasilisha hisia mbalimbali, na kwa hivyo huchanganuliwa kwa kuzingatia uhusiano kati ya umbo na dhima. Yahya-Othamn (1998) anasema kuwa ni halali kuvichukulia vihisishi kama njia aliyonayo msemaji katika kutenda aina mbalimbali ya matendo ya usemi. Katika kushughulikia kihisishi, utafiti ulichunguza umbo, na matumizi ya kihisishi katika mawasiliano ya kila siku ya watu na hivyo kutupa mwanga wa kuangaza sababu za kuchagua mada.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Pragmatiki kama utanzu wa sarufi umekuzwa kuanzia mwongo wa sabini katika karne ya ishirini (Huang 2007). Ukilinganishwa na tanzu zingine za sarufi, utanzu wa pragmatiki ni mchanga na unaendelea kukua. Utafiti kuhusu pragmatiki ya kihisishi una nafasi ya kuongezea ujuzi wa kijumla katika taaluma ya pragmatiki kwa kufafanua matumizi ya kihisishi cha Kiswahili katika miktadha mbalimbali. Pamoja na kuongezea ujuzi wa kimsingi, utafiti una uwezo wa kuangaza utoshelevu wa nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu katika maswala ya kipragmatiki.

Pragmatiki inaelekea kuwa na uwiano na taaluma za isimujamii, isimu anthropolojia, na semiotiki (King'ei 2010 na TUKI 1990). Isimujamii ni taaluma inayoeleza uhusiano uliopo kati ya matumizi ya lugha na misingi ya kijamii. Maarifa ya kipragmatiki yatamsaidia mwanaisimujamii katika kuelewa matumizi ya kihisishi na mahusiano ya kijamii. Isimu anthropolojia ni taaluma inayohusu tofauti za lugha kulingana na utamaduni wa watu. Kama ilivyotajwa katika usuli wa utafiti, semiotiki ni taaluma ya ishara na hugawika katika matawi ya sintaksia, semantiki na pragmatiki. Matokeo ya utafiti yatakuwa yenye manufaa katika taaluma ya isimujamii, isimu anthropolojia na semiotiki.

Katika kuchunguza na kutathmini dhana iliyoidhinishwa na silabasi ya Kiswahili nchini Kenya, utafiti wa kihisishi unaelekea kuwa na manufaa katika isimu pedagojia. Isimu pedagojia ni sayansi ya ufunzaji na ujifunzaji wa lugha, ambayo husisitiza

kinachofunzwa na mbinu za kufunza. Ufunzaji na ujifunzaji wa kihisishi katika Kiswahili una nafasi ya kuendeleza pedagojia ya Kiswahili.

Darasani, ujuzi wa kipragmatiki utamsaidia mwalimu kufafanua maana na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili anapofundisha. Wanafunzi wakielewa uamilifu wa kihisishi, wataweza kutumia lugha kwa ufasaha katika muktadha wa kimawasiliano unaofaa (Matrood 2010). Ujifunzaji bora wa jinsi ya kutumia vihisishi kulingana na muktadha utamwezesha mwanafunzi kuboresha uwezo wake wa kipragmatiki wa kutumia Kiswahili kikiwa lugha ya pili, katika mazoezi kama ya uandishi wa insha.

Wasomi wa lugha waweza kufaidika kutokana na utafiti huu kwa kurejelea data katika kufanya tafiti linganishi kuhusu matumizi ya kihisishi. Pamoja na tafiti linganishi za vihisishi katika lugha mbalimbali, utafiti unaweza kuwa wa kifasihi, kuhusiana na uchanganuzi wa vihisishi vinavyotumiwa na wahusika mbalimbali katika kazi za fasihi. Mbali na wahusika, utafiti wa kifasihi waweza kuhusu fani mbalimbali zinazotumika pamoja na vihisishi kama vile misemo.

Kwa ujumla, utafiti huu umechochewa na sababu za aina mbalimbali: sababu za kinadharia, sababu za utumikizi, na sababu za utendakazi. Hali hii inaashiria kuwa matokeo ya utafiti yatakuwa na sababu zenye manufaa. Sababu za kuchagua mada hazikosi uwiano na mambo mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Taarifa ya kijumla kuhusu dhana ya kihisishi tayari imeshughulikiwa katika usuli wa utafiti (Tazama § 1.1). Sehemu hii inashughulika na uhakiki wa maandishi bayana kuhusu kihisishi. Maandishi yaliyolengwa yanahusu maana, umbo, kategoria, dhima, sifa za kimofolojia, kisemantiki, na kipragmatiki za kihisishi, uakifishaji, na matumizi ya vihisishi kama lugha na ishara. Maandishi haya yaligawanywa katika makundi mawili: tafiti kuhusu kihisishi katika lugha zingine, na tafiti kuhusu kihisishi cha Kiswahili.

### 1.7.1 Tafiti Bayana kuhusu Kihisishi katika Lugha Zingine

Tahakiki kuhusu kihisishi katika lugha zingine ilichunguza namna kihisishi kimechanganuliwa katika lugha zifuatazo: Kiingereza, Kiarabu, Kituruki, na Kivietinamu. Tafiti hizi zimeshughulikia maana na uamilifu wa kihisishi, umbo na nafasi ya kihisishi, sifa za kimofolojia, na sifa za kipragmatiki za kihisishi. Utangulizi wa toleo maalumu la *Jarida la Pragmatiki* la 1992, lililozinduliwa kwa ajili ya vihisishi, ulizungumzia jinsi kihisishi kilikuwa kimepuuzwa katika isimu kwa sababu mbili kuu: historia (Tazama § 1.0) na sifa zake.

Sifa zinahusu namna ambavyo kihisishi kimeelezwa kisintaksia kama kategoria ya maneno na pia aina ya matamshi, jambo ambalo hutatanisha. Maoni ya Ameka (1992a) katika kuondoa utata huu ni kuwa, kihisishi kichukuliwe kama neno na pia kama usemi, hoja inayokitofautisha kihisishi na kategoria zingine za maneno. Kihisishi pia kifafanuliwe kulingana na muktadha kinamotolewa. Tamati ya utangulizi wa jarida hili

inatoa wito kwa wanaisimu na hasa wanaisimu wa kipragmatiki kuchukua jukumu la kufafanua kihisishi katika lugha nyingi zaidi ulimwenguni.

Maana katika kihisishi imeshughulikiwa na watafiti mbalimbali (Abdulla na Talib 2009, na Jovanovic 2004) ambao wanaafikiana kuwa kihisishi huwa na maana. Ulinganishi wa matumizi ya vihisishi katika Kiingereza na Kiarabu ni utafiti uliofanywa na Abdulla na Talib (2009), wakirejelea vigezo vya kisemantiki vya Wierzbicka (1992). Utafiti wao ulichunguza maana, ukaangalia kama kulikuwa na ulinganifu wa vihisishi, na kutalii uwezekano wa kuainisha vihisishi kwa kutumia vigezo hivi vya kisemantiki.

Kulingana na vigezo hivi, vihisishi huainishwa katika makundi matatu: maana kimatilaba (nahisi kitu), maana tambuzi (najua kitu) na maana volitivu (nataka kitu). Matokeo yalionyesha kuwa, hakukuwa na ulingalifu wa moja kwa moja wa vihisishi katika Kiingereza na Kiarabu. Vihisishi katika Kiingereza na Kiarabu haviwezi kuainishwa kwa kutumia utaratibu wa Wierzbicka kwa sababu kihisishi kimoja kilikuwa na uwezo wa kuwa katika makundi zaidi ya moja ya maana kimatilaba, maana tambuzi au maana volitivu. Kwa njia linganifu, utafiti huu una umuhimu kwa sababu unahusu maana za vihisishi katika lugha tajwa, jambo ambalo lilitusaidia katika kutambua maana za kihisishi cha Kiswahili. Tofauti na utafiti wetu ambao unahusu pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili, utafiti wao ulijikita katika taaluma ya semantiki.

Umbo la kihisishi cha Kiingereza, nafasi na maana zake linabainishwa na uchunguzi wa Jovanovic (2004). Utafiti huo ulinuia kujadili kihisishi cha Kiingereza na kuweka wazi umuhimu wake katika lugha. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa kwa upande wa fonolojia, vihisishi vingi hufuata mpangilio wa konsonanti vokali, na kwa upande wa mofolojia vihisishi havina maumbo maalumu. Kisintaksia, nafasi ya kihisishi huwa mwanzoni mwa sentensi ambapo hujisimamia.

Vihisishi vingi vya Kiingereza, kulingana na utafiti wa Jovanovic (keshatajwa), ni vya asili, ilhali vichache ni vya mkopo na vihisishi vinaweza kuwekwa katika makundi tofautitofauti kutegemea umuhimu wake kipragmatiki. Utafiti huo ulichangia utafiti wetu katika kuchanganua umbo na dhima za kipragmatiki za kihisishi cha Kiswahili. Tofauti ni kuwa, utafiti wetu ulitumia nadharia tofauti ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu ambayo hujihusisha na mambo ya kiisimujamii na pia dhima za kipragmatiki za kihisishi cha Kiswahili zilipatikana kutokana na mawasiliano halisi ya watu.

Dhima za kipragmatiki za vihisishi vya Kituruki kwa msingi wa njia tambuzi katika akili ya mtamkaji zilishughulikiwa na Büyükkantarcioğlu** (2006). Kihisishi kinaweza kutekeleza dhima tofautitofauti za kipragmatiki si kwa sababu ya muktadha wa hali, bali kwa sababu ya njia tambuzi katika akili ya mtamkaji. Kutegemea habari ya msemaji, msikilizaji huunda wazo na kwa kutegemea aina ya uundaji, dhima fulani ya kipragmatiki ambayo itashirikishwa na kihisishi inatambulika mwanzo katika mchakato wa kiakili. Utafiti wa Büyükkantarcioğlu** (keshatajwa) ulichangia utafiti wetu kwa dhima za

kipragmatiki za kihisishi. Utafiti wetu uliegemea muktadha wa mawasiliano tofauti na wake.

Nguyen (2011) alifanya utafiti kuhusu sifa za kimofolojia na sifa za kipragmatiki za kihisishi cha Kiingereza na kihisishi cha Kivietinamu. Utafiti huo ulidhamiria kuchunguza iwapo vihisishi katika lugha hizi vilifanana au vilitofautiana. Data ya utafiti ilikusanywa kutoka kwa filamu kwa kutumia mbinu ya maelezo na uchanganuzi linganishi. Vihisishi viliainishwa katika kategoria mbalimbali kwa kurejelea sifa za kimofolojia na sifa za kipragmatiki. Utafiti ulionyesha kuwa, kulikuwa na mfanano katika kutumia vihisishi kwani kihisishi kimoja kilikuwa na uwezo wa kutekeleza dhima tofauti za kipragmatiki. Tofauti ilibainika kuwa, katika Kiingereza vihisishi ambavyo hutumika huweza kujisimamia, jambo ambalo halitokei sana katika vihisishi vya Kivietinamu. Utafiti wa Nguyen (keshatajwa) ulitufaa katika uainishaji wa vihisishi vya Kiswahili. Utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa wake ni linganishi.

Tafiti bayana kuhusu kihisishi katika lugha zingine zimeshughulikia maana, umbo, nafasi, kategoria na sifa za kiisimu za kihisishi katika lugha mbalimbali. Tahakiki hii imeonyesha kuwa, kihisishi kina nafasi ya kufanyiwa tafiti katika lugha zaidi kwa kutumia nadharia na mbinu tofautitofauti. Tafiti bayana kuhusu kihisishi cha Kiswahili zitaangaziwa ili kutoa ufafanuzi zaidi wa kihisishi.

### 1.7.2 Tafiti Bayana kuhusu Kihisishi cha Kiswahili

Baada ya kujadili tafiti kuhusu kihisishi katika Kiingereza, Kiarabu, Kituruki, na Kivietinamu, tutachunguza tafiti bayana kuhusu kihisishi cha Kiswahili. Tafiti kuhusu kihisishi cha Kiswahili zimeshughulikia alama ya mshangao katika Kiswahili, vihisishi vya Kiswahili kama mawasiliano ya kitamaduni, matumizi ya kihisishi kama lugha na ishara, na sifa za kihisishi cha Kiswahili.

Uchunguzi wa alama ya mshangao katika kuakifisha ulifanywa na Ohly (1985). Kulingana na sarufi mapokeo, alama ya mshangao katika Kiswahili hutumika pamoja na vihisishi ama katika miundo madhubuti ya kisintaksia na kifonolojia. Madhumuni ya kufanya utafiti huu yalikuwa kuelezea upya dhima ya alama ya mshangao kwa kuhusisha uchanganuzi wa kipragmatiki. Utafiti huo ulichangia utafiti wetu kwa kuchunguza alama ya mshangao ambayo hutumiwa pamoja na kihisishi.

Utafiti kuhusu vihisishi vya Kiswahili sanifu kama mawasiliano ya kitamaduni ulishughulikiwa na Eastman (1983). Eastman (keshatajwa) alinuia kuonyesha kuwa vihisishi ni sehemu ya msamiati wa kitamaduni ambavyo hufungamanisha lugha na jamii husika. Vihisishi viliainishwa katika kategoria tano kutegemea dhima zake katika utamaduni wa Waswahili na pia orodha ya vihisishi mia moja na thelathini (130) ikatolewa katika *Kamusi Sanifu ya Kiswahili*. Utafiti huo ulitufaa katika uainishaji wa kihisishi kutegemea dhima za kipragmatiki. Tofauti na utafiti wake, utafiti wetu

uliainisha kihisishi kutegemea vipengele tofauti kwa utumikizi wa nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu.

Eastman (1992) alifanya utafiti mwingine ambapo alichunguza vihisishi vya Kiswahili kwa kurejelea ugumu uliopo wa kuweka mipaka kati ya matumizi ya lugha na matumizi ya ishara. Vihisishi huhusisha usemi na ishara. Katika mawasiliano, kihisishi chaweza kutamkwa pekee au pamoja na ishara. Wakati mwingine ishara pekee hutumiwa kwa uamilifu wa kihisishi. Vihisishi kama semi za mawasiliano huonyesha dhana ya mfumo wa kijamii ambao Waswahili hushiriki.

Utafiti kuhusu kihisishi cha Kiswahili pia ulifanywa na Yahya-Othamn (1998) ambaye alikuwa na nia ya kubainisha sifa za kihisishi cha Kiswahili na pia kuainisha vihisishi katika ufafanuzi wa kijamii. Katika utafiti huo, kihisishi cha Kiswahili kiliainishwa katika makundi manne: vihisishi elezi, vihisishi jamilishi, vihisishi maelekezo, na vihisishi mfumo. Utafiti huo ulisisitiza umuhimu wa muktadha katika utumiaji wa vihisishi vya Kiswahili. Utafiti wa Yahya-Othamn (1998) ulitufaa kwa mifano ya vihisishi vya Kiswahili, tofauti ni kuwa utafiti wetu ulishughulikia maumbo na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili.

Tahakiki ya maandishi kwa ujumla imefafanua mada mbalimbali za kihisishi zilizoshughulikiwa katika Kiswahili na katika lugha kwa ujumla. Mada sita ziliangaziwa: maana, maumbo, kategoria, dhima za kipragmatiki na dhima za semantiki, uakifishaji,

sifa na matumizi ya kihisishi kama lugha na ishara, na zimedhihirisha kuwa kihisishi bado kina nafasi kubwa ya kufanyiwa utafiti. Utafiti wetu ulidhamiria kuchunguza pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili kwa kushughulikia maumbo na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili kwa misingi ya nadharia tofauti.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti wa kipragmatiki unahitaji kurejelea nadharia zinazotegemea misingi ya kijamii, kitamaduni, na kimawasiliano. Nadharia zifuatazo zinaweza kutumika katika utafiti kama huu: Uchanganuzi mazungumzo, Ethnografia ya mawasiliano, Tendo la Usemi, Kidokezwa cha Grice, na Uchanganuzi Usemi Jadilifu. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu iliteuliwa kutumika katika utafiti huu kwa vile hutangamanisha taaluma kwa uthabiti zaidi.

### 1.8.1 Uchanganuzi Usemi Jadilifu

Uchanganuzi Usemi Jadilifu ni nadharia iliyoendelezwa pakubwa na Fairclough (1989 na 1995) ikiangazia maswala ya isimujamii. Fairclough (1989) alizingatia hoja kuwa, matumizi ya lugha hutegemea mahusiano ya watu katika jamii, sababu za watu za kijamii zilizofasiliwa na mandhari ya kijamii ambapo masharti ya kijamii huamua sifa za usemi. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu (UUJ) ilitokana na Isimu Jadilifu ambayo ilianzishwa katika Chuo Kikuu cha East Anglia katika mwongo wa sabini wa karne ya ishirini. Kwa jumla, wanaisimujamii wa wakati huo walikuwa wakilishughulikia kwa uchache suala la utabaka wa kijamii na mamlaka. Katika mtazamo huo, lugha huangaliwa


kama mfumo wa uzoefu wa kijamii, ambapo lugha ina viangama vitatu: sehemu ya jamii, mchakato wa kijamii, na mchakato wa uzoevu wa kijamii.

Kulingana na Fairclough (1995), Nadharia ya UUJ inashughulikia suala la jinsi muundo wa lugha unaamilisha dhima za msingi za kijamii. Uchanganuzi Usemi Jadilifu ni nadharia matinishi inayojihusisha na kutoa maelezo ya kisarufi yaliyo muhimu katika uchanganuzi wa maana lugha. Utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya UUJ: muundo wa usemi na mbinu za uchanganuzi.

#### 1.8.1.1 Muundo wa Usemi

Usemi unarejelea matini andishi ambayo huwakilishwa kimatamshi, na huhusisha hali za kijamii ambazo zinaweza kuelezwa kama hali za uzalishaji na za ufasiri (Fairclough 1989 na Wodak 2002). Hali za kijamii zinahusiana na viwango vitatu vya mfumo wa kijamii: muktadha wa kijamii ambao usemi hutokea, kiwango cha asasi za kijamii ambacho huhusisha muktadha mpana wa usemi na kiwango cha jamii jumlifu.

**(1.1) Kielelezo cha Muundo wa Usemi**




Kwa mujibu wa Fairclough (1989: 25).

Hali hizi za kijamii huunda sehemu ya rasilimali ambayo watu huileta kwa uzalishaji na ufasiri na ambayo huunda njia ambazo matini huzalishwa na kufasiriwa. Katika kielelezo 1.1, matini huwakilisha matamshi, maandishi, au lugha ishara. Matini ni zao katika mchakato wa uzalishaji na ni rasilimali katika mchakato wa ufasiri. Michakato ya uzalishaji na michakato ya ufasiri huathiriwa na hali za kijamii. Usemi kwa hivyo huhusisha matini, mahusiano na miktadha. Katika uchanganuzi, ni lazima kubainisha uhusiano kati ya matini, mahusiano na miktadha, hoja inayotuelekeza katika mbinu za uchanganuzi.

### 1.8.1.2 Mbinu za Uchanganuzi

Nadharia ya UUJ inatambulisha mbinu tatu za uchanganuzi: maelezo, ufasiri na ufasili. Mbinu ya maelezo huhusu ufafanuzi wa matini kutegemea fasiri na fasili zilizojitokeza. Ufasiri ni mbinu ya kuelezea mahusiano ya matini kama zao la mchakato wa uzalishaji, na matini kama chumo la mchakato wa ufasiri. Katika ufasiri, michakato tambuzi ya washiriki huchanganuliwa. Mbinu ya mwisho ya ufasili hushughulika na uhusiano kati ya mahusiano na muktadha wa jamii ambapo jamii huamua michakato ya uzalishaji na michakato ya ufasiri na athari zake.

Mihimili ya UUJ ilifaa kwa utafiti wetu wa pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili. Katika mhimili wa muundo wa usemi, usemi huhusisha matini, mahusiano, na miktadha. Mhimili huu ulitusaidia katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya vihisishi (matini), mahusiano ya kijamii na muktadha wa mawasiliano. Mbinu za uchanganuzi zilitumika katika kuchanganua maumbo, na matumizi ya vihisishi ili kutoa maelezo, ufasiri na ufasili wa kihisishi cha Kiswahili. Nadharia ya UUJ husisitiza uchanganuzi wa muktadha katika kuelewa matumizi ya lugha. Uchanganuzi Usemi Jadilifu kama tulivyotaja hapo awali ni nadharia ya kiisimujamii (Tazama §1.8.1), ili kufanikisha utafiti, nadharia hii ilihitaji nadharia ya kisarufi ambayo ni Sarufi Amilishi Mfumo.

## 1.8.2 Sarufi Amilishi Mfumo

Sarufi Amilishi Mfumo ni mtazamo wa kisarufi ambao husisitiza nafasi ya mawasiliano (Halliday 1985, 1994 na Halliday na Matthiessen 2004). Nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo (SAM) hulenga maana kwa namna zinavyowasilishwa na maumbo. Kwa

mtazamo huu, mfumo wa lugha huangaliwa sawa na mtandao wa maana. Hoja muhimu inayosisitizwa ni jinsi wazungumzaji huunda maana inayotarajiwa, kupitia kwa matini. Nadharia ya SAM hushughulika na sababu za matumizi ya lugha. Sarufi Amilishi Mfumo ina mihimili mitatu: muundo wa sarufi, amali za maana, na amali za kishazi.

#### 1.8.2.1 Muundo wa Sarufi

Muundo wa sarufi huzingatia madai kuwa, lugha ni mfumo amilishi na hutambua na kufuma tanzu tatu: sintaksia ambayo huonyesha uhusiano kati ya maumbo ya lugha yenyewe, semantiki inayohusika na uhusiano kati ya maumbo na maana msingi, na pragmatiki ambayo huonyesha uhusiano wa maana na msemaji kulingana na muktadha wa matumizi ya lugha.

Sarufi Amilishi Mfumo hutazama matini kwa namna ambavyo inakidhi mahitaji ya umilisi mawasiliano na utoshelevu wa kipragmatiki. Mtazamo huo unategemea hoja kuwa, lugha ni ishara ya kipragmatiki, ishara ya kufanikisha mawasiliano, pale ambapo pragmatiki hudhibiti semantiki nayo semantiki ikadhibiti sintaksia. Kwa njia hii, SAM ina uhusiano na taaluma ya semiotiki ambayo hutambulisha tanzu za sintaksia, semantiki na pragmatiki (Tazama §1.1). Sarufi Amilishi Mfumo hushikilia kuwa, lugha haiwezi kueleweka kikamilifu bila kuzingatia maswala ya kipragmatiki. Ili kukidhi mahitaji haya, SAM imetambua amali tatu za maana.

#### 1.8.2.2 Amali za Maana

Amali za maana zimebainishwa na aina tatu za maana: maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi (Halliday 1994). Aina hizi za maana hazitumiki kila moja pekee bali hutumika sambamba katika kueleza maana. Amali zote zina umuhimu sawa kwa vile huunda maana zilizo na uhusiano.

Maana dhanishi huwasilisha uwezo wa msemaji wa kutambua mambo. Maana dhanishi ndiyo hubeba maudhui katika lugha. Kupitia kwa maana dhanishi, lugha husimba tajriba za kitamaduni na kijamii na msemaji akasimba tajriba zake binafsi. Maana dhanishi hutuwezesha kuelewa na kueleza ujuzi na tajriba kwa jumla.

Maana tagusani ni maana jamilishi na huhusisha kitengo tangamanishi cha matumizi ya lugha kutegemea vikwazo vya kijamii. Maana tagusani huonyesha uhusiano kati ya msemaji na mlengwa na huwafaa wasemaji wa lugha katika kufasili na kutafsiri wajibu na dhima za kijamii. Kupitia kwa maana tagusani, watumizi wa lugha huweza kuasisi, kuimarisha, na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii. Maana tagusani inabainika kama amali tekelezi ya lugha ambayo inazingatia matumizi ya lugha kama tendo la usemi. Msemaji ni mshirika wa tendo la usemi, kwa namna ambavyo anajiingiza katika muktadha wa hali halisi ya mawasiliano, ili aweze kujieleza na kueleweka. Msemaji ataeleweka kwa kugusa mielekeo, imani, tabia, falsafa, hisia, pamoja na mawazo ya mlengwa. Mtagusano kimawazo utahitaji mantiki ya maana dhanishi. Uwasilishaji wa maana dhanishi na maana tagusani hutegemea amali ya tatu ambayo ni maana matinishi.

Maana matinishi hurejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa mawasiliano ya lugha. Maana matinishi humpa msemaji vifaa vya kuwasilisha ujumbe kwa njia ya usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha na hali ya mawasiliano. Maana matinishi hutekeleza jukumu la uwasilishi. Kupitia kwa ushirikiano wa maana dhanishi kwa upande mmoja na maana tagusani kwa upande mwingine maana matinishi hufanikiwa kuwakilisha ujumbe kwa namna inavyodhamiriwa.

Maana dhanishi na maana tagusani kwa pamoja hushirikisha kanuni bia za matumizi ya lugha, ambayo ni kudhibiti mazingira yetu maishani na kutumia akili zetu. Amali hizi mbili ni za msingi katika lugha zote ulimwenguni. Maana dhanishi ina uwiano na utanzu wa semantiki nayo maana tagusani ina uwiano na utanzu wa pragmatiki. Pragmatiki ni utanzu wa kisarufi ambao hauwezi kupuuzwa katika kuelewa mawasiliano. Uelewaji wa mawasiliano utategemea aina tatu za maana ambazo hujihusisha na amali za vishazi.

**1.8.2.3 Amali za Kishazi**

Nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo (SAM) hutazama kishazi kama kipashio kidogo zaidi au matini ya kimsingi ambayo hutumiwa kuchunguza na kuchanganua lugha. Kishazi katika muktadha huu ni sentensi sahili. Mtazamo wa SAM huwasilisha amali tatu za kishazi:

1. Kishazi kama ujumbe huwa na jukumu la mawasiliano katika kila lugha. Kishazi hiki kina mtazamo wa kisemantiki unaolingana na maana dhanishi.

2. Kishazi kama upokezano ni mtazamo wa kipragmatiki unaolingana na maana tagusani na ambao hushirikisha mahusiano kati ya msemaji/mwandishi na hadhira.
3. Kishazi kama uwakilishi ni mtazamo wa kisintaksia unaolingana na maana matinishi.

Mitazamo mitatu ya kishazi inawiana yenyewe, na vilevile na amali za maana na taaluma zinazojumuika, na kwa hivyo kuna utawalio kamili katika Sarufi Amilishi Mfumo. Uwiano huo umeendelezwa katika nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu (UUJ). Mbali na mihimili ya UUJ, mihimili ya SAM ilifanikisha utafiti. Katika mhimili wa muundo wa sarufi, utanzu wa pragmatiki ulitusaidia katika kuchunguza matumizi ya vihisishi katika muktadha wa mawasiliano. Mhimili wa amali za maana ulitumika katika kuelezea matumizi ya vihisishi, na mwisho, mhimili wa amali za kishazi ulihusika katika kuchunguza data lengwa ya utafiti ambayo ilikuwa vihisishi ambavyo huwakilisha semi kamilifu. Semi hizi zilichukuliwa kama vishazi huru.

Taarifa kuhusu Sarufi Amilishi Mfumo imetambulisha mihimili mitatu ya muundo wa kisarufi, amali za maana, na amali za kishazi. Mihimili yote mitatu ina uwiano na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu. Uwiano wa Sarufi Amilishi Mfumo na Uchanganuzi Usemi Jadilifu ni msingi thabiti wa mbinu za utafiti.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Utafiti ulijikita katika mawanda mawili makuu: utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulizingatia usomaji wa vitabu, majarida, na tasnifu kwa lengo la kujaliza taarifa kuhusu kihisishi kwa jumla. Aidha, vitabu teule vilisomwa kuhusu nadharia za Uchanganuzi Usemi Jadilifu na Sarufi Amilishi Mfumo kwa minajili ya kuimarisha weledi wa misingi ya nadharia. Utafiti wa maktabani ndio uliokuwa msingi wa kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu mada. Mtandao pia ulitufaa katika kupata hoja zaidi kuhusu kihisishi. Kwa ujumla, utafiti wa maktabani ulikuwa msingi wa utafiti wa nyanjani.

Utafiti wa nyanjani ulidhamiria kupata data msingi kuhusu kihisishi cha Kiswahili. Kwa njia makusudi, utafiti wa nyanjani ulizingatia namna kihisishi cha Kiswahili kinavyotumika katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano. Kwa jumla utafiti ulihusisha mbinu za aina tatu: mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchanganua data, na mbinu za kuwasilisha utafiti.

### 1.9.1 Eneo la Utafiti

Mji wa Mombasa ndio ulikuwa eneo la utafiti wa nyanjani. Mji huu uliteuliwa kwa sababu ni mojawapo wa miji mikuu nchini na una watu kutoka janibu mbalimbali ambao huzungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza ama kama lugha yao ya pili. Kiswahili kinachozungumzwa Mombasa pia hakijaathiriwa sana na lugha zingine ikilinganishwa na miji mingine mikuu kama vile Nairobi.

### 1.9.2 Sampuli na Usampulishaji

Data lengwa ya utafiti huu ilikuwa vishazi huru vya Kiswahili ambavyo huwakilisha au hujumuisha kihisishi. Nyanjani, vishazi vyenye vihisishi vilikusanywa kutoka kwa mazungumzo ya kawaida baina ya watu. Mtafiti alitumia sampuli makusudi kuteua makundi mbalimbali yaliyotafitiwa ikizingatiwa kuwa vihisishi hutokea ghafla katika shughuli mbalimbali za watu katika maisha yao ya kila siku. Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli makusudi hutokana na uteuzi wa kimakusudi ambapo mtafiti huchagua vipengele ambavyo hutumiwa kama sampuli kuwakilisha populesheni. Mtafiti pia alitumia sampuli viwango na makusudi kuwateua wahojiwa. Kothari (keshatajwa) anasema kuwa, sampuli viwango hutumika katika kugawa watu husika katika viwango kwa misingi ya umri, vyeo au elimu. Jumla ya wahojiwa thelathini waliteuliwa kwa kuzingatia vigezo vya umri, jinsia na lugha. Makundi ya wahojiwa yaliwakilisha watoto wa shule za msingi, vijana wa shule za upili na watu wazima.

Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ni usampulishaji faafu ambayo kulingana na Mugenda (2013) hutumika katika tafiti ambazo masuala yanayotafitiwa ni ya kijumla na mtu yeyote wa kawaida anaweza kuchangia. Mtafiti alizuru masoko ya Kongowea Mwembe Tayari, na Marikiti ambayo ni masoko makuu na yanaaminika kuhudhuriwa na watu wengi. Utafiti pia ulifanywa katika Shule ya Msingi ya Star of the Sea na Shule ya Upili ya Tudor mjini Mombasa. Shule hizi ziliteuliwa kwa misingi ya kuwa ni shule za serikali na inaaminika kuwa wakati wa michezo wanafunzi huzungumza Kiswahili. Data pia ilikusanywa kutoka katika mitaa mbalimbali ya mji wa Mombasa. Mtafiti alikusanya

data kwa kuwahoji watafitiwa na pia kwa kutazama na kusikiliza na kisha kunakili vishazi vyenye vihisishi.

Kitovu kingine cha data kilikuwa kamusi. Mtafiti alizalisha data msingi ya utafiti kutoka kwa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI 2013). Uteuzi wa vihisishi katika kamusi ulizingatia mbinu makusudi. Vihisishi viliteuliwa kimakusudi ili kutumika kama data msingi katika uainishaji na ubainishaji wa maumbo. Kwa jumla vihisishi mia moja hamsini na mbili ambavyo ni idadi jumlifu ya vihisishi katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* vilitumika katika utafiti.

### 1.9.3 Mbinu za Kukusanya Data

Data ilikusanywa kupitia usomaji, uchunzaji na mahojiano. Mtafiti aliwateua wasaidizi wawili waliomsaidia katika kukusanya data. Usomaji ulihusu udurusu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ili kudondoa vihisishi vilivyotumika kama data msingi nyanjani. Baada ya kusoma, mtafiti alinukuu vihisishi vilivyoteuliwa. Vihisishi hivi vilitumiwa na wahojiwa wakati wa utamkaji na pia katika kutambua vihisishi kwenye mazungumzo ya watu mbalimbali kwa kutumia mbinu ya uchunzaji.

Mbinu ya uchunzaji humwezesha mtafiti kutazama matukio mbalimbali katika mazingira husika. Nyanjani, mtafiti alitazama na kusikiliza mazungumzo ya watu katika shughuli zao za kila siku na kunakili vishazi venye vihisishi vilivyojitokeza katika mazungumzo

hayo. Vihisishi vilinakiliwa kwenye simu na kisha baadaye kutolewa kwenye simu na kunakiliwa kwenye daftari.

Katika mbinu ya mahojiano, mtafiti aliwahoji watafitiwa thelathini ana kwa ana kwa kutumia kiongozi cha mahojiano. Wahojiwa walihitajika kutaja vihisishi vinavyotumika katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano. Majibu ya wahojiwa yalinakiliwa kwenye daftari. Wahojiwa pia walihitajika kuvitamka vihisishi mbalimbali katika tungo ili maumbo ya vihisishi hivyo pamoja na tonisho yaweze kubainishwa. Mbinu tatu za ukusanyaji data ziliteuliwa ili kupata data toshelevu. Kariuki (2012) akimnukuu Wiersma (1986) anasema kwamba, kutumia mbinu nyingi za kukusanya data kwa njia elekevu kutakuwa na manufaa ya kurutubisha mbinu za uchanganuzi wa data.

### 1.9.4 Vifaa vya Utafiti

Kifaa cha utafiti ni kitu chochote kinachotumiwa ili kuwezesha kupatikana kwa data inayohitajika katika utafiti. Utafiti huu ulihitaji vifaa vifuatavyo katika kukusanya data: kiongozi cha mahojiano ambacho kilimwongoza mtafiti katika kuwahoji wahojiwa na kalamu na daftari na pia simu kwa minajili ya kunakili vihisishi na vishazi vyenye vihisishi vilivyotumika katika mazungumzo na katika mahojiano.

### 1.9.5 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kabla ya kwenda nyanjani. Nyanjani, kibali cha utafiti

kiliwasilishwa kwa mkuu wa jimbo la Mombasa na mkuu wa elimu wa jimbo hilo waliotoa idhini ya kufanya utafiti. Mtafiti pia aliwahakikishia watafitiwa kudumishwa kwa heshima na kuwaarifu kuhusu kushiriki kwao katika utafiti. Wasaidizi katika utafiti walipewa mafunzo ya jinsi ya kufanya utafiti na kuwa na maadili nyanjani.

### 1.9.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulizingatia hatua tatu kutegemea malengo ya utafiti. Katika hatua ya kwanza, data yote ya utafiti iliainishwa kisha kihisishi cha Kiswahili kuwekwa katika kategoria mbalimbali: msingi, upili, mkopo, na hisia na kupangwa kwenye majedwali. Hatua ya pili ilihusisha kuchanganua umbo la kihisishi cha Kiswahili ambapo vihisishi vilitumiwa kama mifano. Vihisishi vyenye maumbo yanayofanana viliwekwa pamoja na kuorodheshwa. Maumbo haya yalichanganuliwa kwa kutumia vigezo vya kifonolojia, kimofolojia, na kisintaksia kama vile silabi, mpangilio wa konsonanti vokali, tonisho na kundi neno.

Hatua ya tatu ilishughulika na uchanganuzi wa vihisishi kutegemea matumizi yake katika miktadha. Hatua hii ilitarajiwa kudhihirisha matumizi ya kihisishi cha Kiswahili kwa kuzingatia mihimili ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu na Sarufi Amilishi Mfumo. Mihimili ya kinadharia ilimsaidia mtafiti katika kuchunguza dhima za kipragmatiki katika kihisishi cha Kiswahili, pamoja na kuwakilisha data za utafiti.

### 1.9.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Kimsingi, utafiti umewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo yamehimiliwa kwa mifano na majedwali. Taarifa muhimu inahusu maumbo na matumizi ya kipragmatiki, hasa dhima ya kimawasiliano. Utafiti umewasilishwa kwa sura nne zenye taarifa zifuatazo: utangulizi, maumbo ya kihisishi, matumizi ya kihisishi cha Kiswahili, na hitimisho.

Sura ya kwanza imeweka msingi wa utafiti kwa kuegemea taarifa zifuatazo: usuli wa utafiti, swala la utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada, maswali na malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili itashughulikia maumbo ya kihisishi cha Kiswahili.

# SURA YA PILI

# MAUMBO YA KIHISISHI CHA KISWAHILI

## 2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza ilitambulisha mada ya utafiti ambayo ni Pragmatiki ya Kihisishi cha Kiswahili. Sehemu ya upeo na mipaka ya utafiti katika sura ya kwanza ilirejelea umbo la kihisishi cha Kiswahili kwa kudokeza jinsi dhima ya kipragmatiki ya tonisho ilivyotumika katika kusawiri maumbo ya kihisishi (Tazama § 1.5). Vilevile katika sehemu ya tahakiki ya maandishi, maelezo kuhusu umbo la kihisishi yalijitokeza katika utafiti wa Jovanovic (2004) aliyeshughulikia umbo la kihisishi cha Kiingereza (Tazama § 1.7). Sura hii ya pili imechanganua maumbo mbalimbali ya kihisishi cha Kiswahili kwa lengo la kueleza vigezo vilivyotumika katika uundaji wa maumbo haya. Umbo hurejelea mpangilio wa vipashio vya hadhi moja katika neno au kipashio kikubwa zaidi**.** Maumbo ya kihisishi yalishughulikiwa kuhusiana na tanzu tatu za kisarufi ambazo ni fonolojia, mofolojia, na sintaksia.

## 2.1 Maumbo ya Kifonolojia

Umbo la kifonolojia huhusisha idadi ya silabi na ruwaza za tonisho. Ruwaza za tonisho ni vipashio vya fonolojia vinavyohusu fonolojia arudhi. Silabi ni kiungo cha neno kinachobainika kifonetiki, na kinachojumuisha sauti ya vokali au konsonanti silabi. Idadi ya silabi katika kihisishi ilifafanuliwa kwa kurejelea umbo la silabi moja na umbo la silabi nyingi.

### 2.1.1 Umbo la Silabi Moja

Baadhi ya vihisishi vya Kiswahili vimeundwa kwa silabi moja. Umbo la silabi moja linajidhihirisha kwa maumbo finyu ya konsonanti vokali, vokali pekee na konsonanti silabi ambayo huwa nazali (N). Maumbo ya konsonanti vokali hujitokeza kwa wingi katika umbo la silabi moja ikilinganishwa na maumbo ya konsonanti pekee au vokali pekee.

#### 2.1.1.1 Umbo la Konsonanti Vokali

Umbo la konsonanti vokali ndilo umbo la kawaida katika matumizi ya lugha kwa jumla. Silabi ya umbo la konsonanti vokali ni silabi bora zaidi ikilinganishwa na aina nyingine za silabi. Konsonanti vokali ni silabi bia kwa vile hupatikana katika sarufi ya lugha zote ulimwenguni na hupendelewa na watu wengi. Konsonanti vokali ni silabi wazi ambayo hutumika sana katika Kiswahili. Vihisishi vya silabi moja ni rahisi katika utamkaji wake kinyume na vihisishi vya silabi nyingi kwa vile ni vifupi. Maumbo {*do*}, {*lo*}, {*po*}, na {*la*} ni vihisishi vya silabi moja ambavyo ni vihisishi kamilifu. Kutokana na utafiti imebainika kuwa, vihisishi vyote vya silabi moja vyenye maumbo ya konsonanti vokali ni vya msingi ila kihisishi {*la*} ambacho ni cha mkopo. Mifano ya maumbo ya konsonanti vokali inadhihirika katika Jedwali 2.1

**Jedwali 2.1: Vihisishi vya Konsonanti Vokali**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Do | *Do!* Mtoto wewe kumbe husikii eeeh! |
| 2 | Lo | *Lo!* Nastahili kuwa mkutanoni mie. |
| 3 | Po | *Po!* Abdi wewe kila mara wawaachia kina Nuru mpira, wataka watushinde? |
| 4 | La | *La!* Alisafiri leo kwenda kwa nyanya. |

Mifano iliyo katika Jedwali 2.1 inaonyesha maumbo ya vihisishi ambavyo vimeundwa kwa silabi moja za konsonanti vokali. Katika mfano wa kwanza msemaji anatumia *do* kuonyesha mshangao kwa tabia za mtoto. Pili, *lo* inaonyesha mshtuko ambapo dada mmoja anashtuka anapokumbuka kuwa alistahili kuwa mkutanoni. Kihisishi *po* kimetumika na mtoto kuonyesha dharau kwa mwenzake anayecheza mpira vibaya. Mwisho, *la* inatumika na mtoto kukataa kuwa mamake hayupo nyumbani. Umbo la silabi moja pia huwakilishwa na umbo finyu la vokali pekee.

#### 2.1.1.2 Umbo la Vokali Pekee

Vokali ina uwezo wa kuwakilisha silabi kamili. Izingatiwe kuwa, vokali pekee hutamkika kwa urahisi kwa vile zinapotamkwa hakuna hewa inayozuiliwa popote katika mkondo wa hewa. Vihisishi vinapoundwa kwa vokali pekee zinazofanana huwa maumbo ya silabi

moja, kwa mfano *$aa$* na *$ee$*. Maumbo haya hutamkika kama silabi moja yenye wakaa. Kihisishi *$ei$* kina vokali changamano. Vokali changamano hapa imewakilishwa na herufi mbili tofauti. Vihisishi vya umbo la vokali pekee vinabainishwa katika Jedwali 2.2.

**Jedwali 2.2: Vihisishi vya Vokali Pekee**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | a [ α] | *A,* Vuka basi! |
| 2 | aa [α:] | *Aaa!* Umeyasikia ati, Zainabu kapewa talaka. |
| 3 | ee [ε:] | *Ee!* Wacha aje ajue mambo ya nauli. |
| 4 | ei [εi] | *Ei!* Wee! Ati mzee Gitau? |

Kwa kawaida vokali hufanya konsonanti isikike katika matamshi. Vihisishi vya vokali pekee vinawakilishwa na vokali: /*e*/ na /*i*/ ambazo ni vokali za mbele na /*a*/ ambayo ni vokali ya kati. Vihisishi vinavyoundwa kwa vokali pekee ni vya kategoria ya vihisishi msingi. Vokali sahili kama vile /*a*/ ni silabi moja kwa vile ni silabi wazi. Mbali na umbo la vokali pekee, kihisishi cha Kiswahili kina silabi moja yenye umbo la konsonanti silabi.

#### 2.1.1.3 Umbo la Konsonanti Silabi

Baadhi ya vihisishi huwa na maumbo ya konsonanti silabi. Konsonanti silabi ni konsonanti ambayo huunda silabi kivyake bila vokali (Kihore, Massamba na Msanjila, 2003). Maumbo ya konsonanti silabi ya vihisishi yamezua mjadala wa wasomi kuhusu ikiwa vihisishi ni maneno kamilifu au la. Ameka (1992a) anasema kuwa, kulingana na mfumo wa sauti katika lugha, vihisishi vya konsonanti pekee havichukuliwi kama maneno. Hata hivyo anasisitiza kuwa, ukiukaji wa kifonolojia usiwe kigezo cha kupinga vihisishi kama maneno. Sababu kuu ni kuwa, kuna vihisishi vingine ambavyo hufuata ruwaza za sauti za mfumo wa lugha ambao ni konsonanti vokali. Utafiti huu umetambua maumbo ya konsonanti silabi kama vihisishi kwa vile ni semi zinazojisimamia na zenye maana.

Katika Kiswahili, konsonanti inayotumika pekee kama vihisishi ni konsonanti nazali /m/. Ingawa kwa kawaida katika Kiswahili maneno yenye asili ya Kibantu huundwa kwa silabi wazi, kuna sauti nyingine ambazo ni konsonanti zenye sifa ya usilabi. Sauti nazali hutamkwa kwa upekee kama silabi. Sauti /m/ hutumika kuunda vihisishi {*mmm*} na {*mmh*}. Mbali na sauti nazali /m/, sauti /s/ imetumika kuunda kihisishi {*sss*} ambacho ni kihisishi mkopo. Umbo la konsonanti silabi huunda vihisishi kamilifu vinavyotumika katika Kiswahili. Vihisishi vilivyoundwa kwa konsonanti pekee vimebainishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.3: Vihisishi vya Konsonanti Silabi**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Mmm | *Mmm,* ni mlevi yule, achana naye. |
| 2 | Mmh | *Mmh,* ndivyo ilivyo. |
| 3 | Sss | *Sssss!* |

Maumbo {*mmm*}, {*mmh*}, na {*sss*} ni vihisishi kamili ambavyo vimeundwa kwa konsonanti pekee. Vihisishi {*mmm*} na {*mmh*} ni vihisishi msingi ilihali {*sss*} ni kihisishi mkopo chenye maana ya kuwanyamazisha wanaopiga kelele. Vihisishi {*mmm*}, {*mmh*}, na {*sss*} ni maumbo ya silabi moja. Katika utamkaji, vihisishi hivi hutamkwa kama silabi moja yenye wakaa. Vihisishi {*mmm*} na {*mmh*} vimeundwa kwa sauti nazali /m/ na vinatamkika kwa urahisi bila kuambatishwa vokali. Silabi $m$ ni kawaida kuipata na kwa hivyo kuwa na uasilia katika kuitamka. Kihisishi {*sss*} kinapotamkwa husikika kama kinachojumuisha vokali /i/. Wakati mwingine {*sss*} hutamkwa pamoja na ishara ya kidole mdomoni hasa kama anayeambiwa anyamaze ni mtoto. Mbali na maumbo ya silabi moja, kihisishi cha Kiswahili pia hujidhihirisha katika umbo la silabi nyingi.

### 2.1.2 Umbo la Silabi Nyingi

Vihisishi vya silabi nyingi hutumika kwa wingi ikilinganishwa na vihisishi vya silabi moja. Utafiti umeshughulikia umbo la silabi nyingi kuanzia silabi mbili hadi silabi nne. Mbali na idadi zilizotajwa, vihisishi vya silabi zaidi ya nne pia vilibainishwa lakini

vilikuwa nadra. Umbo la silabi nyingi ni la maumbo ya silabi mbili, silabi tatu, na silabi nne. Jedwali 2.4 linabainisha vihisishi *hata*, *poko*, na *toba* ambavyo vina silabi mbilimbili.

**Jedwali 2.4 Vihisishi vya Silabi Mbili**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Hata! | *Hata!* Hatujakutana. |
| 2 | Poko! | Sitakwambia kitu *poko!* (akitema mate) |
| 3 | Toba! | Yarabi! *Toba!* Roho yangu. Taratibu! |

Vihisishi vilivyo katika Jedwali 2.4 vina silabi mbilimbili. Ilibainika kuwa vihisishi vya silabi mbili ni vingi kwa vile ni takribani thuluthi moja ya vihisishi vyote vilivyoshughulikiwa. Kihisishi *hata* kina silabi mbili /*ha*/ na /*ta*/. *Hata* inaonyesha kukataa kwa msemaji kwa anayoulizwa. /*Po*$*ko*/ ni kihisishi cha dharau. Katika mfano wa pili, msemaji amekasirishwa na msikilizaji kwa kutoboa siri zao na kwa hivyo kwa dharau anamsisitizia mwenzake kwa kutumia *poko* kuwa hawezi akamwambia kitu tena. Kihisishi /*to*$*ba*/ kinadhihirisha mshtuko wa msemaji baada ya kuepuka ajali.

Vihisishi vya silabi mbili huundwa kwa mpangilio wa konsonanti vokali, konsonanti vokali na havikosi uwiano na vihisishi vya silabi tatu. Umbo la silabi tatu linajidhihirisha katika vihisishi: *hewala, labeka,* na *kelele* ambavyo vinaonyeshwa katika Jedwali 2.5. Vihisishi vya silabi tatu vilevile vinafuata mpangilio wa konsonanti vokali.

**Jedwali 2.5: Vihisishi vya Silabi Tatu**

| | Kihisishi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1 | Hewala! | *Hewala!* Nenda. |
| 2 | Labeka! | *Labeka* mwalimu. |
| 3 | Kelele! | *Kelele!* (Shule ya msingi) |

Kihisishi /*he*$*wa*$*la*/ kina silabi tatu, na katika muktadha huu kimetumika na msemaji kumridhia msemewa aende alikokuwa akienda. Mwanafunzi anaitwa na mwalimu na kuitika kwa /*la*$*be*$*ka*/. Katika kutamka kihisishi *labeka*, silabi ya mwisho /*ka/* husikika kama [*k*]. Silabi tatu pia zinabainika katika kihisishi /*ke*$*le*$*le*/ ambacho ni cha kuwanyamazisha wanaopiga kelele. Fauka ya vihisishi vya silabi tatu, umbo la silabi nne hujidhihirisha katika kihisishi cha Kiswahili. Maumbo *ripuripu, jazakalla,* na *tafadhali* ni mifano ya vihisishi vya silabi nne. Tazama Jedwali 2.6.

**Jedwali 2.6: Vihisishi vya Silabi Nne**

| | Kihisishi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1 | Ripuripu! | *Ripuripu* hureee |
| 2 | Jazakalla! | *Jazakalla* kheri. |
| 3 | Tafadhali! | Naam, ishirini, nitafutie *tafadhali.* |

Maumbo ya silabi nne hubainika sana katika vihisishi mkopo vya Kiswahili. Kihisishi /*ja*$*za*$*ka*$*lla*/ hutumiwa kwa maana ya Mungu akuzidishie. Katika mfano huu, kijana mmoja anampa mzee kiti aketi katika mkutano, naye mzee anamwambia kijana {*jazakalla*} kheri kwa maana kuwa, Mungu na amzidishie heri. Watoto uwanjani wanashangilia na kuipa timu yao nguvu za kushinda kwa kutumia kihisishi /*ri*$*pu*$*ri*$*pu*/. Ingawaje kihisishi {*ripuripu*} kinaonyesha umbo la kujirudia {*ripu*} na {*ripu*}, hakiwezi kutenganishwa, kinadhihirisha maana kusudiwa tu kinapotumika kama *ripuripu*. Kihisishi */ta*$*fa*$*dha*$*li*/ hutumiwa na mtu anayetaka kutendewa jambo kwa hisani. Kwa mfano, mama anatumia {*tafadhali*} kuaagiza bidhaa na kumwomba muuzaji kumtafutia bidhaa anazohitaji.


Vihisishi vya silabi zaidi ya nne pia vilibainika. Vihisishi vya kuomba dua vya /*a*$*la*$*ha*$*m*$*du*$*li*$*lla*$*hi*/ na /*au*$*dhu*$*bi*$*la*$*hi*/ vyenye silabi nane na tano mtawalia vilitambuliwa. Kihisishi /*sha*$*shi*$*ma*$*mi*$*shi*/ chenye umbo la silabi tano kilibainika pia lakini matumizi yake hayakujitokeza nyanjani. {*Shashimamishi*} ni kihisishi cha mkopo ambacho kina maana ya tamko ambalo huelezea hali ya kudharaulika. Watafitiwa hawakuwa na ufahamu wa kihisishi {*shashimamishi*} ambacho hutumika kuonyesha dharau. Wengi wa watafitiwa walikiri kuwa hawajawahi kukisikia wala kukitumia kihisishi {*shashimamishi*}. Kihisishi {*shashimamishi*} hakikufahamika na wenyeji watafitiwa pengine kwa vile ni cha mkopo. Data iliyotegemewa kuhusu kihisishi {*shashimamishi*} ilikuwa data msingi kutoka kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*

Sehemu hii imejadili maumbo mbalimbali ya kihisishi kwa kurejelea idadi ya silabi. Maumbo ya silabi moja na maumbo ya silabi nyingi yamechunguzwa. Silabi ni muhimu kwani huunda maneno yanayotumika katika mawasiliano. Imedhihirika kuwa vihisishi vya mpangilio wa konsonanti vokali katika umbo la silabi moja na hata umbo la silabi nyingi ni vingi. Jambo ambalo linafanana na mahitimisho katika utafiti wa Jovanovic (2004) anayesema kuwa kifonolojia vihisishi vingi vya Kiingereza ni vya mpangilio wa konsonanti vokali (Tazama § 1.7.1) Mpangilio wa silabi katika kihisishi ambao umezungumziwa hujidhihirisha pia katika umbo la kiarudhi la kihisishi.

### 2.1.3 Umbo la Kiarudhi

Arudhi husimamia muundo, maumbo na mahusiano mwafaka ya vipashio vya sauti vinavyozidi foni (Kindija 2012). Sifa arudhi ni sura ambazo huweza kutumika katika kutofautisha maumbo linganifu. Kwa kawaida, matumizi ya sifa arudhi hurejelea wakaa, kidatu na shadda. Umbo la kiarudhi la kihisishi linategemea silabi na tonisho. Tonisho huwakilisha ruwaza za kidatu. Kidatu ni sifa ya msikiko sauti ambayo humwezesha msemaji kubadili kiwango chake cha sauti katika usemaji. Hivyo basi kidatu ni kiwango cha juu, cha kati, au cha chini cha msikiko wa sauti katika usemaji. Halliday na Matthiessen (2004) katika Sarufi Amilishi Mfumo wanawasilisha aina tano za kidatu: chini (CH), juu (JU), kati (KA), chini-juu (CH-JU) na juu-chini (JU-CH) kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.7

**Jedwali 2.7: Aina za Kidatu**

| | **Ishara** | **Viwango** | **Matumizi** | **Viwango katika Matumizi** |
|---|---|---|---|---|
| 1 |  | Chini | *Jamani* poleni, | CH-JU-CH [*jamani*] |
| 2 |  | Juu | *Aka* kumbe we ni mwizi! | CH-JU [*aka*] |
| 3 |  | Kati | *Ati* waringa, waringia nini? | KA-KA [*ati*] |
| 4 |  | Chini – juu | *Aka*, mi sijaiba. | CH-JU [*aka*] |
| 5 |  | Juu – chini | O*ooh,* ndo maana wafungua ile akaunti? | JU-CH [*oooh*] |

Kwa Mujibu wa Halliday na Matthiessen (2004: 141)

Umbo la kihisishi huweza kuathiriwa na aina ya kidatu. Mbaabu (1992) anasema kuwa vihisishi hutamkwa kwa sauti, kwa haraka au kwa utaratibu kuliko maneno mengine ya kawaida. Kidatu huathiri ujumbe wa msemaji kwa msikilizaji. Katika Jedwali 2.7, {*Jamani*} imetamkwa kwa kidato cha chini kuonyesha huruma kwa yaliyowapata warejelewa. Kidatu cha juu katika kutamka {*aka*} kinaashiria mshangao. Ili kumdhalilisha mtu, {*ati*} inatamkwa kwa kidato cha kati. Msemaji katika mfano wa tatu anayadharaulia mbali maringo ya msichana mmoja. Kidatu kimeanzia chini na kupanda

katika kutamka {*aka*} katika mfano wa nne kuonyesha kukataa. Msikilizaji anakataa kuwa hajaiba. Mwisho, {*oooh*} inapotamkwa kwa kidatu kinachoanzia juu na kushuka inaonyesha kuridhia jambo fulani.

Kidatu hupewa upeo zaidi na wakaa.Vihisishi huweza kutamkwa kwa kurefusha silabi ya mwisho. Vihisishi ambavyo silabi zake zimerefushwa hutamkwa kwa kidatu cha juu ili kudhihirisha ujumbe unaokusudiwa. Kidatu kinachoandamana na wakaa huwa cha kiwango cha juu jinsi inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.8: Vihisishi vyenye Wakaa**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Jamaniii [jamani:] | *Jamaniii!* Nisaidieni! Naumia. |
| 2 | Hureeee [huree:] | *Hureeee!* Tumeshinda! |
| 3 | Alaaa [ala:] | *Alaaa!* Wewe ndiye Martin? |

Maumbo katika Jedwali 2.8 ni mifano ya vihisishi vinavyotamkwa kwa kidatu cha juu pamoja na wakaa. Kihisishi {*jamaniii*} katika mfano wa kwanza kimetumika na mtu aliye taabani kuitisha msaada. {*Jamani*} inapotamkwa kwa wakaa na kidatu cha juu, inaonyesha msemaji anahitaji msaada wa dharura kinyume na ikitamkwa katika hali ya kawaida kwa mfano: *Jamani nisaidieni*. Katika mfano huu, msemaji anaomba msaada lakini si wa dharura. Kidatu cha juu katika kutamka {*hureeee*} kinaonyesha msisitizo katika kushangilia na kumalizika kwa mchezo. Msisitizo huu unadhihirisha furaha

waliyonayo washindi. Kihisishi {*alaaa*} kimetamkwa kwa wakaa na kidatu cha juu kuonyesha kukubali kwa msemaji kuwa sasa anatambua kuwa huyo ndiye Martin. Kihisishi {*alaaa*} ni tofauti na kihisishi {*ala*} cha kawaida ambacho hutamkwa kwa kidatu cha juu kuonyesha mshtuko.

Ubainishaji wa maumbo ya kifonolojia umeonyesha kuwa, kifonolojia vihisishi hudhihirisha umbo la silabi moja, umbo la silabi nyingi, na umbo la kiarudhi. Umbo la silabi moja limejitokeza katika maumbo finyu ya konsonanti vokali, vokali pekee na konsonanti silabi. Kihisishi cha Kiswahili pia kimedhihirisha kuwa na silabi mbili, silabi tatu, silabi nne, silabi tano na hata silabi nane. Imebainika kuwa, sifa arudhi huchangia katika kutofautisha maana ya vihisishi. Maumbo ya kifonolojia hayakosi uwiano na maumbo ya kimofolojia

## 2.2 Maumbo ya Kimofolojia

Umbo la kimofolojia hubainika kupitia kwa mpangilio wa mofu katika neno. Mofu ni kipashio cha kimaumbo kinachowakilisha mofimu. Mofu huhusisha viambishi na mzizi katika neno. Mofimu ni kipashio kidogo amilifu katika maumbo ya maneno (Kihore, Massamba na Msanjila 2003). Maumbo ya kimofolojia yaliyobainika ni matatu: umbo la mofimu moja, umbo la mofimu mbili, na umbo la mofimu changamano.

### 2.2.1 Umbo la Mofimu Moja

Kimsingi, vihisishi vya Kiswahili huwa ni mofimu moja ambayo haiambishwi, kwa hivyo ni mofimu huru. Mofimu huru haiwezi kutenganishwa zaidi katika vipashio vidogo vidogo bila kupoteza maana. Ilibainika kuwa vihisishi viliweza kujisimamia na kutoa maana kamilifu. Umbo la mofimu moja hujibainisha katika mofimu sahili na mofimu ambatano. Vihisishi {*hongera*}, {*katu*}, na {*taibu*} ni maumbo ya mofimu moja moja sahili. Maumbo haya hayawezi kugawanyika zaidi na hubeba maana kisarufi. Umbo la mofimu moja sahili linatambulishwa katika Jedwali 2.9.

**Jedwali 2.9: Vihisishi vya Mofimu Moja Sahili**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Hongera! | *Hongera* kwa kupata mchumba. |
| 2 | Katu! | Wallahi mimi sikuamini *katu* ulivyosema. |
| 3 | Taibu! | *Taibu* kaka. |

Maumbo katika jedwali ni mofimu huru ambayo yanaweza kujisimamia. Kihisishi {*hongera*} hutumika katika kumpongeza mtu kwa mafanikio yake. Msemaji anampongeza mwenzake kwa kupata mchumba. Mofimu {*katu*} inaonyesha kukataa kabisa. Msemaji katika mfano wa pili katika Jedwali 2.9, anaapa kuwa hakuamini kabisa aliyoambiwa. Katika kukubali yanayosemwa kihisishi {*taibu*} huweza kutumiwa. Umbo la mofimu moja sahili huwa ni mofimu huru na hukaribiana na umbo la mofimu moja ambatano linalorejelewa katika sehemu ifuatayo.

### 2.2.2 Umbo la Mofimu Moja Ambatano

Mofimu moja inaporudiwa, inaunda umbo la mofimu moja ambatano. Kihisishi kimoja chenye mofimu moja chaweza kurudiwa na kuunda kihisishi chenye mofimu moja ambatano. Wakati mwingine kihisishi kilichoundwa hakibadilishi maana lakini kurudia huku kunakuwa kwa kutilia mkazo au msisitizo kwa yanayosemwa. Jedwali lifuatalo linaonyesha vihisishi *basibasi*, *sawasawa*, na *hodihodi* ambavyo ni vya umbo la mofimu moja ambatano.

**Jedwali 2.10: Umbo la Mofu Moja Ambatano**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Basibasi | *Basibasi* Nimesikia! |
| 2 | Sawasawa | *Sawasawa!* Nitaleta kesho. |
| 3 | Hodihodi | *Hodihodi* wenyewe. |

Mbinu iliyotumiwa katika kuunda maumbo haya ya mofimu moja ambatano inaitwa uradidi. Uradidi ni mbinu ya kurudia maneno. Kihisishi {*basi*} kina maana ya tosha, lakini kinaporudiwa na kuwa {*basibasi*} hudhihirisha msisitizo. Mama anamwambia mtoto aache kulalamika kwa vile ameyasikia malalamishi yake. {*Sawa*} huwa na maana ya ndiyo, lakini kihisishi hiki kinaporudiwa na kuwa {*sawasawa*} kinatumika kutilia mkazo katika kukubali kuwa jambo linalorejelewa litatendwa. Msichana anakumbushwa na mwenzake kuhusu kitabu, naye anakubali na kumsisitizia kwa kutumia {*sawasawa*} kuwa angemletea siku ambayo ingefuata. Kihisishi {*hodihodi*} kimetumika kubisha kwa

himizo ili wenyewe wafungue mlango haraka. Umbo la mofimu moja ambatano halikosi uwiano na umbo la mofimu mbili ambalo limeelezwa katika aya inayofuata.

### 2.2.3 Umbo la Mofimu Mbili

Kwa kawaida vihisishi haviambishwi katika Kiswahili, lakini kuna vihisishi ambavyo hukiuka sheria hii. Baadhi ya vihisishi vya Kiswahili huongezewa viambishi hasa kwa kutegemea matumizi. Kiambishi ni istilahi ambayo hutumiwa hasa katika mofolojia kuelezea kijenzi cha neno ambalo huongezewa katika mizizi ya maneno. Baadhi ya vihisishi huambishwa viambishi awali na vingine huambishwa viambishi tamati ili kuunda kihisishi chenye umbo la mofimu mbili. Vilevile kuna maumbo ya mofimu mbili ambayo hutokana na kuwekwa kwa mofimu mbili au zaidi pamoja kwa mfano, {*wa*}{*tallahi*}, na {*ma*}{*salaale*}jinsi ilivyo katika Jedwali 2.11.

**Jedwali 2.11: Vihisishi vyenye Viambishi Awali**

| | **Kihisishi Kilichoambishwa** |
|---|---|
| 1 | **Wa**tallahi |
| 2 | **Ma**salaale |

Jedwali 2.11 linaonyesha vihisishi vya mofimu mbili ambazo zimetokana na kihisishi kuongezewa kiambishi awali. Utafiti ulibaini kuwa, kihisishi {*tallahi*} ambacho hutumika katika kuapa, kikiongezewa kiambishi awali {*wa*} huonyesha msisitizo zaidi kuwa linalosemwa ni la kweli. Kihisishi msingi {*salaale*} kina maana sawa ya mshangao

na kihisishi mkopo {*ma*}{*salaale*}ambacho kimeongezewa kiambishi {*ma*} mwanzoni. Vihisishi {*tallahi*}, na {*salaale*} vinapoongezewa viambishi awali, vinabadilisha maumbo na kuwa na mofimu mbili: {*wa*}{*tallahi*} na {*ma*}{*salaale*}. Vihisishi vingine huongezewa viambishi mwanzoni ili kusisitiza linalosemwa au hata kuonyesha wingi wa wahusika. Viambishi vinavyoongezwa si vya lazima kwani vihisishi husika vyaweza kutumika kikamilifu bila ya kuambishwa na vikadhihirisha maana iliyokusudiwa.

Jinsi ilivyo na viambishi awali, viambishi tamati pia hubainika katika kihisishi cha Kiswahili. Viambishi tamati huja baada ya kihisishi. Vihisishi vya Kiswahili wakati mwingine huongezewa mofimu tamati {*ni*} ili kuonyesha wingi wa wahusika. Vihisishi {*shikamooni*}, {*karibuni*}, na {*poleni*} ni mfano wa vihisishi vyenye viambishi tamati kama inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 2.12: Vihisishi vyenye Viambishi Tamati**

| | **Wingi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Shikamoo**ni** | *Shikamooni* baba na mama. |
| 2 | Karibu**ni** | Nashukuru! *Karibuni* tena. |
| 3 | Pole**ni** | *Poleni*! Jamani! *Poleni!* |

Vihisishi mbalimbali ambavyo maumbo yake yamebadilishwa kwa kuongezea kiambishi tamati {*ni*} vimedhihirishwa katika Jedwali 2.12. Vihisishi vipya vimebadilisha maumbo kutoka kuwa na mofimu moja hadi mofimu mbili ambazo zinawakilisha mzizi wa

kihisishi na mofimu ya wingi. Katika mfano wa kwanza, mtoto anatumia {*shikamoo*}{*ni*} kuwasabahi wazazi wake kwa pamoja. Katika mfano wa pili, {*karibu*}{*ni*}imetumiwa na mwenyeji kuwaaga wageni waliomtembelea. Kihisishi {*pole*}{*ni*}kimetumika kuwafariji wahusika wengi waliopatwa na msiba. Imebainika kuwa idadi kubwa ya vihisishi vinavyoambishwa {*ni*} ni vya upili yaani vihisishi vinavyoundwa kutokana na kategoria zingine za maneno kama vile nomino na vitenzi.

Mbali na uambishaji, vihisishi vya mofimu mbili vyaweza kuundwa kutokana na mbinu ya uunganishaji. Maumbo haya hutokana na kuunganisha mofimu mbili huru. Mofimu hizi huwa na maana tofauti lakini zinapounganishwa huunda kihisishi kimoja. Vihisishi *Sabalheri, sabalnuru, masalheri,* na *masalnuru,* vina mofimu mbilimbili na hutumika katika maamkizi jinsi inavyodhihirika katika Jedwali 2.13.

**Jedwali 2.13: Vihisishi vya Mofimu Mbili Kutokana na Uunganishaji**

| | **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Sabalheri | *Sabalheri* kaka? |
| 2 | Sabalnuru | *Sabalnuru.* |
| 3 | Masalheri | Hassani, *masalheri?* |
| 4 | Masalnuru | *Masalnuru* Kassim. |

Maumbo yaliyo katika Jedwali 2.13 yameundwa kwa kuunganisha mofimu mbili huru. {*Sabalheri*} ni salamu ya asubuhi. Jibu lake ni {*sabalnuru*}. Vihisishi {*sabalheri*} na {*sabalnuru*} vina mofimu mbilimbili. {*Sabal*} ni neno lenye asili ya Kiarabu kwa maana ya asubuhi, {*heri*} ni hali ya amani, nayo {*nuru*} ni mwanga (Ngugi 2014). Kwa hivyo anayeamkua humtakia mwenzake asubuhi njema yenye amani naye humjibu kuwa awe na asubuhi njema yenye mwanga. {*Masalheri*} ni salamu ya jioni na jibu lake ni {*masalnuru*}. Neno {*masal*} lina asili ya Kiarabu kwa maana ya jioni. Mofimu {*heri*} na {*nuru*} zinadhihirisha maana ya amani na mwanga mtawalia kama ilivyo katika salamu ya asubuhi. Katika salamu ya jioni, anayeamkua anamtakia mwenzake jioni njema yenye amani naye akamtakia jioni njema yenye mwanga. Vihisishi vyenye umbo la mofimu mbili vimejadiliwa katika sehemu hii. Sehemu ifuatayo itarejelea vihisishi vya umbo la mofimu changamano.

### 2.2.4 Umbo la Mofimu Changamano

Vihisishi vya mofimu changamano huundwa kutokana na kuweka vijisehemu mbalimbali vya maneno mawili tofauti au zaidi ili kuunda neno moja lenye mofimu zaidi ya moja. Umbo la mofimu changamano ni tofauti na umbo la mofimu mbili kutokana na uunganishaji kwa vile katika uunganishaji, mofimu mbili huru zinaunganishwa ilihali umbo changamano linaundwa na vijisehemu vya maneno tofauti. Vihisishi *kunani, kulikoni, enyi,* na *ewe* ni mifano ya maumbo ya mofimu changamano jinsi inavyodhihirika katika Jedwali 2.14.

**Jedwali 2.14: Vihisishi vya Mofimu Changamano**

| **Kihisishi** | **Matumizi** |
|---|---|
| Kunani | Mashalla! *Kunani* bwana, jionee mwenyewe! |
| Kulikoni | Maeneo ya Mombasa, Mwembe Tayari, Miritini, tufahamisheni *kulikoni* barabarani |
| Enyi | *Enyi!* Mwaja ama hamji nijipange. |
| Ewe | *Ewe*! Mwenyezi Mungu, tuhurumie haya mafuriko yamezidi. |

Katika mofimu changamano, sehemu ya mwanzo ya neno la kwanza hujumuishwa na sehemu ya mwisho ya neno la pili. Wakati mwingine neno zima laweza kuchukuliwa na kuongezewa mofimu kutoka katika neno la pili. Mbinu inayotumika katika uundaji wa aina hii huitwa uhulutishaji. Kihisishi {*kunani*} ambacho hutumika katika kutaka kujua kinachoendelea, kimeundwa kutokana na mofimu {*kuna* na *nini*}. Kihisishi {*kunani*} kimeundwa kwa kuchukua neno la kwanza ambalo lina mofimu mbili {*ku*} na {*na*} na kuongezea mofimu {*ni*} ya neno la pili. Kihisishi {*kulikoni*} hutumika katika kutaka kufahamu kilichofanyika. {*Kulikoni*} ni kihisishi ambacho ni ufupisho wa *kulikuwa na nini*. Katika kuunda {*kulikoni*}, mofimu tatu za neno la kwanza yaani {*ku*} ya mahali, {*li*} ya wakati na {*ku*} ya mahali zinajumuishwa na mofimu moja {*ni*} ya neno la pili na kuunda kihisishi cha mofimu nne {*ku*}{*li*}{*ko*}{*ni*}. Katika uundaji wa kihisishi {*kulikoni*} kuna michakato fiche ambayo imesababisha kudondoshwa kwa kitenzi {*wa*} na kiunganishi {*na*} na kubadilisha mofimu {*ku*} kuwa {*ko*} ili kuunda kihisishi kipya.

Kihisishi {*Enyi*} ni kifupisho cha {*ee*}{*nyinyi*}. Kihisishi cha mwisho {*ewe*} kimeundwa kutokana na kuunganishwa kwa {*e*} na {*we*} ambazo ni ufupisho wa {*ee*}{*wewe*}. Kihisishi {*ewe*} hutumika katika kuita hasa Mwenyezi Mungu wakati wa maombi na kina mofimu mbili. Umbo la mofimu changamano linahitimisha mjadala kuhusu maumbo ya kimofolojia.

Kimofolojia, maumbo matano yamebainishwa katika sehemu hii kwa kurejelea kigezo cha mofimu. Ifuatayo ni orodha ya maumbo yaliyobainishwa: umbo la mofimu moja sahili, umbo la mofimu moja ambatano, umbo la mofimu mbili kutokana na uambishaji na uunganishaji na umbo la mofimu changamano. Maumbo ya kimofolojia hayakosi uwiano na maumbo ya kisintaksia ambayo yanajadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 2.3 Maumbo ya Kisintaksia

Kimsingi, umbo la kisintaksia hudhihirishwa na mpangilio wa virai katika kihisishi. Kirai hutazamwa kama kundi la maneno ambalo hulenga neno kuu na ambalo kwa pamoja hutekeleza dhima ya kisarufi (Halliday na Matthiessen 2004). Kirai katika Sarufi Zalishi hujulikana kama kundi katika Sarufi Amilishi Mfumo. Utafiti huu ulitumia ‘kundi maneno’ kurejelea kirai kwa mujibu wa nadharia ya utafiti.

#### 2.3.1 Umbo la Kundi la Maneno

Umbo la  kisintaksia la kihisishi cha Kiswahili lilichunguzwa kwa kurejelea kundi neno ambalo hudhihirika katika baadhi ya vihisishi. Vihisishi vya aina hii huundwa kwa

maneno zaidi ya moja. Maumbo ya vihisishi vilivyoundwa yaweza kuwa panuzi ambapo kundi linachomoza maneno mengine au finyizi ambapo kundi lina maneno ya aina moja. Kundi neno huwa na jina bayana zaidi: kundi nomino au kundi hisishi. Katika kundi nomino, neno kuu huwa nomino kwa mfano, *haki ya Mungu*, *hadithi hadithi*, na *salaam aleikum*. Kundi hisishi hutangulizwa kwa kihisishi kwa mfano *la hasha* na *haya haya*. Vihisishi vya umbo la kundi maneno vinadhihirika katika jedwali lililo hapa chini.

**Jedwali 2.15: Vihisishi vya Kundi Maneno**

| | **Kirai Hisishi** | **Matumizi** |
|---|---|---|
| 1 | Haki ya Mungu | *Haki ya Mungu* si mimi. |
| 2 | La hasha | Ali hawezi, *la hasha!* Siye aliyeiba. |
| 3 | Hadithi hadithi | *Hadithi hadithi!* – Hadithi njoo. |
| 4 | Haya haya | *Haya haya!* Bwana utatugonga. |
| 5 | Salaam aleikum | *Salaam aleikum*. |

Maumbo katika Jedwali 2.15 yanadhihirisha vihisishi ambavyo vimeundwa kwa maneno zaidi ya moja. Kihisishi {*haki ya Mungu*} ni kundi la maneno matatu: nomino {*haki*}, kihusishi {*ya*} na nomino {*Mungu*}. Maneno haya hudhihirisha tu maana inayokusudiwa ya kuapa, yanapotumiwa yote kwa pamoja: {*haki ya Mungu*}. Kihisishi {*la hasha*} ni umbo finyizi lenye vihisishi viwili, {*la*} na {*hasha*}. {*Hadithi hadithi*} ni kundi lenye nomino mbili ambazo hutumika pamoja kama kihisishi. Nomino hizi zikitumika moja moja zinapoteza dhima ya kihisishi na kuwa tu nomino yenye maana ya ngano. Umbo

{*haya*} limerudiwa kuunda kihisishi cha maneno mawili: {*haya haya*} chenye maana ya tosha au simama. Kina mama sokoni wanamsimamisha msukuma rukwama kwa kutumia {*haya haya*} ili asiwagonge. *Salaam aleikum* ni kihisishi cha salamu chenye maneno mawili yenye asili ya Kiarabu: {*salaam*} na {*aleikum*}. {*Salaam*} ina maana ya amani na {*aleikum*} ina maana ya kwenu ninyi nyote. Kihisishi {*salaam aleikum*} kwa hivyo kina maana ya, amani iwe kwenu ninyi nyote/ juu yako. Mbali na umbo la kundi maneno, umbo la vijenzi viwili pia hudhihirika katika kihisishi cha Kiswahili kama inavyobainishwa katika sehemu inayofuata.

### 2.3.2 Kihisishi cha Vijenzi Viwili

Kihisishi cha salamu kilirejelewa katika kujadili umbo la vijenzi viwili. Kihisishi cha vijenzi viwili kilichukuliwa kuwa sentensi sahili ambayo ni sawa na kishazi. Kishazi kilichorejelewa ni kishazi kama uwakilishi kulingana na nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo. Kihisishi cha salamu; *jambo,* hutegemea wahusika wanaosalimiwa na basi hujitokeza kama *hujambo, hamjambo* na *hawajambo*. Vihisishi vya kuitika salamu hizi vitakuwa *sijambo, hatujambo* na *hawajambo* mtawalia kama inavyobainishwa na Jedwali 2.16.

**Jedwali 2.16: Kihisishi cha Maamkizi**

| AMKIZI | | ITIKIO | |
|---|---|---|---|
| **Kihisishi** | **Msingi** | **Kihisishi** | **Msingi** |
| Hujambo | Huna + jambo | Sijambo | Sina + jambo |
| Hamjambo | Hamna + jambo | Hatujambo | Hatuna + jambo |
| Hawajambo | Hawana + jambo | Hawajambo | Hawana + jambo |

Jedwali 2.16 linadhihirisha sura mbalimbali za salamu {*hujambo*} na viitikio vyake. Michakato katika maamkizi haya na viitikio vyake ni fiche. Kila kihisishi katika jedwali kina umbo la vijenzi viwili, kwa mfano katika kihisishi {*hujambo*} anayeamkua anamuuliza mwenzake kama hana jambo naye anamjibu hana jambo. Maneno mawili {*huna*} na {*jambo*} yamefungamanishwa pamoja kuunda kihisishi {*hujambo*}. Katika kiitikio anayejibu anasema {*sijambo*} yaani sina jambo. Vilevile katika {*hamjambo*} na {*hawajambo*}. Katika *hawajambo,* warejelewa hawako katika muktadha wa mazungumzo. Msemaji anawajulia hali warejelewa kupitia kwa msikilizaji ambaye pengine ana uhusiano na warejelewa.

Kulingana na Halliday na Matthiessen (2004), katika Sarufi Amilishi Mfumo, kishazi kama uwakilishi huchanganua umuhimu wa uhusiano kati ya neno na maana zake. Uhusiano huu una sifa tatu: mchakato wa maana ambao unatambulika kwa kitenzi, wahusika katika mchakato wa tajriba na mazingira ambayo huhusishwa na mchakato huu.

Kihisishi cha salamu kimechanganuliwa katika jedwali lifuatalo kwa kurejelea sifa tatu za kishazi kama uwakilishi.

**Jedwali 2.17: Dhihirisho la Kishazi kama Uwakilishi**

| **Mhusika** | **Mchakato** | **Mazingira** |
|---|---|---|
| Mimi | Sina | Jambo |
| Sisi | Hatuna | Jambo |
| Wewe | Huna | Jambo |
| Nyinyi | Hamna | Jambo |
| Wao | Hawana | Jambo |

Katika Jedwali 2.17, kihisishi cha salamu kinapitia michakato tofauti ambayo haijitokezi moja kwa moja katika kihisishi chenyewe. Michakato ambayo inawakilishwa na vitenzi inaambishwa viambishi vikanushi kutegemea mhusika, kwa mfano mhusika ‘mimi’ anawakilishwa na kikanushi {*si*}, mhusika sisi anawakilishwa na {*hu*}, wewe anawakilishwa na {*u*}, nyinyi {*m*} na wao wanawakilishwa na {*wa*}. Mazingira hayabadiliki, yanabaki kuwa nomino {*jambo*} katika mifano yote. Umbo la vijenzi viwili linahitimisha maumbo ya kisintaksia na maumbo ya kihisishi cha Kiswahili kwa ujumla.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza maumbo mbalimbali ya kihisishi cha Kiswahili kwa kutumia vigezo vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Uchanganuzi umebainisha kuwa, kihisishi cha Kiswahili kina maumbo mawili ya kifonolojia: umbo la silabi moja na umbo la silabi nyingi. Kimofolojia, maumbo matatu yalibainishwa: umbo la mofimu moja, umbo la mofimu mbili, na umbo la mofimu changamano. Maumbo mawili ya kisintaksia: umbo la kundi la maneno na umbo la vijenzi viwili pia yamebainishwa. Mbali na maumbo, kihisishi cha Kiswahili kina uwezo wa kuchanganuliwa kwa kutumia kigezo cha matumizi ambacho kitaangaziwa katika sura ya tatu.

## SURA YA TATU

## MATUMIZI YA KIHISISHI CHA KISWAHILI

### 3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilishughulikia kwa undani maumbo ya kihisishi cha Kiswahili na kuweza kujibu swali la kwanza la utafiti. Sura hii ya tatu imejadili na kufafanua matumizi ya kihisishi cha Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano. Dhana ya matumizi inarejelea kazi au namna lugha inavyohusika katika muktadha wa mawasiliano. Lugha hutumika katika amali nyingi ambazo baadhi yake zaweza kudhihirishwa na vihisishi.

Noel (1989) anasema kuwa, waandishi wengi wamerejelea na kujaribu kuweka katika kategoria mbalimbali amali za lugha. Halliday (1985, 1994) katika Sarufi Amilishi Mfumo anagawanya amali za lugha katika makundi matatu makuu: maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi kama ilivyotajwa katika sura ya kwanza (Tazama §1.8.2.2). Kwa mujibu wa Noel (keshatajwa), amali hizi tatu kuu za lugha zaweza kugawanywa zaidi katika amali ndogondogo ili kuonyesha njia mahsusi ambazo watu hutumia lugha katika hali mbalimbali kutimiza mahitaji yao ya kimawasiliano. Utafiti ulichanganua matumizi ya kihisishi cha Kiswahili kwa kurejelea amali hizi ndogondogo kwa usaidizi wa nadharia.

Nadharia za Uchanganuzi Usemi Jadilifu (UUJ) na Sarufi Amilishi Mfumo (SAM) zilitumika katika uchanganuzi wa matumizi ya kihisishi cha Kiswahili kama ilivyotajwa

katika misingi ya nadharia (Tazama §1.8). Katika mhimili wa muundo wa usemi katika nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu, usemi huhusisha matini, mahusiano, na miktadha. Matini yalikuwa vihisishi vya Kiswahili. Msemaji anazalisha kihisishi ambacho kinafasiriwa na msikilizaji baada ya kulielewa lengo la msemaji wakati wa mawasiliano. Uzalishaji na ufasiri wa kihisishi hiki ulitegemea uhusiano wa msemaji na msikilizaji na pia hali zao za kijamii. Mhimili wa muundo wa usemi ulitumika katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya vihisishi, mahusiano ya kijamii na muktadha wa mawasiliano ili kuweza kubaini matumizi ya vihisishi.

Mhimili wa mbinu za uchanganuzi ulitumika katika kuchanganua matumizi ya vihisishi ili kutoa maelezo, ufasiri na ufasili wa kihisishi cha Kiswahili. Mbali na mihimili ya UUJ, mihimili ya SAM ilifanikisha utafiti. Katika mhimili wa muundo wa sarufi, utanzu wa pragmatiki ulitusaidia kuchunguza matumizi ya vihisishi katika muktadha wa mawasiliano. Mhimili wa amali za maana ulitumika katika kuchunguza amali mbalimbali za lugha na kuonyesha jinsi vihisishi mbalimbali hudhihirisha amali hizi. Mhimili wa amali za kishazi ulitumika kuchunguza data lengwa ya utafiti ambayo ilikuwa vishazi huru ambavyo huwakilisha au hujumuisha kihisishi. Kama vile sura ya kwanza ilivyotaja (Tazama §1.8.2.3), mitazamo mitatu ya kishazi inawiana yenyewe na vilevile na amali tatu za maana ambazo hutumika sambamba kuelezea maana. Kishazi na amali za maana kwa hivyo zilitumika kwa pamoja bila kutenganishwa. Matumizi ya Kihisishi cha Kiswahili yalibainishwa kwa kurejelea amali bayana saba: uarifu, ujamilishi, unafsishi, uliwazi, ukalimizi, utendezi, na uchangamshaji.

### 3.1 Uarifu

Lugha ndiyo njia kuu ya kupata na kupitisha maarifa yetu. Lugha husemekana kutumika kama amali ya uarifu wakati ujumbe unaotolewa ni wa kujuza (Noel 1989). Vihisishi katika kundi hili hurejelea hali ya kimaarifa na kimawazo ya msemaji wakati wa kuvitamka. Katika uarifu, msemaji anataraji msikilizaji kupata ujumbe fulani. Vihisishi vinavyoonyesha uarifu vinajumuisha vihisishi vya kukubali, vihisishi vya kukataa, na vihisishi vya kutaka taarifa.

#### 3.1.1 Vihisishi vya Kukubali

Katika mazungumzo, watu hukubaliana na mambo wanayoyazungumzia. Msemaji anataraji ujumbe wake upokelewe na msikilizaji, na msikilizaji anadhihrisha upokezi wa ujumbe kwa kukubali. Mazungumzo yanapoendelea, anayesikiliza anaweza kuonyesha kukubaliana na yanayosemwa kwa kutumia vihisishi: *aa, ahaa, ndiyo, sawa, eeh, hewaa, sadakta, naam, taibu, enhee, haya* na *mmh.* Msikilizaji hukubali kutegemea aliyoambiwa na msemaji kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

1. Mary: Nguo hii ni nzuri kweli?

   Jane: *Ahaa!* Imekupendeza, Mashalla!
2. Do! Mtoto wewe kumbe husikii *eeeh?*
3. Mama A: Umefungua akaunti mpya?

   Mama B: *Ndiyo!* Ina manufaa kemkem.
4. Baba: Salimu! Njoo nikutume.

   Salimu: *Sawa* baba naja.

Katika mfano wa kwanza, Mary na Jane wanajiandaa kwenda katika sherehe. Mary anamuuliza Jane kama nguo aliyoivaa ni nzuri, naye Jane anakubali kuwa ni nzuri kwa kutumia *ahaa.* Katika muktadha huu, *ahaa* inatamkwa kwa kidatu kinachopanda na kisha kushuka, ni sawa na kusema ndiyo. Katika mfano wa pili, kihisishi *eeeh* kinatumiwa na mama kwa mtoto anayeonyesha kuwa anakubali kweli mtoto hasikii. Katika maongezi ya akina mama kuhusu benki, mama B anakubali kwa kutumia kihisishi *ndiyo* kuwa akaunti aliyofungua ina manufaa mengi. Salimu katika mfano wa mwisho anapoitwa na babake amjongee, anakubali kwa kutumia *sawa* kuonyesha kuwa ataenda kwa babake ili aweze kutumwa.

Vihisishi *hewaa, sadakta,* na *taibu* hutumiwa kuonyesha kuwa mtu anaafiki jambo linaloendelea au linalosemwa, na analifurahia. Vihisishi *hewaa* na *taibu* hutamkwa kwa kidatu kinachopanda na kushuka. Kihisishi *sadakta* hutamkwa kwa kidatu cha wastani. Kihisishi *naam* kinapotamkwa kwa kidatu cha wastani na mkazo kuwekwa katika silabi ya kwanza kinaleta maana ya kukubali. Tazama mifano ifuatayo.

5. Mtoto A: Nguvu za umeme zimerejea.

   Mtoto B: *Hewaa!* Twende mwanzo tumalizie ile sinema ya juzi.

6. *Sadakta! Sadakta!* Naona twaendelea vizuri, wale wa kutuma salamu

   tafadhali tujongeeni mbele.

7. *Taibu* kaka.

8. Mtoto: Nilikupa hamsini.

Muuzaji: *Naam*, mwambie aliyekutuma zimeisha

Katika mfano wa tano, nguvu za umeme zilikuwa zimepotea na zinaporejea mmoja wa watoto anawafahamisha wenzake kuwa zimerudi. Mtoto B anakubali kwa kutumia *hewaa* na kuwafahamisha wenzake kuwa ni vizuri kwanza waende wakatazame ile sinema waliyokuwa wakitazama siku iliyotangulia. *Sadakta* katika mfano wa sita, imetumiwa na mtangazaji wa stesheni ya redio ya Pwani akiwahimiza watu waliofika uwanjani Makadara mjini Mombasa kujongea mbele ili kutuma salamu. Mtangazaji anatumia *sadakta* kuafiki kuwa shughuli hiyo inaendelea vizuri. Katika mfano wa saba, ndugu mmoja anamweleza mwenzake kuhusu uzuri wa kuanzisha biashara ya kuuza nguo, naye mwenzake anatumia *taibu* kuonyesha kuwa anakubaliana na yanayosemwa na nduguye. Mwisho, katika mfano wa nane, mtoto mdogo aliyekuwa ametumwa dukani anarejeshwa dukani akadai baki ambayo alistahili kurudishiwa na muuzaji. Anaporudi dukani, anamweleza mwenye duka kuwa alimpa shilingi hamsini naye muuzaji anamjibu *naam* kwa maana ya ndiyo, lakini anamwarifu mtoto akamwambie mamake kuwa hakuna baki. Ili kudhihirisha maana hii, muuzaji anaitamka *naam* kwa kidatu cha wastani.

Kihisishi *enhee* hutumika kuonyesha kukubali au kukubaliana na yanayosemwa. Katika matumizi haya, *enhee* hutumika sawa na *aha*. Katika mazungumzo, *enhee* pia hutumika kwa maana ya kuitikia yanayosemwa na kutaka anayezungumza aendelee kuelezea analozungumzia. Katika matumizi ya kutaka anayezungumza aendelee kutoa maelezo, *enhee* hutamkwa kama swali kwa kidatu kinachopanda kwa nia ya kutaka kujua

kinachofuata. Kihisishi *haya* kinapotumika pamoja na kitone na kutamkwa kwa kidatu cha chini, hutoa maana ya sawa. Kwa mfano katika maongezi ya watu wawili, anayesikiliza atakubali anachoambiwa kwa kutumia *haya* kumaanisha anayoambiwa ni sawa au anakubaliana nayo.

9. Binti I: Ni elfu mbili tu.

   Binti II: *Enhee.*

10. Juma: Nilikuwa natembea sokoni…

    Musa: *Enhee?*

    Juma: Nikamwona mama amebeba mtoto…

    Musa: *Enhee?*

11. *Haya*. Baki nayo, si wajidai hukumbuki wewe tena, basi nishukishe…njooo

    mwanangu tushuke.

Katika mfano wa tisa, bei ya nguo inatajwa kuwa elfu mbili, jambo analokubaliana nalo binti wa pili kwa kutumia *enhee*. Juma anasimulia yaliyompata sokoni naye Musa anaitikia kwa *enhee* inayotamkwa kama swali kwa kidatu kinachopanda ili kumfanya Juma aendelee kusimulia. Matumizi ya *haya* katika mfano wa kumi na moja yanaonyesha mama mmoja ambaye alikuwa kwenye gari la abiria, anayedai baki yake kutoka kwa utingo lakini utingo anajifanya kuwa hakuna baki. Mama anakasirika na kumwambia utingo *haya* kwa maana ya sawa na kumwomba amshukishe.

Kuridhia au kuonyesha kuwa unakubaliana na yanayosemwa, waweza kutumia kihisishi *mmh*. Katika muktadha huu, *mmh* hutamkwa kwa kurefushwa huku kidatu kikipanda. *Mmh* pia hutumika unapomtaka mtu arudie alichosema pengine kwa kukosa kuelewa. Hapa hutamkwa kwa kidatu cha juu huku ikiambatana na alama ya kuuliza. Matumizi ya kihisishi *mmh* yanadhihirika katika mifano ifuatayo.

12. *Mmh!* Ndivyo ilivyo.

13. Jane: Rukia! Waitwa na mwalimu.

    Rukia: *mmh?*

    Jane: Waitwa na mwalimu.

Msemaji katika mfano wa kumi na mbili anakubali kwa kutumia *mmh* kuwa hali ipo jinsi alivyoelezewa. Hii ni baada ya mwenzake kumwelezea jinsi hali imekuwa tangu kufariki kwa mzee Gitau aliyekuwa mwajiri wao. Katika mfano wa kumi na tatu, Jane anamwita Rukia na kumwarifu kuwa alikuwa akiitwa na mwalimu, lakini Rukia hajaelewa anachoambiwa na Jane na kwa hivyo anatumia kihisishi *mmh* kumtaka Jane arudie alichosema ili aweze kukitekeleza.

Vihisishi vya kukubali vimeonyesha kuwa, ili msikilizaji kutoa jibu kwa yaliyosemwa na msemaji, ni sharti kuuelewa ujumbe huo na kisha kuufasiri kutegemea muktadha wa mazungumzo. Baada ya kuufasiri ujumbe, msikilizaji anakubaliana na yaliyosemwa kwa kutumia kihisishi cha kukubali. Wakati mwingine ikiwa msikilizaji hakubaliani na

yanayosemwa, ufasiri wake utamwelekeza kukataa, na katika muktadha huu atakataa kwa kutumia vihisishi vya kukataa kama inavyoonyeshwa katika sehemu inayofuata.

### 3.1.2 Vihisishi vya Kukataa

Kukataa ni kukana au kuonyesha hali ya kutokubaliana na jambo au tendo fulani (TUKI 2013). Matumizi ya vihisishi kama: *hapana*, *a-a, aka*, *abadan, hasha, hata, kamwe, katu*, *la*, na *ng'o* hudhihirisha dhana ya kukataa. Ikiwa jambo limefanyika na mtu fulani anatuhumiwa kulitenda na ilhali si yeye aliyetenda, atakataa kwa kutumia vihisishi vya kukataa. Wakati mwingine vihisishi vya kukataa hutumiwa kuonyesha kuwa msemaji hafahamu jambo linalozungumziwa.

14. Mama: Si pesa ulipewa jana asubuhi wewe?

    Muuza maji: *Hapana!* Nakumbuka tena vizuri sana, hukunilipa. We! Nipe pesa niende zangu.

15. Mama: Umetoka Majengo wewe?

    Mtoto: *A-a*, mimi sikwenda; mama mimi sikwenda huko.

16. Mgeni: Wee! Mama yuko?

    Mtoto: *Aka.*

17. Mzee: Mamako yuko?

    Msichana: *La!* Alisafiri leo kwenda kwa nyanya.

18. Mimi sikufika kwao *abadan katan.*

Katika mfano wa kumi na nne, muuza maji anadai pesa za maji lakini mama aliyeletewa maji anasisitiza kuwa alimlipa pesa za maji. Muuza maji kwa hasira anakataa kwa kutumia *hapana* kuwa hakulipwa pesa. Kihisishi *hapana* chaweza kutamkwa kwa kidatu cha chini ikiwa mazungumzo ni ya upole. Katika maandishi, *hapana* ya kidatu cha chini itaakifishwa kwa alama ya kituo au nukta. Ikiwa ni kukataa kwa ukali au hasira, *hapana* itatamkwa kwa kidatu cha juu na katika maandishi itafuatwa na alama ya hisi.

Ilibainika kuwa kihisishi *a-a* hutumiwa sana na watoto katika kukana. Wakati mtoto amefanya kosa akiulizwa swali atakataa kwa kutumia *a-a* ambayo hutamkwa kwa kidato cha chini. Katika mfano wa kumi na tano, mama anamuuliza mtoto kama alienda Majengo, naye mtoto anakataa kwa kutumia *a-a*. Ilibainika kuwa, kihisishi *a-a* hakitumiki sana katika maongezi rasmi. Kihisishi *aka* kikitamkwa kwa kidatu cha chini kinachopanda, hutoa maana ya kukanusha au kukataa. *Aka* pia hutumiwa kuonyesha kuwa haiwezekani yaani msemaji haamini kuwa mambo yapo jinsi yalivyo. Mfano wa kumi na sita unaonyesha mazungumzo kati ya mgeni na mtoto, mgeni anataka kujua kama mamake mtoto yuko naye mtoto anakataa kwa kutumia *aka* kuwa mama hayuko.

Kihisishi *la* hutumiwa kukataa na ndicho kihisishi ambacho kimezoeleka na watu wengi katika hali zote, hali rasmi na hali zisizo rasmi. Ili kusisitiza kwamba jambo linalosemwa si la kweli, *la* hutumika pamoja na *hasha*: *la hasha* na hutamkwa kwa kidatu cha juu ili kuonyesha kukataa kabisa. Vihisishi hivi viwili vyaweza kutumika kila kimoja pekee, na katika hali hii hutamkwa kwa kidatu cha wastani. Wakati mwingine kukataa kwaweza

kuambatana na ishara ya kutingisha kichwa. Mzee katika mfano wa kumi na saba anamuuliza msichana kama mamake yupo nyumbani. Msichana anakataa kwa kutumia *la* kwa maana kuwa mama hayupo.

Mtu akanushapo jambo na ikatokea kuwa hasikizwi au haaminiki, atatumia *abadan* kuonyesha kuwa jambo hilo sivyo lilivyo. *Abadan* yaweza kutumika pamoja na *katan*; *abadan katan* sawa na *asilani* au *katu* kuleta maana kwamba lisemwalo haliwezekani. Kuonyesha kuwa linalosemwa halitatendwa, kihisishi *kamwe* hutumiwa. Kihisishi hiki hutamkwa kwa kidatu cha juu ili kutilia nguvu ukanushaji. Mara kwa mara *kamwe* hutumika katika kukanusha jambo litakalofanywa wakati ujao. Mtoto anapoulizwa na babake katika mfano wa kumi na nane kama alikuwa ameenda hadi kwa rafikiye, anakana kuwa hakufika nyumbani kwa rafikiye kwa kutumia *abadan katan*. Mtoto anasisitiza hapa kuwa kwa kweli hakufika kule kunakotajwa.

Ujumbe wa msemaji unaleta athari ya kukataa kwa msikilizaji. Kutokana na mifano iliyotajwa hapo juu, imebainika kuwa msikilizaji hakubaliani na yaliyosemwa na msemaji ama anapinga anayoambiwa kutenda. Kulingana na anayoarifiwa, inamlazimu kutumia kihisishi cha kukataa ili kufanikisha maongezi. Mbali na vihisishi vya kukataa, amali ya uarifu hudhihirika katika vihisishi vya kutaka taarifa.

### 3.1.3 Vihisishi vya Kutaka Taarifa

Kama ilivyotajwa katika sura ya pili (Tazama § 2.2.3), kihisishi *kulikoni* ni ufupisho wa ‘kulikuwa na nini’. Ingawa kihisishi hiki kinaashiria wakati uliopita, watumiaji hawazingatii matumizi haya bali hukitumia kihisishi *kulikoni* kwa maana sawa na kihisishi *kunani* ambacho ni ufupisho wa ‘kuna nini?’ Vihisishi *kulikoni* na *kunani* hutumika na mtu anayetaka kufahamu kinachoendelea au kupata taarifa fulani. Katika mazungumzo, ikiwa mtu hajasikia lililosemwa na angependa aliyesema arudie, atatumia kihisishi *ati* kwa maana ya ‘wasema nini’ au ‘rudia ulichosema’ ili aweze kupata taarifa hiyo. *Ati* katika muktadha huu hutamkwa kwa kidatu cha chini kinachopanda hadi juu ikiambatana na alama ya kuuliza. Zingatia mifano inayofuata.

19. Mtangazaji: Maeneo ya Mombasa, Mwembe Tayari, Miritini, tufahamisheni *kulikoni* barabarani?
20. Mashalla! *Kunani* bwana, jionee mwenyewe! (Wavuvi wanastaajabia samaki wakubwa waliowavua)
21. *Ati*? Wasema nini?

Katika mfano wa kumi na tisa, mtangazaji wa stesheni ya redio ya Pwani anawauliza wasikilizaji wamfahamishe jinsi hali ilivyo barabarani baada ya mvua kubwa kunyesha kwa kutumia *kulikoni*. Baada ya swali hili, msikilizaji mmoja anamjulisha kuwa katika sehemu ya Majengo barabara zimeharibiwa na mafuriko. Katika mfano wa ishirini, wavuvi wamepata samaki wakubwa na wanastajabia pato lao ambapo mmoja anamuuliza mwenzake *kunani* na kumweleza ajionee mwenyewe samaki waliowapata. Msemaji

katika mfano wa ishirini na moja, anatumia *ati* kuonyesha kuwa hajasikia vizuri yanayosemwa na angependa yarudiwe.

Katika sehemu hii, amali ya uarifu imejadiliwa na mifano mbalimbali ya vihisishi vinavyodhihirisha uarifu kuonyeshwa. Imebainika kuwa, baada ya msikilizaji kuarifiwa au kupokea ujumbe kutoka kwa msemaji, ni sharti kuuelewa ili aweze kuufasiri. Ufasiri wa msikilizaji utategemea muktadha wa mawasiliano. Msikilizaji atafasiri na kutathimini taarifa aliyoipokea na kuifananisha na ujuzi alionao pamoja na tajriba yake. Amali ya uarifu haikosi uwiano na amali ya ujamilishi inayojadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 3.2 Ujamilishi

Lugha hutumika katika mwingiliano wa kijamii na hurahisisha mawasiliano. Binadamu kama viumbe wa kijamii huhitaji kushiriki fikra na hisia za wenzao. Lugha kwa hivyo, hutumika kuweka na kudumisha uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji (Noel 1989). Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu hutazama lugha kama chombo muhimu katika shughuli za kijamii na hujikita katika kuangalia mahusiano ya kijamii yanayodhihirika kiusemaji (Fairclough 1989). Vihisishi vinavyodhihirisha amali ya ujamilishi ni vile ambavyo vina uwezo wa kuunda na kudumisha mtagusano wa kimawasiliano; kuwafanya watu kuwa na utulivu na upatanifu na wenzao. Amali ya ujamilishi hudhihirika katika vihisishi vifuatavyo: vihisishi vya kubisha, vihisishi vya kukaribisha, vihisishi vya salamu, vihisishi vya kuita, vihisishi vya kuitika, vihisishi vya shukrani, vihisishi vya samahani, vihisishi vya pongezi, na vihisishi vya kuaga.

### 3.2.1 Kihisishi cha Kubisha

Kihisishi *hodi* hutumika katika kubisha mlango ili uweze kufunguliwa na aliye ndani. Wakati mwingine *hodi* huandamana na ishara ya kugongagonga mlango. Mbali na kubisha mlango, *hodi* pia hutumika katika kuomba ruhusa ya kuingia kwa mfano katika boma, mkutanoni au ndani ya nyumba. Katika matumizi ya pili, *hodi* haiambatani na ishara. Jibu la *hodi* ni 'karibu'. Msemaji anabisha kwa *hodi* naye msikilizaji anajibu 'karibu' ili kumkaribisha mgeni wake. Vihisishi vya kubisha hutumika katika muktadha sawa na vihisishi vya kukaribisha.

### 3.2.2 Vihisishi vya Kukaribisha

Katika makaribisho, kuna uhusiano kati ya mwenyeji na mgeni. Mgeni anapoomba ruhusa ya kuingia, mwenyeji wake anamkaribisha kwa *karibu* au *kongoni*. *Kongoni* hutumika katika kumkaribisha mtu ambaye anafahamika kwa wenyeji. Eastman (1983) anasema kuwa, *kongoni* ni sawa na kusema 'tuwemo' yaani sisi sote tuwe ndani pamoja. Ilibainika kuwa *kongoni* ina uzito zaidi katika kumkaribisha mtu ikilinganishwa na *karibu*. *Karibu* hutumika kumkaribisha mtu yeyote lakini *kongoni* hutumika kuwakaribisha watu unaowafahamu kama marafiki au watu wa ukoo ambao una uhusiano wa karibu nao au hata wageni maalumu ambao mara nyingi huwa wametoka mbali. Kwa mfano msichana anasema, "Aaa! *Kongoni* anti." kumkaribisha shangazi aliyetoka safarini.

Katika kumwitikia mtu aliyebisha hodi na ambaye angependa kuingia ndani, kihisishi *karibu* hutumika. Kihisishi *karibu* pia hutumiwa kumtuliza mgeni hasa aliyetoka mbali au

hata mwenyeji ambaye hakuwepo nyumbani na amerejea kutoka safarini. Wakati mwingine *karibu* hutumika katika kumwitikia mtu anayeaga na kuondoka kwa maana ya 'rudi tena.' Vilevile *karibu* hutumiwa kama jibu kwa shukrani unayopewa na mtu uliyemtendea mema. Zingatia mifano hii.

22. Mgeni: Hodi wenyewe!

    Mwenyeji: *Karibu!* Mlango uko wazi.

23. *Karibu! Karibu* mume wangu, pole kwa safari.

24. Kaka: Kwaheri dada (Akiondoka).

    Dada: *Karibu* tena kaka.

25. Joel: Mama Zubeda asante kwa mwaliko wako.

    Mama Zubeda: *Karibu* Joel.

Katika mfano wa ishirini na mbili, mgeni anabisha hodi mlangoni na kuitikiwa na mwenyeji *karibu* kwa maana kuwa aingie ndani. *Karibu* katika mfano wa ishirini na tatu imetumika na mke anayemkaribisha na kumtuliza mumewe ambaye amefika kutoka safarini. Katika muktadha huu, *karibu* imerudiwa kuonyesha msisitizo. Katika mfano wa ishirini na nne, kaka ambaye alikuwa amemtembelea dadake anamuaga huku akiondoka na dada anamjibu *karibu* kwa maana kuwa ana uhuru wa kurudi tena. Katika mfano wa ishirini na tano, mama Zubeda alikuwa na karamu na baada ya karamu wageni wanafumukana ambapo Joel anamshukuru mama Zubeda kwa kumualika, naye mama Zubeda anamjibu *karibu* kuonyesha kuwa anakaribishwa tena wakati mwingine. Katika

mahusiano ya kijamii, baada ya kumkaribisha mgeni na kumpokea, mgeni na mwenyeji wanajuliana hali na hili hufanyika kwa kutumia vihisishi vya salamu.

### 3.2.3 Vihisishi vya Salamu

Salamu ni njia ya kuamkuana. Tamaduni nyingi zina taratibu mbalimbali za kuzingatiwa wakati wa kutoa salamu. Utaratibu maalumu na maadili ambayo hufuatwa wakati wa salamu umewekwa ili kudumisha nidhamu ya kuamkuana. Jambo muhimu ni yupi aanze kutoa salamu na ni wepi wanaofaa kutolewa salamu. Kwa kutilia maanani vipengele hivi, mwongozo ufuatao hutumiwa wakati wa kutoa salamu:

(a) Aliyepanda (kipando) amsalimie anayetembea.

(b) Anayetembea amsalimie aliyeketi.

(c) Wachache wawasalimie walio wengi.

(d) Mdogo amsalimie mkubwa.

(e) Kila mtu ana wajibu wa kumsalimia anayemjua na asiyemjua.

(www.alhidaaya.com/sw/node/1799)

Vihisishi vinavyotumika kama salamu hutegemea wakati wa kutoa salamu na pia uhusiano au umri wa anayetoa salamu. Kwa mfano, kihisishi *shikamoo* hutumiwa na wadogo wa umri kwa wakubwa ili kuonyesha heshima na unyenyekevu. Mkubwa atajibu *marahaba*. Kulingana na utamaduni wa Waswahili, *shikamoo* ilimaanisha *nakushika mguu* yaani mdogo anamshika miguu yule mkubwa naye mkubwa anamjibu mdogo *marahaba* maanake *nakubali*. Kidesturi salamu hizi lazima ziambatane na majina au vyeo vya washiriki. Utafiti ulibaini kuwa, ni makosa kusema tu *shikamoo* au *marahaba* bila

kutaja majina au vyeo vya wahusika. Kama ilivyotajwa katika sura ya pili (Tazama § 2.13), kihisishi *Shikamoo* huweza kuambishwa kwa kuongezewa kiambishi tamati cha wingi {*ni*} wahusika wanaosalimiwa wanapokuwa wengi.

26. Mtoto: *Shikamoo* baba?

    Baba: *Marahaba* mwanangu.

27. Msichana: *Shikamooni* baba na mama?

    Wazazi: *Marahaba*

28. Mwanafunzi: *Shikamoo* mwalimu?

    Mwalimu: *Marahaba* Juma, umetumwa nini?

Katika mfano wa ishirini na sita, mtoto anamsabahi baba *shikamoo* naye baba anamjibu *marahaba* kukubali salamu za mtoto. Katika mfano wa ishirini na saba, msichana anapoamka anawakuta wazazi wake sebuleni na kuwaamkua wote pamoja kwa *shikamooni*, nao wanamjibu kwa pamoja *marahaba*. Katika mfano wa mwisho, mwanafunzi mbaye ametumwa afisini anakutana na mwalimu mlangoni na kumwamkua kwa *shikamoo*. Mwalimu anamjibu *marahaba* na kumuuliza alichokuwa ametumwa afisini. Ilibainika kuwa *shikamoo* hudhihirisha heshima kuu kwa wakubwa na hutumika katika nyakati zote za siku.

Kihisishi *salaam aleikum* hutumika wakati wowote. Salamu hii haina ubaguzi wa kijinsia, wakati, umri na mandhari. *Salaam aleikum* ina maana kuwa amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yako (Tazama § 2.3.1). Jibu lake ni *Waleikum salaam* yaani na wewe pia

amani iwe kwako. Wakati mwingine *salaam aleikum* yaweza kuongezewa kiambishi ‘a’ mwanzoni na kuwa *asalaam aleikum.* Baadhi ya wahojiwa walisema kuwa *asalaam aleikum* haina tofauti na *salaam aleikum* lakini wengine walishikilia kuwa, kiambishi ‘a’ kikiongezewa kinaleta dhana ya wingi wa wanaosalimiwa. Wakati mwingine salamu hii hurefushwa kwa kuongezea maneno mengine. Tazama mifano ifuatayo.

29. Mpiga simu: Haloo *salaam aleikum?*
30. Musa: *Salaam aleikum wa rahmatu Allah.*
    Barak: *Waleikum salaam wa rahmatu i-lahi wa barakatu.*

Katika mfano wa ishirini na tisa, mpiga simu anamsalimu mwenzake kwa *salaam aleikum* kabla ya kuanzisha mazungumzo ili kumtakia mwenzake mema. Mwenzake katika upande ule wa pili anastahili kujibu *waleikum salaam* kama ilivyo desturi ili pia kumtakia mwenzake amani ya Mwenyezi Mungu. Katika mfano wa thelethini, Musa anapokutana na Juma njiani, anamsabahi kwa *Salaam aleikum wa rahmatu Allah* kwa maana ya ‘amani na Baraka zake Mungu ziwe nawe’. Juma naye anamjibu *waleikum salaam wa rahmatu i-lahi wa barakatu* yenye maana kuwa ‘amani na baraka za Mungu ziwe nawe pia.’ Ilibainika kuwa *salaam aleikum* ni salamu muhimu sana katika jamii kwa sababu huwahakikishia wanajamii usalama wao. Unapomsalimu mwenzako kwa *salaam aleikum* unaonyesha kuwa hautamdhuru au haumtakii mabaya.

Kihisishi cha salamu, *hujambo* hakibagui wakati, jinsia, wala umri. Kiitikio chake ni *sijambo*. Anayeamkua anamjulia mwenzake hali kwa kumuuliza kama hana jambo naye

anamjibu kuwa hana jambo yaani yu mzima. Kwa kawaida hata kama una tatizo, unastahili kujibu salamu jinsi inavyostahili kisha utaje tatizo lako baadaye. Salamu hazina majibu yaliyo kinyume cha majibu ya kawaida. Kama ilivyotajwa katika sura ya pili (Tazama § 2.3.2), salamu hii hutegemea idadi ya wahusika na kwa hivyo viambishi vyake hubadilika kutegemea nafsi za wanaosalimiwa kwa mfano, kama ni nafsi ya pili wingi (nyinyi) itakuwa: *Hamjambo? – Hatujambo. Hujambo* huambatana na jina au cheo cha anayeamkiwa.

31. Kaka: *Hujambo* dada?

    Dada: *Sijambo* kaka.

32. Mwalimu: *Hamjambo* wanafunzi?

    Wanafunzi: *Hatujambo* mwalimu, shikamoo.

    Mwalimu: marahaba wanafunzi, ketini.

    Wanafunzi: Asante mwalimu.

Katika mfano wa thelathini na moja, kaka anapokutana na dada anamjulia hali kwa kumsalimu *hujambo* naye dada anamjibu *sijambo* kwa maana kuwa yu mzima hana neno. Katika mfano wa thelathini na mbili, mwalimu wa darasa la nne katika shule ya msingi anaingia darasani na kuwasalimu wanafunzi kwa *hamjambo.* Wanafunzi wanasimama na kumjibu *hatujambo* na pia kumuamkua mwalimu kwa shikamoo. Mwalimu anajibu salamu za wanafunzi na kuwaamuru waketi na kisha somo linaanza.

Salamu ndicho kiini cha kuanzisha mazungumzo kati ya msemaji na msikilizaji. Baada ya salamu, msemaji na msikilizaji hushiriki katika mazungumzo mbalimbali. Katika mazungumzo haya, msemaji anaweza kumwita msikizaji. Kuita huku kunaweza kuwa kwa kutumia majina halisi ya wahusika au kwa kutumia vihisishi vya kuita.

### 3.2.4 Vihisishi vya Kuita

Watu wanapotangamana huwaita wenzao kwa kutumia vihisishi kama vile *aisee, bwana, enyi,* na *taire*. *Aisee* na *bwana* hutumika unapomwita mwenzako asikilize unayomwambia na ilibainika kuwa hutumika sana na wanaume. Vihisishi *aisee* na *bwana* vyaweza kutumika kila kimoja pekee au kwa pamoja; *aisee bwana! Enyi* hutumika kuwaita wahusika wengi waliokusanyika pamoja. *Taire* hutumiwa na waganga kuyaita mazimwi. Tazama mifano ifuatayo.

33. *Aisee bwana!* Wacha kelele, huku ni Mombasa.
34. *Enyi!* Mwaja ama hamji nijipange?
35. Mganga: *Taire! Taire! Taire!*

Katika gumzo la wazee jioni katika mfano wa thelathini na tatu, panatokea mzee mmoja anayezungumza kwa sauti na kukashifu vitendo vya baadhi ya viongozi. Mzee mwingine katika kikundi anamwita *aisee bwana* na kumwomba aache kelele na kumkumbusha kuwa alikuwa Mombasa bali si katika mji mwingine. Anasisitiza kuwa alikuwa Mombasa kwa misingi ya imani kuwa, watu wa Mombasa ni wapole na hawapendi kelele. Katika mfano wa thelathini na nne, kijana anawaita wenzake walioko mbali naye kwa kutumia

*enyi* ili waende aliko. Mwisho, katika mfano wa thelathini na tano, mganga anayaita majuju kwa sauti na kwa kurudia *taire* mara nyingi. Ilibainika kuwa ilikuwa ni lazima majuju yaitwe kwa sauti kuu na pia mara nyingi ili yaweze kujitokeza mbele ya mganga. Baada ya kujitokeza basi ilikuwa ni fursa ya mganga kuzungumza nayo. Mganga pia angeweza kuwatuliza na kutaka usikivu wa wateja wake kwa kuwaamrisha *taire taire.* Amri hii iliwafanya wateja kumsikiliza na kungojea maagizo kutoka kwake.

Kihisishi *ewe* kinapotamkwa kwa kidatu kinachoanzia chini na kupanda hutumiwa katika maombi kama njia ya kumwita, kumsihi na kumwomba Mungu. *Ewe* hutumika sawa na *ee.* Kihisishi *ewe* pia ni ufupisho wa ‘ee wewe’ na kinapotamkwa kwa kidatu cha juu hutumika katika kumwita mtu unayetaka kusema naye kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

36. *Ewe* Mwenyezi Mungu, tuhurumie haya mafuriko yamezidi.

37. *Ewe* John! Njoo tusemezane.

Mfano wa thelathini na sita unaonyesha matumizi ya *ewe* ambapo inatamkwa kwa kidatu kinachoanzia chini na kupanda kuleta dhana ya kumwita Mungu katika maombi. Mhusika anamwomba Mungu awaepushe na madhara ya mafuriko. *Ewe* katika mfano wa thelathini na saba, imetumika kama ufupisho wa ‘ee wewe’ kwa maana ya kumwita John. Msemaji anamwita John ili waweze kusemezana.

Katika mazungumzo, msemaji huweza kumshirikisha msikilizaji kwanza pengine kwa kumwita ili aweze kumsikiliza au kujongea mahali alipo. Wakati msemaji anapomwita msikilizaji, anatekeleza amali ya ujamilishi kwa kutumia vihisishi vya kuita. Kuita huku kunasaidia katika kudumisha uhusiano kati yao kwa kuwaleta pamoja kimawazo pengine ili waweze kushiriki mazungumzo. Baada ya kuitwa msikilizaji ataufasiri ujumbe wa msemaji na kuuelewa na kisha kutekeleza anayohitajika kufanya kulingana na ujumbe wa msemaji. Baada ya kuitwa, msikilizaji anaweza kumjibu msemaji kwa kuitika akitumia vihisishi vya kuitika.

**3.2.5 Vihisishi vya Kuitika**

Katika shughuli za kila siku za wanadamu, watu hutangamana na wenzao nyumbani, sokoni, shuleni, na hata garini. Katika shughuli hizi, watu huwaita wenzao na wanaoitwa huitika. Utafiti ulibaini kuwa, kuna jinsi nyingi za kuitika kutegemea umri au uhusiano wa wahusika. Kwa mfano, *abee, labeka, eeh, naam,* na *afande.* Ilibainika kuwa kihisishi *eeh* hutumika sana siku hizi katika mazingira yasiyo rasmi hasa na vijana wanapoitwa na wenzao.

Kihisishi *Abee/bee* hutumika na wanawake kuitika wanapoitwa na mtu aliye na umri mkubwa kuwaliko ili kuonyesha heshima. Wanawake waweza kuitika kwa kihisishi *abee* tu ama waweza kuongezea jina la anayewaita kwa mfano, *abee* mama. *Labeka* ni kihisishi cha kuitika cha heshima zaidi cha jinsia zote. Ukimwita mtu na aitike *labeka* yaonyesha kuwa anayeitika anamheshimu na kumnyenyekea yule anayemwita. Kihisishi

hiki hata hivyo, hakitumiki sana siku hizi kwa sababu watu wengi hasa vijana hupendelea kutumia kihisishi *eeh* katika kuitika.

38. Mama: Rehema!

    Rehema: *Abee* mama.

39. Mwalimu: James!

    James: *Labeka* mwalimu.

40. Kijana I: Luka:

    Kijana: II: *Eeh!*

    Kijana I: Twachelewa.

Rehema katika mfano wa thelathini na nane, anapoitwa na mama anaitika kwa *abee* kisha anajongea karibu na mama ili aweze kusema naye. Katika mfano wa thelathini na tisa mwalimu anamwita James naye James anaitika kwa *labeka* kwa sababu ya heshima aliyonayo kwa mwalimu wake. Mwisho katika mfano wa arubaini, kijana wa kwanza anamwita mwenzake naye anaitika kwa *eeh* na kisha anaarifiwa kuwa walikuwa wanachelewa. Kihisishi *eeh* kilijitokeza kuwa maarufu sana miongoni mwa vijana.

Kihisishi *naam* hudhihirisha matumizi mbalimbali kutegemea muktadha wa mawasililiano. Katika amali ya uarifu (Tazama § 3.1.1), kihisishi *naam* kimetumika kuonyesha kukubali, lakini katika sehemu hii kihisishi *naam* kinatumika kuonyesha kuitika au kuitikia na basi kudhihirisha amali ya ujamilishi. Mtu anapoitwa na mwenzake

huitika kwa kutumia *naam.* Utafiti ulibaini kuwa, kidesturi wanaume walistahili kuitika kwa kihisishi *naam* lakini siku hizi kinatumika na jinsia zote katika kuitika. Wakati wa kuitika, kidatu kinaanzia chini na kupanda. Kihisishi hiki chaweza kuandamana pia na jina la anayeita. Matumizi ya kihisishi *naam* yanaonyeshwa katika mifano ifuatayo.

41. Baba: Ali!

    Ali: *Naam* baba!

42. Mama I: Tulisafiri salama, lakini tulipofika Voi…

    Mama II: *Naam.*

    Mama I: Mambo yakaanza kubadilika…

    Mama II: *Naam.*

Katika mfano wa arubaini na moja, baba anamwita Ali ili aweze kusema naye. Ali anaitika kwa *naam* ambapo kidatu kinaanzia chini na kupanda. Wakati wa kuitika Ali anaambatisha *naam* na jina la baba ambaye ndiye anayemwita. Wakati mwingine *naam* hutumika katika kuitikia wakati wa mazungumzo na kumtaka anayezungumza aendelee kusema kama inavyojitokeza katika mfano wa arubaini na mbili. Mama I anasimulia yaliyotokea safarini, naye mama II anaitikia kwa *naam* ili kumtaka mwenzake aendelee kusimulia. Katika matumizi haya, *naam* hutamkwa kama iliyofupishwa kama vile, *nam.* Kwa mfano katika, maongezi ya simu waweza kumsikia mtu anayeongea kwa simu akiitikia tu kwa *naam*, *naam* hata ukakosa kuelewa wanachozungumzia.

Askari wanapoitwa na wakubwa wao huitika kwa *afande*. Mbali na askari, ilibainika kuwa kihisishi *afande* pia hutumika na wafanyikazi wengine wa utawala kwa mfano machifu, wakuu wa kaunti ndogo na wakuu wa kaunti kwa wakubwa wao. *Afande* ni kihisishi ambacho huandamana na saluti ishara ya heshima kwa wakubwa. Wakati mwingine kihisishi *afande* hutumika kuonyesha kukubali unapoulizwa kitu na mkubwa wako na pia hutumika katika kumwita mkubwa wako kwa heshima bila kutaja Jina lake. Tazama mifano ituatayo.

43. Mkuu wa kaunti: Madam Jane!

Mkuu wa kaunti ndogo: *Afande!*

44. Sajini: Koplo Ali! Umeishughulikia ile faili?

Koplo: *Afande.*

Sajini: Sawa.

Koplo: *Afande!* na yule mzee wa jana anahitaji msaada wetu.

Sajini: Tutaangalia kesho.

Koplo: Ndiyo *afande.*

Katika mfano wa arubaini na tatu, mkuu wa kaunti anapomwita Jane, Jane anaitika kwa *afande* kuonyesha heshima kwa vile mkuu wa kaunti ni mkubwa wake kazini. Mbali na kuitika kwa afande, Jane anapiga saluti. Katika kuitika, kila wakati *afande* huandamana na saluti kudhihirisha heshima kwa cheo cha anayeita. Sajini katika mfano wa arubaini na

nne anamuuliza koplo kama ameishughulikia faili tajwa naye koplo anakubali kuwa ameishughulikia kwa kutumia *afande*. Koplo anamwita sajini kwa kutumia *afande* na kumwelezea kuwa mzee waliyekuwa wamemshughulikia siku iliyotangulia bado alihitaji msaada wao. Sajini anapomjibu kuwa wangemshughulikia siku itakayofuata, koplo anakubali kwa kusema kuwa ndiyo *afande* yaani ndiyo mkubwa.

Mbali na kuitika, vihisishi *naam* na *afande* vimedhihirisha matumizi mengine ya kuita, na kuitikia kutegemea muktadha wa mawasiliano ambayo pia yanabainisha amali ya ujamilishi. Kwa ujumla, vihisishi vya kuitika vimeonyesha kuwa, watu wanapoitwa na kuitika, basi huunda na kudumisha mtagusano kati yao. Baada ya kuitika, wahusika huweza kushiriki mazungumzo. Katika mazungumzo haya, kunaweza kutolewa shukrani kwa jambo lililotendwa, kwa mfano mwenyeji yuaweza kumshukuru mgeni wake kwa kumtembelea. Katika hali hii, vihisishi vya shukrani hutumika jinsi inavyodhihirika katika sehemu inayofuata.

### 3.2.6 Vihisishi vya Shukrani

Baada ya kufanyiwa jambo zuri au kupewa usaidizi na mtu, ni vizuri kumshukuru mtu huyo au hata Mungu kwa msaada wake. Kihisishi *asante* hutumika kutoa shukrani. Mbali na kupewa msaada au kufanyiwa jambo zuri, shukrani zaweza kutolewa kwa mtu aliyekutuliza au kwa mtu aliyekusifia kwa jambo fulani. Shukrani huweza kuzidisha au kudumisha uhusiano mwema kati ya wahusika. Mifano ifuatayo inadhihirisha matumizi ya vihisishi vya shukrani.

45. Shukrani sana Liz kwa kuongea nasi. *Asante* sana.

46. Mutua: Poleni kwa msiba

Mary: *Asante*, tushapoa.

47. Msichana I. Vipi! Ee, umeng'ara leo!

Msichana II. *Asante.*

Katika mfano wa arubaini na tano, mtangazaji wa redio anamuuliza Liz ambaye ni wakili kuhusu haki za mtoto aliyekuwa amebakwa. Baada ya mazungumzo mtangazaji anamshukuru Liz kwa kutumia *asante* sana kwa sababu ya kuwapa taarifa waliyokuwa wakihitaji. Katika mfano wa arubaini na sita, Mutua anampa Mary pole kwa sababu ya msiba wa kufiwa na mama yao, naye Mary anamshukuru Mutua kwa kutumia *asante* kwa kumpa pole na kumwarifu kuwa washapoa. Katika mfano wa arubaini na saba, Msichana I anampongeza Msichana II kwa sababu ya kurembeka na kuwa nadhifu. Hii ni baada ya msichana I kuvaa nguo mpya alizokuwa amenunua kwa sababu ya sherehe ya harusi. Msichana II anakubali pongezi za msichana I na kumshukuru. Mbali na vihisishi vya shukrani, amali ya ujamilishi pia hushirikisha vihisishi vya maagano katika kuendeleza mkufu wa mahusiano ya kijamii kama inavyodhihirika katika sehemu inayofuata.

### 3.2.7 Vihisishi vya Maagano

Watu wanapokutana na kutawanyika, hutakiana heri na kuagana kwa kutumia vihisishi. *Alamsiki* hutumika wakati wa usiku. Haya ni maagano ya watu wanapoenda kulala.

Kihisishi *alamsiki* hata hivyo hakitumiki sana, na kinapotumika hutumiwa na vijana wa shule ambao mara nyingi, kulingana na uchunguzi wetu, huwa wamekisoma shuleni. Badala ya kutumia *alamsiki,* watu wengi hutumia: ‘lala salama’ au ‘usiku mwema.’ Kiitikio cha *alamsiki* ni *binuru.* Baada ya kutangamana katika shughuli mbalimbali, watu huagana kwa kusema *kwaheri* au *kwaheri* ya kuonana. *Kwaheri* pia hutumika katika kuwaaga watu wanaosafiri jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

48. Mwanafunzi I: *Alamsiki* Aisha.

    Aisha: *Binuru,* tuonane asubuhi inshalla.

49. Mke: *Kwaheri* mume wangu.

    Mume: *Kwaheri* mwenzangu tutaonana wakati mwingine.

50. Mwanamke: *Kwaherini* jamani, tukutane juma lijalo.

Katika mfano wa arubaini na nane, baada ya masomo ya usiku mwanafunzi anamuaga Aisha kwa *alamsiki* na kuelekea kwenye bweni lake kupumzika naye Aisha anayelala katika bweni tofauti anamjibu *binuru* na kuongezea kuwa wangeonana asubuhi kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Wanafunzi hawa wanaagana kwa kila mmoja kumtakia mwenzake usiku mwema wanapoenda kulala. Katika mfano wa arubaini na tisa, mke anamuuga mume anayesafiri kwa *kwaheri* naye mume anamjibu *kwaheri* na kumuahidi kuwa wangeonana wakati mwingine. Mwisho katika mfano wa hamsini, baada ya mkutano mama mmoja anawaaga wenzake kwa *kwaheri* wanapofumkana.

Kihisishi *haya* kinapotumiwa pamoja na kituo na kutamkwa polepole kwa kidatu cha chini, huleta maana ya kwaheri. *Haya* pia hutumika katika kuwahimiza watu wanaofanya jambo fulani ili waharakishe au watie bidii. Katika muktadha huu, kihisishi *haya* kinarudiwa na kutamkwa kwa kidatu kinachopanda. Tazama mifano ifuatayo.

51. *Haya* mama, acha tuanie gari. Gari litakuja hapa hapa.

52. *Haya! Haya! Haya!* Tuharakishe, chunga begi lako, wanaoshuka kutoka juu *haya! Haya*! Njia ni moja, tupande vidatu, chunga mzigo, soko limehamishwa, baada ya vidatu nunua vitu.

Mfano wa hamsini na moja unaonyesha *haya* ya maagano. Baada ya mazungumzo, wageni wa mama wanamuaga na kumwambia kuwa gari lingewachukuwa hapo walipo. *Haya* katika mfano wa hamsini na mbili imerudiwa kuonyesha himizo. Feri inapotia nanga katika kivuko cha Likoni, mtangazaji katika feri anatumia kihisishi *haya* kuwahimiza abiria waharakishe kutoka kwenye feri na kuwaarifu kuhusu kuhamishwa kwa soko. Mbali na vihisishi vya maagano, vihisishi vya samahani hudhihirisha amali ya ujamilishi kama inavyobainika katika sehemu inayofuata.

### 3.2.8 Vihisishi vya Samahani

Matumizi ya vihisishi vya samahani yanahusisha vihisishi vya kuomba radhi na vihisishi vya kuomba nafasi: *samahani, kumradhi, pole, hashakum, kidogo, hebu* na *simile.* Mtu akimtendea mwenzake jambo la kuudhi ataomba msamaha kwa kutumia *samahani*.

*Samahani* pia hutumika katika kuomba radhi kwa kukosa kuhudhuria hafla au mkutano fulani uliokuwa umealikwa. Hili hutokea wakati unapokutana na mtu aliyekupa mwaliko. Matumizi ya *samahani* yanadhihirika katika mifano hii.

53. Babake Faruk, tumekuweka. *Samahani*, mambo ndo yamekuwa mengi.
54. *Samahani* ndugu kwa kukosa kuhudhuria arusi yako, siku hiyo nilipatwa na dharura.

Katika mfano wa hamsini na tatu, naibu wa mwalimu mkuu katika Shule ya Upili ya Tudor anamwomba radhi mzazi wa Faruk kwa kukawia kumhudumia. Anatumia *samahani* na kumwambia babake Faruk kuwa, shughuli ndizo zimekuwa nyingi. Katika mfano wa hamsini na nne, bwana mmoja aliyekuwa amealikwa harusini anapokutana na bwana harusi anaomba msamaha wa kutohudhuria harusi yake kwa kutumia *samahani* na kusema kuwa wakati wa harusi alipatwa na dharura.

Kihisishi *kumradhi* hutumika katika kuomba radhi jinsi kilivyo kihisishi *samahani*. *Kumradhi* pia hutumika wakati ambapo mtu anataka kufanya jambo ambalo litamlazimu kuwasumbua watu wengine. Kabla ya kufanya jambo hilo itambidi mtu huyo kutumia *kumradhi* au hata *samahani* katika kuomba ruhusa ya kufanya jambo hilo. Msemaji pia anaweza kuomba radhi kwa kutumia kihisishi *pole* kwa kumkosea mwenzake kwa njia moja au nyingine. Tazama mifano inayofuata.

55. Mwanafunzi: *Kumradhi* mwalimu, naomba kwenda msalani.
56. *Pole*, kwa kukuweka. We nenda, nikiwa tayari nitakuita.

Mwalimu anayefunza darasani katika mfano wa hamsini na tano, anaombwa ruhusa ya kutoka nje na mwanafunzi. Kwa sababu masomo yanaendelea, mwanafunzi hawezi tu kusimama na kusema anataka kwenda msalani, la, lazima atumie *kumradhi* kuomba samahani kwa sababu ya kutatiza somo linaloendelea. Katika hali hii mwanafunzi anaweza kuruhusiwa na mwalimu kutoka nje kwa sababu ya mwanafunzi kuwa na heshima. Mfano wa hamsini na sita unaonyesha mzee mmoja ambaye anatumia *pole* kumwomba dereva msamaha kwa sababu ya kumfanya amsubiri sana.

Kihisishi *hashakum* hutumika katika kumwomba mtu radhi kabla ya kusema jambo ambalo litamuudhi. Kwa mfano, waweza kusema *hashakum* sikutusi, kisha ukamtusi mtu. Wahojiwa wengi hawakuwa na ufahamu wa kihisishi *hashakum*. Kwa hivyo ilbainika kuwa kihisishi *hashakum* hakitumiki sana na watu katika maongezi yao ya kila siku katika jamii.

Neno *kidogo* halijaorodheshwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* kama kihisishi lakini ilibainika kuwa, *kidogo* hutumika kama kihisishi wakati mtu anapoomba nafasi ya kupita hasa katika magari ya usafiri. Badala ya watumizi kusema nipishe nipite, wamekuwa na mazoea ya kusema tu *kidogo!* Anayeambiwa *kidogo* huelewa kuwa anastahili kumpisha mwenzake. Pia, badala ya kusema subiri kidogo, *kidogo* kutumiwa peke yake na hivyo basi kuwa kihisishi. Kihisishi *simile* hutumika kwa maana sawa na *kidogo*. *Simile* hutumiwa na mtu anayetaka apewe nafasi ya kupita. Mtu anapotaka apewe nafasi ya kupita mahali ambapo kuna watu wengi na pengine hakuna nafasi ya kupita atatumia kihisishi *hebu* kuomba nafasi. Mifano ifuatayo inadhihirisha matumizi haya.

57. Abiria: *Kidogo!*

58. *Kidogoo!* Naja.

59. *Simile* dada!

60. *Hebu*, nipeshe tafadhali.

Katika mfano wa hamsini na saba, *kidogo* inatumiwa na abiria garini kuomba nafasi ya kupita ili aweze kushuka. *Kidogo* ya pili katika mfano wa hamsini na nane inatumiwa na mtu anayeitwa na mwenzake waende sokoni, naye anamwambia mwenzake asubiri kidogo ajitayarishe. *Simile* katika mfano wa hamsini na tisa, imetumika kumwomba dada nafasi ya kupita. Katika muktadha huu, *kidogo* inapotumika pekee inakuwa kihisishi kwa sababu ni usemi unaojisimamia. *Kidogo* inapotumika pamoja na kitenzi kwa mfano, *nipishe kidogo* inakuwa kielezi na wala si kihisishi tena. Katika mfano wa sitini, abiria garini anaomba nafasi ya kupita kwa kutumia *hebu* ili aweze kushuka. Katika muktadha huu *hebu* ya kuomba nafasi yaweza kutumika pekee yake na ilete maana iliyokusudiwa au iambatane na maneno mengine. Amali ya ujamilishi pia hudhihirishwa na vihisishi vya pongezi ambavyo vinajadiliwa katika sehemu inayofuata.

### 3.2.9 Vihisishi vya Pongezi

Pongezi hutolewa kwa mtu ambaye amefanikiwa au ametenda jambo zuri. Vihisishi *heko* na *hongera* hutumika kuwapongeza watu kwa mafanikio waliyoyapata. Pongezi hutarajiwa kumfanya msikilizaji ajihisi mshindi katika jambo fulani. Pongezi

zinapotolewa huonyesha uhusiano mzuri ulioko kati ya msemaji na msikilizaji na kuzidisha mtagusano kati yao. Tazama mifano ifuatayo.

61. *Hongera!* Umefanikiwa katika mtihani wako!
62. *Heko!* Ametoa shilingi elfu kumi, hebu tumpigie mgeni wetu makofi. Tena! Tena...

Katika mfano wa sitini na moja, mwanafunzi anapewa pongezi na mama kwa sababu ya kufanya vyema katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne. Mama anatumia kihisishi *hongera* huku akiwa na furaha na bashasha kumpongeza mwanawe. Katika mfano wa sitini na mbili, kiongozi wa Kanisa anawaongoza waumini katika kumpongeza mgeni wa heshima kwa mchango wake. Kiongozi huyu anatumia *heko* katika kutoa pongezi na kuwashirikisha waumini katika kumpigia mgeni makofi. Vihisishi vya pongezi: *hongera* na *heko*, mara nyingi huambatana na kushangilia kwingi kwa kupiga makofi na vigelegele.

Sehemu ya 3.2 imeshughulikia amali ya ujamilishi na imebainika kuwa, vihisishi huchangia katika kudumisha mahusiano mema ya kijamii. Amali jamilishi inahusiana sana na maana tagusani katika Sarufi Amilishi Mfumo ambayo ni kitengo tangamanishi cha matumizi ya lugha kutegemea vikwazo vya kimawasiliano katika jamii na ambayo huwawezesha watumizi wa lugha kudumisha mahusiano ya kijamii (Tazama §1.8.2.2). Ni dhahiri kuwa, msemaji hutumia vihisishi vya kubisha, vihisishi vya kukaribisha, vihisishi vya salamu, vihisishi vya kuita, vihisishi vya kuitika, vihisishi vya shukrani, vihisishi vya

samahani, vihisishi vya pongezi na vihisishi vya maagano ili kujenga uhusiano wa kijamii kati yake na msikilizaji. Vihisishi kama hivi vimetumiwa kuonyesha nia ya msemaji ya kuanzisha ama kumaliza mawasiliano na pia mwelekeo wake kwa usemi unaoendelea. Amali ya ujamilishi ina uhusiano wa karibu na amali ya unafsishi ambayo hudhihirisha hisia mbalimbali za msemaji.

### 3.3 Unafsishi

Noel (1989) anasema kwamba, lugha ni njia ya kudhihirisha hisia zetu. Kiini cha amali ya unafsishi ni akili ya msemaji na hutumika wakati msemaji anajaribu kuonyesha hisi au mwelekeo wake kwa kutumia lugha. Vihisishi kama sehemu ya lugha huwakilisha amali ya unafsishi na hili linadhihirika zaidi kutokana na fasili ya vihisishi kama maneno yanayodhihirisha hisia. Vihisishi vya unafsishi huonyesha hali aliyo nayo msemaji wakati wa mawasiliano kwa mfano uchungu, furaha, masikitiko, au hasira. Binadamu ni kiumbe wa kijamii na hakosi maingiliano na watu wengine. Katika maingiliano haya, lazima awahurumie walio na shida, afurahi na wanaofurahi na kulia na wanaolia, haya yote yanatekelezwa kupitia vihisishi vinavyoonyesha amali ya unafsishi. Vihisishi vinavyodhihirisha unafsishi ni kama, vihisishi vya mshangao, vihisishi vya kusihi, vihisishi vya dharau, vihisishi vya mshtuko, na vihisishi vya majuto.

#### 3.3.1 Vihisishi vya Mshangao

Mshangao ni hali ya kuduwaa na kutojua la kufanya kutokana na jambo lililotokea (TUKI 2013). Hali hii ya kuduwaa hudhihirishwa kupitia kwa vihisishi, na yaweza kuwa chanya au hasi kutegemea aina ya tukio. Vihisishi *ala*, *do*, *lahaula*, *kumbe*, *lo, wa*,

*salaale, ah, he, hei, enhee, aka, ati, o, haya, jamani* na *auuu* vilitumika katika kuonyesha mshangao. *Ala* hutumika kuonyesha mshangao na huleta dhana ya 'ni vipi?' *Do* vilevile hutumika katika kuonyesha mshangao. Zingatia mifano hii.

63. *Ala!* Kwa nini wanichokoza?

64. *Do!* Nyanyuka mtoto wewe, waangushwa na nini?

Katika mfano wa sitini na tatu, kihisishi *ala* kimetumiwa na msemaji kuonyesha mshangao kwa yale ambayo ameelezwa na mwenzake ambayo ni ya kumtania. Mfano wa sitini na nne unaonyesha mshangao ambapo mama anashangazwa na kuanguka kwa mtoto. Mama anatumia *do* kuonyesha mshangao na kumwomba mtoto anyanyuke baada ya kuanguka.

Kihisishi *lahaula* hutumika kuonyesha mshangao wa kuridhia kwa jambo lililokuwa likisubiriwa kwa hamu na kisha likatendeka. *Lahaula* hutamkwa taratibu kwa kidatu kinachopanda na kushuka. Kihisishi *kumbe* huonyesha mshangao wa kutokuwa na uhakika na kitu kilivyo au kilivyokuwa. Katika kustaajabu kwa jambo lililofanyika, *lo* hutumika na hutamkwa haraka. Kihisishi *haya* kinapotamkwa kwa kidatu cha juu na kuachiliwa mara moja pamoja na alama ya hisi huonyesha mshangao. Mifano ifuatayo inadhihirisha matumizi haya.

65. Mbona wanidanganya bwana, *kumbe* wewe mwongo. Mimi nataka kahawa chungu.

66. *Lahaula!* Izoo zimerudi, twende kwetu tukaangalie sinema. Twendeni.

67. *Lo!* Leo kuna tope kweli.

68. *Haya!* Ameanguka majini!

Kihisishi *kumbe* katika mfano wa sitini na tano, kimetumika na mteja katika mkahawa anayeshangazwa na mhudumu anayemletea kahawa tofauti na ile aliyoiagiza. Anashangazwa na uongo wa mhudumu ambaye haamini kuwa anaweza kuwa mwongo. Katika mfano wa sitini na sita, *lahaula* imetumiwa kuonyesha mshangao wa kuridhia na watoto waliokuwa wakisubiri kwa hamu na ghamu kurejea kwa nguvu za umeme zilizokuwa zimepotea. Baada ya kunyesha mvua kubwa, kunakuwa na matope mengi na mama mmoja anatumia kihisishi *lo* katika mfano wa sitini na saba kuonyesha mshangao kwa hali ya kuwa na matope. Katika amali ya ujamilishi (Tazama § 3.2.7), kihisishi *haya* kilitumika kuonyesha maagano. Mbali na ujamilishi, *haya* hudhihirisha amali ya unafsishi kwa kuonyesha mshangao. Katika mfano wa sitini na nane, *haya* inatumiwa na kijana mmoja baada ya kunyesha mvua kubwa, anatumia *haya* kushangaa anapomwona mzee aliyekuwa akisukuma baiskeli akianguka nayo kwenye kidimbwi cha maji.

Kihisishi *wa* hutumika kuonyesha mshangao katika jambo zuri au hata baya. Kurudiwa kwa *wa* huonyesha msisitizo. Vihisishi *salaale, ha, he, hei, o* na *auuu* hutumika pia katika kuonyesha mshangao kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

69. *Wa! Wa! Wa!* Umejipodoa kweli, e! Umeng'ara wewe!

70. Aa! *Salaale!* Wawili? Alhamdulillahi.

71. *O!* Jamani! Jamu yaenda mpaka 'airport.'

72. *Auuu! Lo!* Kwa nini alifanya hivyo? Hahaha!

73. *Hei!* Afurahisha huyo!

74. *He!* Hawa Waarabu vipi?

Katika mfano wa sitini na tisa, mvulana anamwona msichana na kushangazwa na jinsi msichana huyo alivyojipamba, na anaonyesha mshangao kwa kutumia kihisishi *wa* kinachokaririwa. *Salaale* katika mfano wa sabini imetumiwa kuonyesha furaha ya mama anayestaajabishwa na habari za mke wa mwanaye kujaliwa watoto pacha. Mfano wa sabini na moja unaonyesha mshangao ambapo dada mmoja anatumia *o* kuonyesha kushangazwa na mlolongo wa magari ambao umefika hadi uwanja wa ndege. Katika gumzo la vijana, kijana wa kwanza anasimulia jinsi mtu mmoja alivyokula chakula siku nzima bila kuchoka. Jambo hili linamstaajabisha kijana wa pili anayeonyesha mshangao mkubwa kwa kutumia *auuu* na *lo* na kisha kicheko. Kihisishi *hei* katika mfano wa sabini na tatu kimetumiwa na mpita njia kuonyesha mshangao kwa mtu anayefanya vituko vya kuwafurahisha watu barabarani. Mwisho katika mfano wa sabini na nne, *he* inatumiwa na mteja katika kinyozi anayeshangazwa na densi ya Waarabu katika sinema anayoitazama.

Katika sehemu ya 3.1, vihisishi *aka, ati,* na *enhee* vilidhihirisha amali ya uarifu. Mbali na amali ya uarifu, vihisishi *aka, ati,* na *enhee* pia hudhihirisha amali ya unafsishi kwa vile hutumika katika kuonyesha mshangao. Vihisishi *aka* na *ati/ eti* vikitamkwa kwa kidatu cha juu huonyesha mshangao kwa tukio fulani. Kihisishi *enhee* pia hutumika kuonyesha mshangao. Ilibainika kuwa, mbali na matumizi ya kukubali ambayo yanadhihirisha amali

ya uarifu (Tazama § 3.1.1), kihisishi *enhee* kikitamkwa kwa kidatu cha juu huonyesha mshangao.

75. *Aka!* Kumbe ni mwizi?

76. *Enhee!* Kumbe! Umezoea kuibia watu pesa, wafikiri watu wajinga eh!

77. *Eti!* Abubakari amefariki?

Katika mfano wa sabini na tano, *aka* imetumika na msemaji kuonyesha mshangao baada ya kugundua kuwa jirani yake ni mwizi. Kihisishi *enhee* katika mfano wa sabini na sita kimetamkwa kwa kidatu cha juu kuonyesha mshangao; mnenaji anashangaa anapogundua kuwa mhusika ameiba pesa. Msemaji katika mfano wa sabini na saba, anatumia *eti* kuonyesha mshangao baada ya kupokea habari za kifo cha Abubakari.

Kihisishi *aa* kikitamkwa kwa kidatu cha chini kinachopanda juu hutumika kwa maana ya kushangaa. *Aa* inapotamkwa kwa kidato cha juu hudhihirisha maumivu. *Aaa* inapotamkwa kwa kidatu cha chini katika vokali ya kwanza, kidatu kikapanda katika vokali ya pili na kushuka katika vokali ya tatu hutumika kuonyesha kukubali yaani ndiyo. Kihisishi *a* kikitamkwa kwa kidatu cha juu na kwa haraka hutumika kuonyesha kukata tamaa kwa msemaji. *Jamani* hutumiwa kudhihirisha mshangao kwa tukio ambalo ni la kushangaza. *Jamani* ya kuonyesha mshangao hutamkwa kwa haraka na kwa kidatu cha juu. Tazama mifano ifuatayo.

78. *Aa!* Salaale! Wawili? Alhamdulillahi.

79. *Aaa!* Umeyasikia ati, Zainabu kapewa talaka.

80. *A!* Dada tuyaache hayo.

81. O! *Jamani!* Jamu yaenda mpaka 'airport'

Katika mfano wa sabini na nane, mama anapata habari kuwa mke wa mwanaye amejaliwa watoto pacha. Kwa habari hizi mama anashangaa kwa kutumia *aa* kuonyesha furaha yake kwa habari hii njema. Katika mfano wa sabini na tisa, mwanamke mmoja katika maongezi yao anawaeleza wenzake jinsi Zainabu alivyopewa talaka. Mwanamke mwingine anachangia na kumsisitizia mwenzake kuwa ni ukweli kwa kutumia kihisishi *aaa* kuonyesha kuwa anakubaliana na yanayosemwa. Katika mfano wa themanini, dada mmoja anazungumza na mzee mwenye nyumba huku akilalamika kwa uchungu kuhusu masaibu ya wapangaji. Mwenye nyumba anamsikiliza na kumwambia dada kuwa atayashughulikia, lakini dada anaendelea tu na malalamishi. Mwenye nyumba anaonekana kuchoshwa na dada huyu na ndiposa anatumia kihisishi *a* kuonyesha kukata tamaa na kumwomba dada ayaache mambo hayo. Katika mfano wa themanini na moja msichana mmoja garini anatumia *jamani* kuonyesha mshangao kwa mlolongo wa magari yanayoenda kwa mwendo wa kobe na ambao umefika hadi uwanja wa ndege. Kutokana na uchambuzi huu, imedhihirika kuwa *aa* ni kihisishi ambacho huonyesha matumizi mbalimbali kutegemea jinsi kinavyotamkwa na pia idadi ya vokali zinazoongezwa au kupunguzwa kwa kihisishi hiki.

Kihisihi *oh* hutumika kuoyesha mshangao kinapotamkwa kwa kidatu cha juu na kuakifishwa kwa alama ya hisi. *Oh* huweza kuongezewa vokali ‘o’ mwanzoni au mwishoni. *Oh* ikiongezewa vokali hizi na kutamkwa kwa kidatu cha chini kinachopanda kisha kushuka hutumika kwa maana ya kuridhia. *Oh* pia hutumika kuonyesha masikitiko wakati inapotamkwa kwa kidatu cha chini na kufuatwa na nukta au kituo. Matumizi haya yanajidhihirisha katika mifano ifuatayo.

82. *Oh*! Mama Rahab, ni wewe!

83. O*ooh,* ndo maana wafungua ile akaunti?

84. *Ooh,* pole. Sasa umepona?

Katika mfano wa themanini na mbili, mlango unabishwa na mwenyeji anapoufungua, anashangaa kwa kutumia *oh* anapotambua kuwa mgeni wake ni mama Rahab. Katika mfano wa themanini na tatu, *oooh* imetumika kuonyesha kuridhia. Mwanadada mmoja anawaelezea wenzake manufaa ya kuweka pesa kwenye benki nao wanaridhia kwa *oooh* kuonyesha kuwa sasa wameelewa ni kwa nini mwanadada huyo aliifungua akaunti tajwa katika benki hiyo. Katika mfano wa themanini na nne, msemaji anamsikitikia mwenzake kwa kutumia *ooh* baada ya kumfahamisha kuwa alikuwa mgonjwa. Baadaye anamuuliza kama alikuwa amepona. Vihisishi vya mshangao vimeshughulikiwa katika sehemu hii, na imebainika kuwa msemaji huvitumia katika kudhihirisha hisia zake. Mbali na vihisishi vya mshangao, vihisishi vya kusihi pia hudhihirisha amali ya unafsishi kama inavyoshughulikiwa katika sehemu ifuatayo.

### 3.3.2 Vihisishi vya Kusihi

Kusihi ni hali ya kumwomba mtu kwa unyenyekevu atende jambo fulani. Msemaji anaponyenyekea anadhihirisha hisia zake kwa msikilizaji na vihisishi *tafadhali* na *jamani* hutumika. *Tafadhali* hutumika kumwomba mtu afanye jambo kwa heshima. *Tafadhali* ni kihisishi cha adabu na humfanya anayeombwa kukubali kulitenda jambo hilo kwa sababu ya heshima ya anayeomba. Katika kumsihi mtu ili afanye jambo fulani, *jamani* hutumiwa na hutamkwa kwa kidatu cha chini kinachopanda huku ikivutwa. Ni kama kumwambia mtu tafadhali. Mtu anapokataa kufanya jambo, msemaji atatumia *basi* ili kumsihi akubali kulifanya jambo hilo. *Basi* hutamkwa kwa kidatu cha wastani kinachoshuka. Zingatia mifano hii.

85. Tangazo la afya kwa watu wa Kwale, Kilifi na Mombasa mwezi wa Juni. Dawa za minyooo kwa watoto wa kati ya miaka miwili na kumi na minne. *Tafadhali* mjulishe jirani.
86. *Jamani*, twende tukanywe chai.
87. Mama we! Mtamuumiza, mwacheni *jamani!*
88. Njoo *basiii…*

Mfano wa themanini na tano unamrejelea mtangazaji katika gari la afya anayepita mjini akiwaarifu watu kuhusu huduma ya afya ambayo ingetolewa kwa watu wa Kwale, Kilifi na Mombasa mwezi wa Juni. Baada ya tangazo, anatumia *tafadhali* kumwomba na kumsihi kila mmoja aliyesikia tangazo hilo kumjulisha mwenzake ili kila mmoja aweze kuwapeleka watoto kupata dawa za minyoo. Katika mfano huu, msemaji anawasihi wasikilizaji ili wachukue hatua ya kuwapeleka watoto wao kupata dawa. Katika mfano

wa themanini na sita, wasichana wafanyakazi wa shirika la kijamii wanajumuika na kuweka mikakati ya kufanya kazi siku hiyo, kabla ya kufumkana mmoja wao anaanza kulalamika kuwa ana njaa na kuwasihi wenzake kwa *jamani* ili waende wakanywe chai. Katika mfano wa themanini na saba, mama anayeshuhudia mwizi akipigwa anawasihi wanaompiga kwa *jamani* kuwa wamwachilie wasije wakamuumiza. Katika mfano wa mwisho, msemaji anamsihi anayeitwa kwa kutumia *basi* ili akubali kwenda anakoitwa. Mbali na kusihi, msemaji anaweza kutumia vihisishi vya dharau kuonyesha hisia zake.

### 3.3.3 Vihisishi vya Dharau

Dharau ni tabia ya kutowathamini watu wengine au vitu. Vihisishi *Aaaa* na *Mmm* vinapotamkwa kwa kidatu cha wastani kinachoshuka huku vikivutwa, huleta maana ya dharau au kupuuzilia mbali kwa yanayosemwa. Dharau mara nyingine huonyeshwa watu ambao huonekana kutokuwa na manufaa au umuhimu wowote jinsi inavyodhihirishwa na mifano ifuatayo.

89. Ali: Wajua yule yuaweza kuwa mamako?

Salim: *Aaaa*, pengine nimwite anti tu.

90. *Mmm,* ni mlevi yule, achana naye.

Katika mfano wa themanini na tisa, Ali na Salim wanazungumzia watu maarufu na miaka yao kisha Ali anamwambia Salim kuwa mwanamke wanayezungumzia ana miaka mingi na hivyo yuaweza kuwa mamake. Salim anapuuzilia mbali hayo kwa kutumia *aaaa* ya dharau na kumwambia kuwa haiwezekani ila pengine amwite shangazi tu. Katika mfano

wa tisini, msichana analalamika kuhusu mtu anayemsumbua na mzee mmoja anamwambia asimsikize kwa vile mtu huyo ni mlevi. Mzee anatumia *mmm* kumpuuzilia mbali na kumdharau huyo mlevi.

Kihisishi *ebo* hutumiwa kuonyesha dharau hasa kwa watoto ambao wametenda jambo la kuudhi. Mtu mzima anapoona jambo hilo basi hutumia *ebo* ili kuwakejeli watoto hao waache kufanya kitendo hicho. Katika kutamka, kidatu huanzia chini na kupanda hadi juu. *Kefule, mavi,* na *mawe* hutumika kudharaulia mbali yanayosemwa na mtu, kuonyesha kuwa hukubaliani nayo. Maneno haya hutamkwa kwa kidatu cha juu kuonyesha kupinga yanayosemwa. Tazama mifano ifuatayo.

91. *Ebo* mtoto wewe, wafanya nini?

92. *Kefule!* Yaani wanidanganya mimi?

93. *Mavi!* Kwani yeye ni nani?

Katika mfano wa tisini na moja, *ebo* imetumika na mama anayeshangazwa na yale yanayofanywa na mtoto ambayo si ya kupendeza. Mama anatumia *ebo* kumkejeli mtoto, jambo linalomfanya mtoto aache analofanya kwa sababu ya aibu. *Kefule* katika mfano wa tisini na mbili imetumika na msichana mmoja anayeambiwa na mwenzake kuhusu zawadi aliyopata katika shindano la bahati nasibu. Baada ya kuambiwa hivyo, anaona kama uzushi na kuyapuuzilia mbali madai hayo kwa kutumia kihisishi *kefule.* Mvulana katika mfano wa tisini na tatu anamwambia mwenzake kuhusu jamaa mmoja ambaye amewatahadharisha wavulana hawa wasimchezee kwani wangeona cha mtema kuni.

Baada ya kuyasikia haya, kijana wa pili anayadharaulia mbali madai haya kwa kutumia kihisishi *mavi* na kumthubutu ajaribu aone.

Kihisishi *ati*, kikitamkwa kwa kidatu ambacho hakipandi wala kushuka hutoa maana ya kudhalilisha mtu na kudharaulia mbali anachofanya. *Ati* pia hutumika kuonyesha kutoamini jambo linalosemwa inapotamkwa kwa kidatu cha juu pamoja na alama ya kuuliza. Katika kuonyesha shaka kuhusu jambo fulani, *ati* hutumika na hutamkwa kwa kidatu cha wastani. Tazama mifano ifuatayo.

94. *Ati* waringa, waringia nini na hata kuoga mwenyewe hujui hapo ulipo.
95. *Ati* alisema tunamaliza pesa na hata ‘credit’ hatoi?
96. *Eti* mara daktari mkubwa hayuko, mara sijui nini.

Msemaji katika mfano wa tisini na nne anatumia *ati* kudharaulia mbali maringo ya msichana mmoja. Msemaji anaona maringo ya msichana huyu yakiwa hayana maana kwa vile anamwambia kuwa hata kuoga hajui. Katika mfano wa tisini na tano, wafanyikazi wa kikundi cha kijamii katika mazungumzo yao hawaamini kuwa mkubwa wao anaweza kulalamika kuhusu kutumia pesa vibaya ilihali hawapi pesa za kuwapigia wateja simu. Mmoja wao anatumia *ati* kuonyesha kutoamini kwake kuwa mkubwa wao anaweza kusema kuwa wanamaliza pesa. Mfano wa tisini na sita unaonyesha mama mmoja anayezungumzia jinsi alivyoshindwa kuwaelewa wauguzi katika hospitali moja

waliokataa kumruhusu ampeleke mgonjwa wake katika hospitali nyingine. Anaonyesha shaka ya jinsi walivyokuwa wakimzungusha kwa visingizio vidogo vidogo.

Kihisishi *khaa* huonyesha hasira. Kihisishi hiki hutumika wakati mtu anakasirishwa na yanayosemwa ambapo anayaona kama yasiyo na maana. *Po* na *poko* hutumika kuonyesha dharau kwa mtu. Wakati wa kutamka, vihisishi *po* na *poko* vyaweza kutamkwa pamoja na ishara ya kutema mate na hutamkwa kwa haraka. Ilibainika kuwa *po* hutumiwa sana na watoto. Matumizi ya *khaa*, *poko,* na *po* yanadhihirika katika mifano ifuatayo.

97. *Khaa!* Nini wewe!
98. Sitakwambia kitu *poko!* (akitema mate)
99. Hufaulu *po!*

Katika mfano wa tisini na saba, *khaa* imetumika na mvulana mmoja kwa mwenzake anayemsumbua. *Khaa* katika muktadha huu inaonyesha kuwa msemaji amekasirika na anayadharau yanayotendwa na mwenzake. *Poko* katika mfano wa tisini na nane, imetumika na dada mmoja kumdharau mwenzake kwa vile hajui kuficha siri. Anatamka *poko* pamoja na kutema mate na kumwambia kuwa hawezi kumfichulia siri kamwe. Katika mfano wa tisisni na tisa, msemaji anatumia *po* kudharaulia mbali juhudi za mwenzake kwa kumwambia kuwa hawezi kufaulu. Msemaji ana maana kuwa juhudi za mwenzake ni za bure na kamwe haziwezi kumsaidia. Hisia pia zaweza kuonyeshwa kupitia kwa vihisishi vya mshtuko vinavyorejelewa katika sehemu ifuatayo.

### 3.3.4 Vihisishi vya Mshtuko

Mshtuko ni hali ya kugutuka kwa ghafla. Mshtuko waweza kutokana na jambo baya lililotokea ghafla. Vihisishi: *mama we, woi, Mungu wangu, toba, yarabi* na *wacha* hutumika kuonyesha mshtuko na hutamkwa kwa kidatu cha juu. *Mama we*, *woi*, *toba*, na *yarabi* huonyesha mshtuko kwa jambo baya ambalo limetokea, linafanyika au lilikuwa karibu kutokea kama inavyodhihirika katika mifano inayofuata.

100. *Mama we!* Mtu yule atazama!

101. *Woi!* Nitaanguka kwa maji!

102. *Yarabi*! *Toba!* Roho yangu. Taratibu!

Mfano wa mia moja unarejelea mama ambaye njiani anamwona mtu wa baiskeli akikazana kujiondoa majini baada ya kunyesha mvua iliyosababisha mafuriko barabarani. Kwa mshtuko, mama anapiga mayowe kwa kutumia kihisishi *mama we* na kusema kuwa mtu yule angezama, ishara ya kutaka msaada kutoka kwa watu wengine. Katika mfano wa mia moja na moja, msichana mdogo anayeshiriki katika mchezo wa kuteleza anapiga yowe na kusema kuwa ataanguka majini baada ya kukaribia kidimbwi cha maji. Kihisishi *woi* katika mfano huu kinaonyesha mshtuko wa msichana huyu. Katika mfano wa mia moja na mbili, gari ambalo lilikuwa karibu kugongwa na lingine, linafanikiwa kuhepa na kuepuka ajali. Abiria mmoja baada ya kushuhudia kilichofanyika ndiye anaonyesha mshtuko kwa kutumia *yarabi toba*. Abiria huyu anashtuka na kumwita Mungu awasaidie. *Yarabi* ni kihisishi cha kumwita Mungu kwa sababu Rabi ni jina la kumtaja Mungu mlezi.

Mtu anapotenda jambo kinyume na matarajio, hushtuka kwa kusema *Mungu wangu* pengine kwa vile anafahamu matokeo ya jambo hilo. Kwa mfano, mtoto anaangusha bilauri kwa bahati mbaya kisha anashtuka na kusema, *"Mungu wangu!* Nitamwambia nini mama?" Hapa, mtoto anaonyesha mshtuko kwa kuvunja bilauri ya mama. Vihisishi vya mshtuko havikosi uwiano na vihisishi vya majuto ambavyo hudhihirisha pia amali ya unafsishi ambavyo vinajadiliwa katika sehemu inayofuata.

### 3.3.5 Vihisishi vya Majuto

Kihisishi *ole* hutumiwa kuonyesha majuto au masikitiko, kwa mfano wakati jambo baya limefanyika na unajisikitikia utasema: *Ole wangu! Ole* hutumika pamoja na vivumishi vimilikishi kutegemea wanaosikitikiwa. Kwa mfano, mama anamtaka mtoto afanye jambo fulani lakini mtoto analalamika kuwa yeye alifanya siku iliyotangulia, na kwa hivyo ni zamu ya nduguze. Mamake hataki kumsikiliza na anamlazimisha kwenda alikomtuma. Mtoto anaamua kwenda alikotumwa lakini kwa majuto ya *ole wenu* kuwalaani nduguze.

Amali ya unafsishi imejadiliwa katika sehemu hii na imebainika kuwa, msemaji hutumia lugha kudhihirisha hisia zake. Katika muktadha huu, si lazima msikilizaji awepo kwa vile msemaji anaweza kuonyesha hisia zake kibinafsi au mbele ya watu. Hivi ni kusema kwamba hisia hizi si lazima zielekezewe mtu. Muhimu hapa ni msemaji. Vihisishi vya hisia hudhihirisha tu hali ya kihisia anayoipitia msemaji wakati wa kuzungumza. Ikiwa hisia za msemaji zinaleta majonzi basi mhusika atahitaji kuliwazwa na watu wengine

kupitia kwa vihisishi vinavyodhihirisha amali ya uliwazi kama inavyodhihirika katika aya ifuatayo.

## 3.4 Uliwazi

Katika uliwazi, lugha inatumiwa kuwatuliza watu walio na shida fulani. Noel (1989) anasema kuwa, kuongea na watu kama vile marafiki, watu wa ukoo, washauri na madaktari, kwa watu wengi ndio njia ya kukabiliana na matatizo ya kibinafsi na kupata usaidizi katika kuyashughulikia matatizo haya. Vihisishi vya kufariji hutumiwa katika kuwafariji, kuwaliwaza, na kuwatuliza waliokumbwa na wasiwasi au shida mbalimbali.

### 3.4.1 Vihisishi vya Kufariji

Wakati wa msiba au wakati wa kuomboleza, vihisishi *makiwa, maskini, jamani,* na *pole* hutumika katika kuwafariji waliopatwa na msiba. Kihisishi *makiwa* kimetokana na nomino 'makiwa' yenye maana ya yatima; mtoto aliyefiwa na wazaziwe. Tazama mifano inayofuata.

103. Wafariji: *Makiwa.*

Waliofiwa: Tunayo.

104. Kijana: Acha nikwambie, nilimuuguza mama muda mrefu na dawa tulikuwa twanunua shilingi elfu moja kila siku.

Mwanamke: *Maskini! Poleni,* hiyo ni gharama kweli.

105. Mwanamke I: Tumemwuuguza babu muda mrefu!

Mwanamke II: *Poleni*! *Jamani poleni!*

Wakati wa msiba wa mtu kufariki, waliofiwa hufarijiwa kwa *makiwa*. Jibu la *makiwa* hutegemea ikiwa marehemu amezikwa au bado. Ikiwa amezikwa jibu litakuwa ‘yashapita’ na ikiwa bado jibu litakuwa ‘tunayo’. *Makiwa* hutumika kuwapa pole waliofiwa. Baada ya kutokea kifo, ndugu, jamaa na marafiki huwatembelea wafiwa kuwasaidia kuomboleza. Watu hawa wanapofika katika boma lenye msiba huwasabahi waliofiwa kwa *makiwa* ambao hujibu kutegemea jinsi hali ilivyo kama inavyodhihirika katika mfano wa mia moja na tatu. Msiba wa kuondokewa na mpendwa huleta huzuni na wasiwasi mwingi. Ilibainika kuwa wafiwa wanapotembelewa na jamaa na marafiki, hupata nguvu na uvumilivu baada ya kutulizwa kwa *makiwa*, kuongea na kukaa pamoja nao. *Makiwa* hutumiwa na wafariji kuwaelekezea waliofiwa.

Watu pia waweza kufarijiwa kwa mabaya yaliyowapata kwa kutumia vihisishi *maskini*, *jamani* na *pole*. Mbali na amali ya uliwazi, vihisishi *jamani* na *pole* pia hudhihirisha amali za unafsishi na ujamilishi (Tazama § 3.2.8, 3.3.1 na 3.3.2). Kihisishi *maskini* hutumika kumhurumia mtu aliyepatwa na maafa au aliyekosewa. Katika muktadha huu, msemaji anakuwa ameshuhudia au kusikia jambo baya lililomkumba msikilizaji na kwa hivyo anatumia vihisishi kuonyesha kuwa anamjali mwenzake. *Jamani* ni kihisishi cha kuonyesha huruma kwa jambo la kuhuzunisha lililotokea kama vile ugonjwa au kifo. Katika matumizi haya, *jamani* hutamkwa kwa kidatu cha chini. Kihisishi *pole* kikitamkwa kwa kidatu cha chini na kufuatwa na kituo, hutumika kuonyesha huruma kwa

jambo lililofanyika kama vile msiba au ugonjwa. *Pole* huwa ni njia ya kuwaliwaza au kuwafariji waliofikwa na jambo hilo.

Katika mfano wa mia moja na nne, kijana anamsimulia mwanamke mmoja jinsi walivyotumia pesa nyingi kumuuguza mama yao ambaye hatimaye aliaga dunia. Mwanamke anamhurumia kijana kwa kutumia *maskini* na *poleni* na kukubali kuwa ugonjwa huo wa mama uliwagharimu sana. Katika mfano wa mia moja na tano, mwanamke wa kwanza anamwelezea mwanamke wa pili jinsi walivyozunguka na babu yao wakimuuguza na kisha akaaga dunia. Baada ya kusikiliza, mwanamke wa pili anamjibu '*jamani poleni'* kwa upole na kwa masikitiko makubwa kuonyesha huruma kwa yote yaliyotendeka.

Kutokana na mifano hii, inabainika kuwa vihisishi vya kufariji: *maskini pole* na *jamani* vyaweza kutumika kila kimoja pekee au kwa pamoja lakini ujumbe ni ule ule wa kufariji na kutuliza. Kwa vile vihisishi hivi hutumika katika muktadha wa majonzi au shida, basi hutamkwa kwa kidatu cha chini na kwa upole.

Ukimuumiza mtu waweza kumfariji au kumpoza kwa kutumia kihisishi *pole.* Katika muktadha huu, *pole* hutamkwa kwa kidatu cha wastani na kwa unyenyekevu ili kumliwaza msikilizaji. Kihisishi *pole* chaweza kurudiwa ili kuonyesha kuwa msemaji anajutia kosa lake. Baada ya kazi au safari ndefu, kihisishi *pole* hutumiwa kumpoza aliyetoka safarini au aliyetoka kazini jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

106. Mama: We huoni wanikanyaga mguu?

Msichana: *Pole* sana mama, sikuwa nakuona.

107. Karibu! Karibu mume wangu, *pole* kwa safari.

108. *Pole* kwa kukuweka. We nenda, nikiwa tayari nitakuita.

Msichana katika mfano wa mia moja na sita anatumia *pole* kumtuliza mama kwa kumkanyaga kimakosa. Vilevile katika mfano wa mia moja na saba, mke anamkaribisha na kumtuliza mume wake kwa sababu ya uchovu wa safari. Katika mfano wa mia moja na nane, mzee mmoja anamtuliza dereva wa teksi kwa kutumia *pole* kwa sababu ya kumfanya dereva asubiri kwa muda mrefu.

Sehemu ya 3.4 imejadili amali ya uliwazi na imebainika kuwa vihisishi vya kufariji hutumiwa na msemaji kumrejelea msikilizaji ambaye amekumbwa na tatizo au msiba. Msikilizaji huliwazika kwa vihisishi *makiwa, pole, maskini* na *jamani* ambavyo husaidia katika kumpunguzia majonzi. Kihisishi *pole* pia kimedhihirisha matumizi ya kuwatuliza watu ama kwa uchovu au kwa kukosewa. Mbali na amali ya uliwazi, vihisishi pia hudhihirisha amali ya ukalimizi ambayo inashughulikiwa katika sehemu inayofuata.

### 3.5 Ukalimizi

Kwa mujibu wa Noel (1989), lugha huhusishwa na utekelezaji wa matambiko na sherehe kwa fomula fulani. Kupitia kwa matamshi au maandishi, tunatumia lugha kutekeleza

ahadi katika majukumu yetu kama wazazi, wafanyikazi, na wananchi kwa ujumla. Maombi ya binadamu kwa Mungu pia huhusisha matumizi ya fomula. Vihisishi hutumika katika kutoa ahadi au kutoa thibitisho au hata kutanguliza na kutamatisha maombi. Vihisishi vya kuapa na vihisishi vya dua hudhihirisha amali ya ukalimizi.

### 3.5.1 Vihisishi vya Kuapa

Kuapa ni kutamka jina la Mungu, mtume au mzazi kwa ajili ya kuthibitisha jambo au kitu (TUKI 2013). Kuna vihisishi vinne vya kuapa: *Wallahi, Billahi, Tallahi* na *haki ya Mungu* ambavyo hutumiwa katika kuapa ili kuthibitisha kwamba linalosemwa ni la kweli. Vihisishi *wallahi, billahi,* na *tallahi* vyaweza kutumika moja moja, viwili au hata vyote vitatu kwa pamoja hasa ikiwa anayeapa anataka kusisitiza kuwa hakutenda kabisa au hatatenda kamwe jambo fulani. Tazama mifano ifuatayo.

109. Kijana: *Wallahi* mimi sikuamini katu ulivyosema.

Mzee: Lakini kaka *wallahi billahi* mimi mwenyewe nimeyaona.

110. Mama: Kamwe! Nasema kamwe sitoi pesa mara ya pili.

Utanikoma eee, nakwambia utanikoma

Muuza maji: Mm! *Wallahi billahi tallahi* sitawahi waletea

maji tena.

111. *Haki ya Mungu* nikipata pesa nitakusaidia.

Katika mfano wa mia moja na tisa, kijana anatumia *wallahi* kuapa kuwa hakuamini aliyomwambia, naye mzee anatumia *wallahi billahi* kuthibitisha kuwa yanayosemwa ni kweli kwa vile yeye mwenyewe ameyashuhudia. Katika mfano wa mia moja na kumi, baada ya mama kukataa katakata kumpa pesa muuza maji, muuza maji anaapa na kutilia mkazo kuwa *wallahi billahi tallahi* hatawahi waletea maji tena hata wafanye nini. *Haki ya Mungu* katika mfano wa mia moja na kumi na moja inatumiwa na kijana anayeapa mbele ya mamake kuwa akifanikiwa kupata pesa atamsaidia ili kumwondolea lindi la umaskini.

Kwa kawaida, katika amali ya ukalimizi, utekelezaji wa sherehe au ahadi huhitaji watu maalumu kama vile mapadri au majaji. Viapo kwa mfano vya kuchukua uongozi baada ya uteuzi au uchaguzi hufanywa na majaji. Hii ni tofauti na vihisishi vya kuapa, kwa sababu ilibainika kuwa, watu huvitumia katika maongezi yao ya kila siku na kwa hivyo hakuhitajiki kuwa na mtu maalumu wa kuelekeza matumizi yake. Vihisishi vya kuapa hutumiwa na msemaji kutoa ahadi fulani ambayo anaapa kutekeleza au kukana jambo fulani ambalo anatuhumiwa kufanya. Vihisishi hivi hutumiwa tu kama thibitisho kuwa atatenda au hakutenda jambo fulani. Mbali na vihisishi vya kuapa, vihisishi vya dua hujumuishwa katika amali ya ukalimizi.

### 3.5.2 Vihisishi vya Dua

Dua ni maombi anayoombwa Mungu tu (TUKI 2013). Vihisishi vinavyorejelea dua vinaelekezwa kwa Mungu. Vihisishi *alhamdulillahi, allahuma, audhubillahi, bismillahi*,

*mashallah, inshallah, jazakallah,* na *amina* ambavyo vimekopwa kutoka kwa Kiarabu huhusika katika dua mbalimbali kutegemea matukio yanayotolewa dua.

Kihisishi *alhamdulillahi* hutumika katika kuanzisha baadhi ya dua kama vile dua ya kuamka ili kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukuamsha vyema. Mbali na dua, *Alhamdullillahi* hutumika katika kushukuru na kushangilia kwa mazuri yaliyopatikana. Katika maongezi yao ya kila siku watu hutumia *alhamdulillahi* kwa mambo yote mazuri ili kutoa shukrani kwa Mungu. Tazama mifano ifuatayo.

112. *Alhamdulillahi!* Nimefaulu!

113. Aa! Salaale! Watoto wawili? *Alhamdulillahi!*

114.Twashukuru,*alhamdulillahi!*

Katika mfano wa mia moja na kumi na mbili, *alhamdulillahi* imetumika na mwanafunzi ambaye anashangilia na kumshukuru Mungu kwa sababu ya matokeo mazuri katika mtihani wake wa kitaifa. Katika mfano wa mia moja na kumi na tatu, mama anashangilia kwa *alhamdulillahi* baada ya kupata habari ya mke wa mwanaye kujaliwa watoto pacha. *Alhamdulillahi* katika mfano wa mwisho imetumika na kina mama wanaomjibu mpita njia aliyewauliza kama ni wazima. Jibu lao lina maana kuwa sifa na shukrani ni kwa Mungu aliyewajalia uzima. Ilibainika kuwa kihisishi *alhamdulillahi* pia hutumika wakati wa kupiga chafya. Baada ya kupiga chafya, *alhamdulillahi* inafuata kwa maana ya kumshukuru Mungu. Ikiwa kuna mtu mwingine wakati wa kupiga chafya atasema: *yarihamkallah* kwa maana ya kumshukuru Mungu kwa niaba ya mwenzake.

Kihisishi *Allahuma* chenye maana ‘Ewe Mola’ hutumika katika kutanguliza dua nyingi kama vile: dua ya kuanza kula, dua ya kulala, dua ya kuingia chooni na dua nyingine nyingi. Kwa mfano, unapoingia chooni unatumia *allahuma* pamoja na maneno mengine kumwomba Mungu akuepushe na mashetani wabaya wa chooni. Watu wazima hutumia *Allahuma* wakati wa kutoa baraka kwa watoto kwa mfano, mkubwa anamshika mtoto kichwani na kusema: *Allahuma barikilau* kama mtoto ni mvulana. *Allahuma barikilaha* hutumika kama mtoto ni msichana.

Kiitikio cha dua au sala ni *amina/amin*. Kihisishi *amina* kina maana ‘na iwe hivyo ulivyoomba.’Kihisishi *amina* hutumiwa mwishoni mwa kila sala na pia katika mazungumzo ya kawaida kwa maana ya ‘na iwe vile umesema’ jinsi inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

115. Abiria: Tutafika *amin* inshallah.
116. Mgeni: Basi mimi naenda, tutaonana wakati mwingine.
     Mwenyeji: *Amina.*
117. Mungu na amuneemeshe. *Amina.*

Abiria garini katika mfano wa mia moja na kumi na tano anatumia *amin* katika maongezi ya simu akimjibu mwenzake kuwa na iwe vile amesema kuwa wafike Mombasa salama salimini kwa majaliwa ya Mwenyezi Mungu. Mgeni katika mfano wa mia moja na kumi na sita anamuaga mwenyeji na kumwambia kuwa wataonana wakati mwingine; naye mwenyeji wake anamjibu *amina* na iwe hivyo yaani wataonana wakati mwingine Mungu

akipenda. Katika mfano wa mia moja na kumi na saba, mzazi anamwombea mwanaye neema na kutumia *amina* mwishoni kwa maana kuwa mambo na yawe jinsi alivyoomba.

Kihisishi *audhubillahi* hutumika kumlaani shetani. Kihisishi hiki hutumiwa kumwomba Mungu akuepushe na mabaya. Kwa mfano, baada ya dereva kuepuka ajali anasema: "*Audhubilahi* wee! Kidogo tungechotwa, leo ni Mungu tu." Katika muktadha huu, dereva anatumia *audhubillahi* kwa maana ya Mungu amewaepusha na lori lililokuwa karibu kuwagonga. Ikiwa umekasirika na unawaza kumfanyia mabaya mtu aliyekukasirisha, unagutuka na kusema *Audhubillahi!* yaani Mungu akuepushe na mawazo ya kishetani. Vilevile ukiwa umelala na ukaota ndoto mbaya, ukizinduka kutoka usingizini utasema: *Audhubillahi!* Kihisishi *Audhubillahi* pia hutumika kuanzisha dua ya kumkemea shetani.

Kihisishi *bisimillahi* chenye maana ya kwa jina la Mwenyezi Mungu hutumiwa kabla ya kuanza jambo lolote hasa jambo zuri. Msemaji atatumia *bisimillahi* kabla ya kuanza chochote ili kupata baraka za Mungu katika kazi au katika jambo linalotekelezwa. *Bisimillahi* yaweza kutumika na maneno mengine kama *bisimillahi rahaman rahim* kwa maana ya kwa jina la Mwenyezi Mungu mwenye rehema na huruma.

*Inshallah* hutumika kwa maana ya kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Imani hapa ni kuwa, hilo jambo linalozungumziwa laweza tu kufanyika Mungu akipenda. Binadamu hana uwezo wowote kwa yoyote yatokeayo. Mtu yeyote hastahili kumwambia mwenzake kuwa kesho atafanya hivi na hivi bila kutumia *inshallah* kwa sababu aweza tu kuyatimiza

yote kwa mapenzi ya Mungu wala si kwa mapenzi ya mwanadamu. Matumizi ya *inshallah* yanajidhihirisha katika mifano ifuatayo.

118. *Inshallah heri*, tutafika Mombasa.

119. *Inshallah* nitajitahidi mara nyingine nipite mtihani.

120. Mwenyeji: Kwaheri tutaonana wakati mwingine.

Mgeni: *Inshallah!* Nyinyi mbaki salama.

Katika mfano wa mia moja na kumi na nane, *inshallah heri* inatumiwa na abiria ambaye ana imani kuwa, kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu safari yao itafikia ukingoni vizuri. Mwanafunzi ambaye hajafanya vizuri katika mtihani wake anatumia *inshallah* katika mfano wa mia moja na kumi na tisa kwa maana ya kuwa Mungu akipenda wakati mwingine atatia bidii ili afaulu katika mtihani wake. Katika mfano wa mia moja na ishirini, mwenyeji anamuaga mgeni na kumwambia kuwa wataonana wakati mwingine naye mgeni anaitikia kwa *inshallah* kuonyesha kuwa wataonana wakati mwingine kwa mapenzi ya Mungu.

Kumshukuru mtu aliyekutendea mema unasema *Jazakalla heri* kwa maana ya Mungu akuzidishie heri. *Jazakalla* pekee hutumika kwa mtu aliyekutendea mema au mabaya. Si sahihi kutumia *jazakalla* pekee katika kushukuru kwa sababu kihisishi hiki kina maana mbili: Mungu akutuze au Mungu akuadhibu. Katika kushukuru, *jazakalla* huambatishwa

na *heri.* Matumizi ya kihisishi *jazakalla* hutegemea jinsia: Wamaume – *jazakallahu heri,* wanawake- *jazakillah heri* na *jazakumullahu* hurejelea wingi wa wahusika.

Msemaji hutumia *mashallah* kumsifu mwenzake ikiwa ameona au kusikia jambo zuri kwa mwenzake. *Mashallah* ina maana ya Mungu akubariki au akuzidishie. Kihisishi hiki hutumika ili kumshirikisha Mungu katika yote unayoyasema na kujikinga na mabaya. Kihisishi *mashallah* hutumika kila wakati mtu anapomsifia mwenzake kama inavyoonyeshwa na mifano hii.

121. Una nywele ndefu. *Mashallah!*

122. Mimi ninashukuru, *mashallah* mke wangu yuajua kupika.

123. *Mashalla!* Kunani bwana, jionee mwenyewe!

Katika mfano wa mia moja na ishirini na moja, msichana mmoja anatamani nywele za mwenzake na badala ya kumwambia tu nywele zake ni ndefu, anatumia *mashallah* kusifia nywele zake kwa maana ya Mungu amzidishie zizidi kuwa ndefu. Mfano wa mia moja na ishirini na mbili unaonyesha maongezi kati ya wanaume kadhaa ambapo kunazuka swala la wanawake ambao wanaolewa lakini hawajui kupika. Wanawake hawa inasemekana kuwa hununulia jamii zao chakula mahotelini. Mwanamume mmoja anajigamba kuwa ana bahati kwa kuwa mkewe anajua kupika. Anatumia *mashallah* kumshukuru Mungu na kumwomba amzidishie mkewe kipaji hicho cha kupika. Katika mfano wa mwisho mvuvi mmoja anatumia *mashallah* kumwambia mwenzake ajionee mwenyewe jinsi Mungu alivyowabariki kwa samaki wengi tena wakubwa wakubwa.

Katika amali ya ukalimizi, ada maalumu hutekelezwa ili kuthibitisha jambo fulani au kumwomba Mungu. Watu huwasiliana na Mungu kwa kufuata mpangilio na kanuni mahususi. Kuna jinsi ya kuanza na kukamilisha maombi. Vihisishi vya kuapa pia vimedhihirisha amali ya ukalimizi kwa vile wasemaji huvitumia katika kudhihirisha kuwa wasemayo ni ya kweli. Amali ya ukalimizi ina uwiano na amali ya utendezi inayojadiliwa katika sehemu ifuatayo.

### 3.6 Utendezi

Katika amali ya utendezi, anayelengwa ni msikilizaji. Mskilizaji anastahili kutenda au kuhisi kulingana na matini. Msemaji anataka kumwathiri msikilizaji. Lugha inapotumiwa katika njia ya utendezi inataraji itikio kutoka kwa msikilizaji. Vihisishi vya kutuliza na vihisishi vya kuamrisha vinapatikana katika kundi hili.

#### 3.6.1 Vihisishi vya Kutuliza

Vihisishi katika kategoria hii hutumika kukomesha kelele au kupunguza ukali wa maumivu. Vihisishi *afya, chup, kelele, sss, hebu, jamani* na *usu* hudhihirisha dhima ya kutuliza. *Afya* huambiwa mtu anapopiga chafya na hasa mtoto ili kumtakia mema. Watu wazima hutamka *chup* kwa haraka ikiandama na ishara ya kidole kimoja kwa mdomo ili kuwanyamazisha watoto hasa kwa hasira. Wakati watu wanapiga kelele hunyamazishwa kwa kihisishi *kelele* ambacho hutamkwa kwa kidatu cha juu na hutumika kama amri ya kuwataka waache kelele. Wanaoongea wakisikia amri: *kelele,* wataacha kuongea. *Sss* na *usu* pia hutumika kama vihisishi vya kuwanyamazisha wanaopiga kelele. Tazama mifano ifuatayo.

124.*Afya!* Kulia juu chini kuna moto.

125.*Chup!* (na ishara ya kidole kwenye mdomo)

126.*Kelele!* (Shule ya msingi).

Ilibainika kuwa kihisishi *afya* hutumiwa na watu wazima kwa watoto wanapopiga chafya kwa mfano katika mfano wa mia moja na ishirini na nne, mama anatumia *afya* kumtakia uzima mtoto anayepiga chafya na kumhimiza kuendelea kukua bila kurudi nyuma kwani nyuma si kuzuri. Katika mfano wa mia moja na ishirini na tano, mtoto anayelia kwa usumbufu akitaka pipi ananyamazishwa kwa *chup*! (na ishara ya kidole kwenye mdomo). Kihisishi *kelele* katika mfano wa mia moja na ishirini na sita kimetumika na mwanafunzi mmoja kuwanyamazisha wenzake ishara kuwa amemwona mwalimu akija darasani.

Kihisishi *hebu* hutumiwa katika kuvuta usikivu wa mtu ama kumwambia asikize. Vilevile mtu anapotaka usikivu hasa kutoka kwa umati wa watu wanaopiga kelele atatumia kihisishi *jamani* kama njia mojawapo ya kuwataka wamsikilize. Katika muktadha huu, *jamani* hutamkwa kwa kidatu cha juu ili watu watulie au waweze kufanya wanaloombwa. Ilibainika kuwa vihisishi *hebu* na *jamani* mbali na kudhihirisha amali ya utendezi, hutumika katika amali ya ujamilishi (Tazama § 3.2.8 na 3.4.1) kuonyesha samahani na katika amali ya uliwazi kufariji mtawalia.

127. Mmm! *Hebu* we! (Kwa mtu wa maji) yaani mi ni wazimu. Si pesa ulipewa jana asubuhi?

128. *Jamani!* Mpeni nafasi awahutubie.

129. Mama we! Mtamuumiza, mwacheni *jamani*.

Katika mfano wa mia moja na ishirini na saba, mama anatumia *hebu* kwa muuzaji maji aliyekuwa akidai pesa za maji ili kumtaka asikize aweze kupewa maelezo kuhusu malipo ya maji. Kihisishi *jamani* kimetumika katika mfano wa mia moja na ishirini na nane kutaka usikivu kutoka kwa umati wa vijana wa bodaboda waliokuwa wamegoma kwa sababu ya barabara mbaya katika mtaa wa Majengo. Wanakataa kumsikiliza mwakilishi wa wodi wakidai kuwa wangependa kuhutubiwa na mbunge wa eneo lao. Kiongozi wa wanabodaboda anawatuliza kwa kutumia *jamani* ili wampe mwakilishi wa wodi nafasi awahutubie. *Jamani* katika mfano wa mwisho inatumiwa na mama ambaye anataka wanaompiga mshukiwa wamsikize na waache kumuumiza mshukiwa.

Kihisishi *basi* kikirudiwa mara nyingi na kutamkwa kwa kidatu cha chini hutumiwa kwa maana ya kumnyamazisha mtu anayelia na hasa mtoto mdogo. *Basi! Basi! Basi!* Wakati mwingine *basi* hutumika kumwamrisha mtu aache kuongea yaani anyamaze, kwa mfano: “*Basi!* Nyamaza!”*Basi* pia hutumika kuashiria kikomo au mwisho wa jambo; hakuna zaidi ya yaliyosemwa au yaliyofanywa. Neno hili hutamkwa kwa kidatu cha juu kudhihirisha amri. Kwa mfano, katika ugomvi mtu atasema: *“Basi* tosha!” Hii ina maana kuwa ugomvi usiendelee. Katika muktadha huu, kihisishi *basi* kinatumika kama amri kudhihirisha amali ya utendezi. Utendezi pia ulibainika katika vihisishi vya kuamrisha vinavyoshughulikiwa katika sehemu ifuatayo.

### 3.6.2 Vihisishi vya Kuamrisha

Neno *shughulika* linapotumika kama kihisishi, huashiria amri katika jeshi ya kuangalia upande wa kulia, kwenda hatua moja mbele na kisha kurudi nyuma kwa kupigapiga miguu ili kurudi katika mstari na kuhakikisha kuwa mstari umenyoka sawasawa wakati wa mafunzo ya gwaride (TUKI 2013). Ingawaje kulingana na kamusi kihisishi hiki hutumiwa na wanajeshi, ilibainika kuwa watu wa kawaida hutumia *shughulika* katika shughuli zao za kila siku kwa maana ya endelea na kazi yako au toka machoni pangu ukafanye uliloagizwa. Kwa mfano:

130. *Shughulika!* Waniangalia kama hunijui, si nimekwambia ukimbie marikiti!

Katika muktadha huu, kihisishi *shughulika* kinatamkwa kwa kidatu cha juu kuonyesha amri. Mama amemtuma mtoto lakini badala ya mtoto kufanya alichoagizwa anasimama na kuendelea kumwangalia mamake; kwa hasira mama anamwamrisha apotee kwa kutumia *shughulika*. Mtoto anastahili kupotea machoni pa mamake na kufanya alichoagizwa haraka iwezekanavyo.

Imedhihirika kuwa, vihisishi vya kutuliza na vihisishi vya kuamrisha vinatumiwa na msemaji kumwelekezea msikilizaji. Msikilizaji anatarajiwa kutenda kutegemea athari aliyopata kutoka kwa msemaji. Kwa ujumla, vihisishi katika amali ya utendezi vimetumiwa na msemaji kutaka usikivu, jibu au kitendo kutoka kwa msikilizaji. Vihisishi

katika amali ya utendezi vilivyoshughulikiwa katika sehemu hii vina uwiano na vihisishi katika amali ya uchangamshaji vinavyorejelewa katika sehemu ifuatayo.

### 3.7 Uchangamshaji

Lugha wakati mwingine hutumika katika kuwachangamsha wasikilizaji. Noel (1989) anasema kuwa, watu huchangamshwa na kufurahika kutokana na nyenzo za lugha kama vile vitendawili, michezo ya maneno, utani, nyimbo, mashairi, na hadithi. Kwa upande wa vihisishi, vitangulizi vya hadithi, na vihisishi vya kushangilia hudhihirisha amali ya uchangamshaji ambapo husisimua hadhira.

#### 3.7.1 Vihisishi vya Kutanguliza Hadithi

Katika utambaji, hadithi hutangulizwa kwa mitindo mbalimbali. Baadhi ya vitangulizi hivi hutumika kama vihisishi. Kitangulizi cha hadithi ni muhimu kwa vile kinakusudiwa kuleta nadhari ya hadhira na kuisisimua ili iweze kuwa tayari kwa hadithi. *Hadithi hadithi* ni mojawapo wa vitangulizi vya hadithi. Mtambaji hadithi atasema: *hadithi hadithi* nayo hadhira itamjibu *hadithi njoo*. *Paukwa* ni kitangulizi kingine cha hadithi ambapo jibu lake ni *pakawa.* Mtambaji aweza kurudia kitangulizi kabla ya kuanza kusimulia hadithi. Tazama mifano ifuatayo.

131. Mtambaji: *Hadithi hadithi!*

     Hadhira: *Hadithi njoo!*

     Mtambaji: Hapo zamani za kale paliondokea…

132. Mtambaji: *Paukwa!*

Hadhira: *Pakawa!*

Mtambaji: Paliondokea chanjagaa kajenga nyumba… (KLB 2009).

Vitangulizi vya hadithi hutolewa na msemaji kwa nia ya kumwathiri msikilizaji na kumweka tayari kuisikiliza hadithi. Msikilizaji ataathirika kwa vile vihisishi hivi vitaamsha ari yake, kumhamasisha kuwa makini kuisikiliza hadithi na kuifurahia. Msikilizaji akiwa makini anaweza kuifuatilia hadithi, kuifurahia na kuielewa vizuri. Uchangamshaji pia hudhihirika katika vihisishi vya kushangilia kama inavyobainika katika sehemu ifuatayo.

### 3.7.2 Vihisishi vya Kushangilia

Kushangilia ni kufurahia jambo lililotokea. Watu huonyesha shangwe na furaha kwa matendo mema ya Mungu kwa kutumia kihisishi *aleluya*. Mara nyingi wao hushangilia kuzaliwa na kufufuka kwaYesu Kristu mwana wa Mungu kwa kuimba *aleluya.* Katika michezo na mikutano ya hadhara kama ya kisiasa, watu hushangilia kwa furaha kwa vihisishi: *oyee*, *ripuripu,* na *huree. Ripuripu* na *huree* vyaweza kutumika kwa pamoja au kila kimoja pekee yake. *Huree* mara nyingi hutumiwa mwishoni mwa mchezo kuashiria tamati ya mchezo na pia wakati timu moja inapopata bao au alama. Vihisishi hivi huandamana na makofi, vifijo na nderemo kama inavyodhirika katika mifano ifuatayo.

133.Waziri: Serikali imetenga pesa za kununua feri ili kupunguza

msongamano.

Wananchi: *Oyeee!* (Wakipiga makofi)

134.Vijana: *Huree!* Tumeshinda! (Wanashangilia kwa vifijo pia).

Kijana: *Ripuripu* –

Vijana: *Huree!*

Katika mfano wa mia moja na thelatini na tatu, waziri anawahutubia wananchi katika kivuko cha Likoni. Katika hotuba yake, waziri anawaambia wananchi kuwa serikali imesikia malilio yao kuhusu uhaba wa feri na imepanga kununua feri zaidi ili kupunguza msongamano. Wananchi wanashangilia kwa *huree* na makofi kuonyesha furaha yao kwa ahadi ya serikali. Vijana wa timu ya kandanda ya Makadara, katika mfano wa mia moja na thelathini na nne, wanashangilia kwa *huree* na vifijo na nderemo kwa kupata ushindi wa magoli mawili kwa nunge. Katika kushangilia huku, kijana mmoja anaimba *ripuripu* na wenzake wanajibu *huree* na hili linaendelea kwa muda mrefu ambapo wote wanachangamka.

### 3.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia matumizi ya kihisishi cha Kiswahili na kuweza kujibu swali la pili. Imedhihirika kuwa, kihisishi cha Kiswahili kina matumizi mbalimbali kutegemea muktadha wa mawasiliano. Matumizi ya vihisishi yamedhihirishwa kupitia kwa amali saba za: uarifu, ujamilishi, unafsishi, uliwazi, ukalimizi, utendezi, na uchangamshaji

Katika amali hizi zote, umuhimu wa msemaji katika uzalishaji wa matini na umuhimu wa msikilizaji katika ufasiri wa matini umebainika. Haya yote yametekelezwa kutegemea muktadha wa mawasiliano jinsi zinavyosisitiza nadharia za Sarufi Amilishi Mfumo na Uchanganuzi Usemi Jadilifu. Baada ya kujadili matumizi ya kihisishi, sura ya nne itatoa hitimisho la utafiti.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

## 4.0 Utangulizi

Utafiti huu ulitekelezwa kwa lengo la kuchanganua kihisishi cha Kiswahili. Madhumuni ya uchanganuzi yakiwa kubainisha kanuni za maumbo mbalimbali na matumizi ya kihisishi cha Kiswahili, pamoja na madhumuni ya kuthibitisha ufaafu wa nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu katika kuchanganua kihisishi cha Kiswahili.

Kihisishi kama kategoria ya maneno hurutubu mawasiliano na kuyafanya yavutie, jambo ambalo linadhihirisha umuhimu wake katika mawasiliano. Mbali na kuwa kihisishi ni muhimu, ilijadiliwa katika sura ya kwanza kuwa kimepuuzwa na wasomi wengi, na wasomi wachache wanaokishughulikia wanakipa nafasi ndogo. Ingawa kihisishi hufunzwa katika shule za msingi na upili nchini, hakijachukuliwa kwa umuhimu mkubwa. Hali hii imesababisha vihisishi vingine kuacha kutumika au kutumika kwa nadra sana. Kutokana na swala hili, utafiti ulinuia kuchanganua kihisishi ili kudhihirisha kuwa kihisishi cha Kiswahili ni muhimu katika mawasiliano.

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu (UUJ) ikisaidiwa na Sarufi Amilishi Mfumo (SAM). Nadharia hizi zilitufaa katika utafiti huu. Katika UUJ, mhimili wa muundo wa usemi ulitumika ambapo usemi huhusisha matini, mahusiano na miktadha. Katika kufafanua matumizi ya kihisishi, mazungumzo kati ya msemaji na

msikilizaji yalitumika. Msemaji aliweza kuzalisha vihisishi ambavyo vilifasiriwa na msikilizaji kutegemea uhusiano wake na msemaji na pia muktadha wa mawasiliano. Mhimili wa muundo wa usemi kwa hivyo ulisaidia katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya vihisishi, mahusiano ya kijamii, na muktadha wa mawasiliano, ili kuweza kubaini matumizi mbalimbali ya vihisishi. Mhimili wa mbinu za uchanganuzi ulitumika katika kuchanganua matumizi tofautitofauti ya vihisishi ili kutoa maelezo, ufasiri, na ufasili wa kihisishi cha Kiswahili. Nadharia ya Uchanganuzi Usemi Jadilifu kwa hivyo ilitosheleza katika kuchunguza maswala ya kiisimujamii ambapo uhusiano katika ya msemaji na msikilizaji ulichunguza katika usemi. Hata hivyo, nadharia hii ilipungukiwa katika kuchunguza maswala ya kisarufi na kwa hivyo ikasaidiwa na nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo ili kufanikisha utafiti.

Mihimili ya Sarufi Amilishi Mfumo ilikuwa faafu. Katika mhimili wa muundo wa sarufi, utanzu wa pragmatiki ulitusaidia kuchunguza matumizi ya kihisishi katika muktadha wa mawasiliano ambapo iliweza kubainika kuwa kihisishi kimoja chaweza kuwa na matumizi mbalimbali kutegemea muktadha wa mawasiliano. Mhimili wa amali za maana ulitumika katika kufafanua matumizi ya kihisishi. Amali tatu za SAM ziligawanywa zaidi katika amali finyu za uarifu, ujamilishi, unafsishi, uliwazi, ukalimizi, utendezi, na uchangamshaji zilizodhihirisha matumizi mbalimbali ya vihisishi. Mhimili wa amali za kishazi ulitumika kuchunguza data lengwa ya utafiti ambayo ilikuwa vishazi huru ambavyo huwakilisha au hujumuisha kihisishi. Katika utafiti huu amali za maana na amali za kishazi zilitumika kwa pamoja bila kutenganishwa na basi kufanikisha utafiti.

Mbinu za maktabani na mbinu za nyanjani zilishirikishwa katika kukusanya data. Usomaji wa maktabani ulifanywa ili kupata taarifa kuhusu kihisishi kwa ujumla. Data ya utafiti wa nyanjani ilikusanywa katika mji wa Mombasa. Katika kukusanya data nyanjani, mbinu za mahojiano na uchunzaji zilitumika. Mbinu ya uchunzaji ilikuwa mwafaka zaidi katika utafiti huu kwa sababu mtafiti aliweza kutazama na kuwasikiliza watu katika hali halisi za shughuli zao. Vishazi vyenye vihisishi vilinakiliwa katika simu na baadaye katika daftari. Kunakili kwenye simu kulikuwa bora zaidi kuliko kunakili kwenye daftari moja kwa moja kwa vile watafitiwa hawakufahamu kuwa walitafitiwa na kwa hivyo walizungumza na kutenda mambo kihalisi. Mahojiano yalitumika sana shuleni kwani walimu na wanafunzi walielewa maana ya kihisishi na basi kujibu maswali vyema.

Sampuli makusudi na sampuli viwango iliyoteuliwa ilikuwa faafu na ilituwezesha kukusanya data. Usampulishaji faafu ulikuwa wa manufaa kwa vile mtafiti aliweza kuteua makundi mbalimbali ya watu; garini, njiani, mahali pa mapumziko, sokoni na kwenye mitaa mbalimbali ili kutazama na kusikiliza na hivyo kupata data iliyohitajika. Watafiti wasaidizi walirahisisha ukusanyaji wa data na kutuwezesha kupata data nyingi kwa haraka na hivyo kufanikisha utafiti. Baada ya ukusanyaji, data ilichanganuliwa kwa hatua tatu. Kwanza, data iliainishwa katika kategoria mbalimbali na kisha umbo la vihisishi likachanganuliwa kwa kutumia vigezo vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Katika hatua ya mwisho, uchanganuzi wa vihisishi kutegemea matumizi yake katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano ulifanywa. Baada ya uchanganuzi wa data, matokeo ya utafiti yaliweza kuwasilishwa katika sura nne kwa njia ya maelezo na majedwali.

## 4.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameangaziwa katika sura ya pili, na sura ya tatu. Sura ya pili imechanganua na kuainisha maumbo ya kihisishi cha Kiswahili. Maumbo ya aina tatu yalibainishwa: maumbo ya kifonolojia, maumbo ya kimofolojia na maumbo ya kisintaksia. Katika sura ya tatu, matumizi ya kihisishi cha Kiswahili yamejadiliwa kwa undani.

Maumbo ya kifonolojia yalidhihirika kwa kurejelea idadi ya silabi na ruwaza za kidatu. Kwa upande wa silabi, ilibainika kuwa kihisishi cha Kiswahili hujitokeza katika umbo la silabi moja na umbo la silabi nyingi. Umbo la silabi moja liliweza kugawanywa katika maumbo finyu zaidi ya vokali pekee, konsonanti silabi na konsonanti vokali. Maumbo ya silabi nyingi yaliyobainishwa yalikuwa: maumbo ya silabi mbili, maumbo ya silabi tatu, maumbo ya silabi nne, maumbo ya silabi tano na maumbo ya silabi nane. Ilibainika kuwa, umbo la silabi mbili lilijitokeza kwa wingi ikilinganisha na maumbo mengine.

Matokeo kuhusu maumbo ya kifonolojia pia yalidhihirisha kuwa, umbo la kiarudhi hutofautisha maumbo linganifu ya vihisishi. Maumbo ya kiarudhi yalidhihirisha ruwaza za kidatu na ruwaza za wakaa. Ruwaza za kidatu zifuatazo zilibainishwa katika kihisishi: juu, chini, kati, juu-chini, na chini-juu. Ilibainika kuwa, kidatu kinachoandama na wakaa huwa cha kiwango cha juu.

Kimofolojia, maumbo ya kihisishi yalibainishwa kwa kutegemea idadi ya mofimu. Maumbo yafuatayo matatu yalijitokeza: umbo la mofimu moja, umbo la mofimu mbili, na umbo la mofimu changamano. Umbo la mofimu moja lilishirikisha vihisishi ambavyo haviambishwi. Vihisishi vilivyo na mofimu moja viligawanywa zaidi katika umbo la mofimu sahili na umbo la mofimu ambatano. Vihisishi vya mofimu mbili pia vilibainishwa ambapo vilichukua ama viambishi awali au viambishi tamati. Pamoja na umbo la mofimu mbili, kihisishi cha Kiswahili pia kilijidhihirisha katika umbo la mofimu changamano. Vihisishi vya mofimu changamano huundwa kutokana na umahuluti. Umbo la mofimu changamano linaashiria uhusiano na umbo la kisintaksia.

Umbo la kisintaksia lilijidhihirisha katika kihisishi cha Kiswahili, kuhusiana na mpangilio wa kundi neno. Umbo la kundi neno liliwakilishwa na vihisishi ambavyo huundwa kwa maneno mawili au zaidi. Umbo la kundi neno liliweza kuchomoza makundi bayana ya kundi nomino na kundi hisishi. Kundi nomino liliwakilishwa na vihisishi vitatu ambavyo vilikuwa na nomino kama neno kuu. Katika kundi hisishi, neno kuu lilikuwa kihisishi, na jumla ya vihisishi viwili vilibainishwa. Vihisishi vilivyodhihirisha umbo la vijenzi viwili vilikuwa vya salamu na vilichukuliwa kuwa vishazi. Kishazi kama uwakilishi kilitumika katika kuchanganua umbo la vijenzi viwili.

Baada ya kuainisha maumbo ya kihisishi katika sura ya pili, sura ya tatu ilichanganua matumizi ya kihisishi cha Kiswahili na kuonyesha jinsi vihisishi hudhihirisha amali mbalimbali za lugha. Amali za uarifu, ujamilishi, unafsishi, uliwazi, ukalimizi, utendezi,

na uchangamshaji zilishughulikiwa ili kuonyesha matumizi mahususi ya vihisishi katika mawasiliano. Mifano ya vishazi vyenye vihisishi ilitumiwa ili kudhihirisha matumizi ya vihisishi katika miktadha ya mawasiliano.

Uarifu ni hali ya msemaji kumjuza msikilizaji ujumbe fulani. Ilibainika kuwa, msikilizaji baada ya kuupokea ujumbe wa msemaji, ni sharti aufasiri kutegemea muktadha wa mawasiliano ili aweze kumjibu msemaji. Msemaji alitumia vihisishi vinavyodhihirisha amali ya uarifu kupitisha ujumbe wake kwa msikilizaji. Vihisishi vya uarifu vilijumuisha: vihisishi vya kukubali, vihisishi vya kukataa, na vihisishi vya kutaka taarifa.

Katika amali ya ujamilishi, umuhimu wa msemaji na msikilizaji ulijitokeza ambapo wao hutumia vihisishi katika kudumisha uhusiano wa kijamii. Vihisishi vya kubisha, vihisishi vya kukaribisha, vihisishi vya salamu, vihisishi vya kuita, vihisishi vya kuitika, vihisishi vya shukrani, vihisishi vya samahani, vihisishi vya pongezi, na vihisishi vya kuaga hudhihirisha amali ya ujamilishi. Iligunduliwa kuwa, vihisishi katika amali ya ujamilishi mara nyingi hutumika pamoja kwa mfuatano ambapo mgeni anapofika atabisha, kisha akaribishwe, salamu zifuate, kisha mazungumzo, pengine shukrani na mwisho kuna kuagana kati ya mgeni na mwenyeji.

Amali ya unafsishi hudhihirisha mhemuko au mchomo wa moyo wa msemaji kwa jambo lililosemwa au lililotendeka. Vihisishi vinavyodhihirisha unafsishi huonyesha hali aliyonayo msemaji, na vyaweza kutokea msikilizaji awepo au asiwepo. Hoja hii ina

maana kuwa, msemaji hamtegemei msikilizaji ili kuvitumia vihisishi hivi, muhimu ni hali aliyomo msemaji. Vihisishi vya mshangao, vihisishi vya dharau, vihisishi vya kusihi, vihisishi vya mshtuko, na vihisishi vya majuto viliwekwa katika amali ya unafsishi.

Katika uliwazi, lugha hutumika kuwatuliza waliokumbwa na tatizo fulani. Ilibainika kuwa msemaji hutumia vihisishi vya kufariji katika kuwatuliza walio kwenye shida kama vile msiba na majonzi ya aina yoyote. Msikilizaji ambaye ndiye mwenye msiba huweza kuliwazika na kupunguziwa majonzi na vihisishi vya kufariji. Pamoja na kutumia vihisishi, ule utangamano na walio na msiba ulisaidia katika kuwapunguzia upweke na majonzi.

Ukalimizi ni amali ya lugha ambayo huhusisha utekelezaji wa matambiko au sherehe kwa fomula fulani. Vihisishi vya kuapa na vihisishi vya dua viliwekwa katika kikundi hiki. Ilibainika kuwa, watu hutumia vihisishi vya kuapa kuthibitisha kuwa watatenda jambo fulani ama kukana kutohusika na jambo wanalotuhumiwa kutenda. Vihisishi vya dua huelekezwa kwa Mungu; watu huwasiliana na Mungu kwa kufuata utaratibu maalumu.

Matumizi ya vihisishi pia yalijitokeza katika amali ya utendezi ambapo mlengwa ni msikilizaji. Vihisishi vya kuamrisha, na vihisishi vya kutuliza vilidhihirisha utendezi ambapo msemaji anamwelekezea msikilizaji ili kumwathiri. Msemaji, baada ya kumwathiri msikilizaji, anataraji itikio kutoka kwa msikilizaji. Msikilizaji anastahili kutenda kulingana na kihisishi kilichotumika.

Katika amali ya uchangamshaji, wahusika huchangamka kutokana na vihisishi vya kutanguliza hadithi na vihisishi vya kushangilia. Katika utambaji wa hadithi mtambaji hutumia vitangulizi vya hadithi ili kuisisimua hadhira na kuitayarisha kwa hadithi. Vihisishi vya kushangilia huwachangamsha wahusika katika shughuli zao hasa katika shughuli za furaha kama vile michezo na sherehe.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa, kihisishi cha Kiswahili kina maumbo mbalimbali na pia matumizi tofautitofauti. Matumizi ya kihisishi cha Kiswahili hutegemea uhusiano wa msemaji na msikilizaji na pia muktadha wa mawasiliano. Kutokana na matokeo haya ya utafiti tunapata mwanga wa kuandika mahitimisho ya utafiti.

**4.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Mojawapo ya malengo ya utafiti yalikuwa kudhihirisha umbo la kihisishi cha Kiswahili. Utafiti umechanganua umbo la kihisishi cha Kiswahili na kubainisha kuwa, umbo la silabi nyingi na hasa vihisishi vya silabi mbili vilijitokeza kwa wingi. Katika lugha, neno la silabi mbili huchukuliwa kuwa bora zaidi kwa sababu ya kudhihirisha toni kwa urahisi ikilinganishwa na neno la silabi moja. Tulitambua kuwa, umbo la kiarudhi liliweza kutofautisha maumbo linganifu ya vihisishi. Kutokana na hoja hii, utafiti unahitimisha kuwa, umbo la silabi mbili lilidhihirika kwa wingi kwa vile hubainisha kwa urahisi ruwaza za kidatu.

Vihisishi hutumika katika mawasiliano ya kila siku ya watu na huambatana na shughuli zao na hasa katika maongezi yasiyo rasmi. Kwa ujumla, utafiti umedhihirisha kuwa, vihisishi vya Kiswahili vyaweza kuendeleza lugha. Wasemaji hutumia vihisishi katika kuleta uhusiano mwema kati yao, kuonyesha hisia zao, kusifu, kuamkua, kukataa, kukubali na kadhalika. Matumizi haya hufanya vihisishi kuwa muhimu katika lugha ya Kiswahili na katika lugha zote za ulimwenguni kwa ujumla. Mahitimisho haya yanatoa nafasi kwa mapendekezo kuhusu utafiti zaidi.

### 4.3 Mapendekezo Kuhusu Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulichanganua kihisishi cha Kiswahili kwa kuegemea isimu, hasa utanzu wa pragmatiki. Kuna haja ya tafiti zaidi kufanywa kwa kuegemea utanzu wa isimujamii. Utafiti kama huu utasaidia katika kubaini ikiwa masuala ya isimujamii yanachangia au kuathiri matumizi ya kihisishi cha Kiswahili. Data ya utafiti ilipatikana nyanjani ambapo vihisishi vinavyotumika katika maisha halisi ya binadamu vilikusanywa. Utafiti zaidi waweza kufanywa kwa kurejelea vihisishi katika vitabu vya fasihi mathalani riwaya na tamthilia ili kuonyesha ikiwa kuna uhusiano kati ya vihisishi vinavyotumika katika kazi ya fasihi na vihisishi vinavyotumika katika maisha halisi ya binadamu. Utafiti wa aina hii unaweza kufanywa kwa misingi tofauti ya nadharia.

Pamoja na kutambua matumizi ya Kihisishi cha Kiswahili nyanjani, utafiti huu uligundua kuwa, baadhi ya vihisishi vilivyoorodheshwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* havitumiki nyanjani. Takribani vihisishi ishirini na vinne havikufahamika au kutumika na

watafitiwa. Vihisishi vya aina hii vinaweza kufanyiwa tafiti zaidi kwa misingi ya kietimolojia ili historia yake iweze kufahamika. Historia ya vihisishi hivi itatoa mwanga wa kwa nini matumizi yake yamedidimia katika jamii na kusalia vitabuni tu.

Katika uchanganuzi wa kihisishi, ilibainika kuwa matumizi ya kihisishi yaliweza kuathiriwa na ruwaza za kidatu. Vihisishi viliweza kutamkwa kwa kidatu cha juu, chini, kati, juu-chini au chini-juu. Ruwaza hizi zilishughulikiwa kwa kutajwa tu. Kuna haja ya utafiti zaidi kufanywa kuhusu tonisho katika kihisishi cha Kiswahili, utafiti ambao utaonyesha kwa michoro ruwaza mbalimbali za kidatu katika kihisishi na jinsi kidatu kinavyoathiri matumizi ya kihisishi cha Kiswahili.

Tafiti zilizopendekezwa hapo juu zina mchango kwa kihisishi cha Kiswahili. Matokeo ya tafiti hizi yatachangia katika kukielewa kihisishi kwa undani zaidi na hivyo kukizidishia umuhimu wa kimatumizi katika jamii. Tafiti kama hizi zikifanikiwa zitachangia katika kuuongezea utafiti huu thamani na basi kuinua thamani ya kihisishi kwa jumla. Vihisishi hurutubu na kufanikisha mawasiliano na havina budi kutiliwa maanani na kushughulikiwa na wataalamu na wasomi wa lugha kama zilivyo kategoria zingine za maneno.

**Marejeleo**


Abdulla, B.A & N. Z.Talib 2009. The meaning of interjections in English and Arabic. *Journal of the College of Arts*. University of Basiah. No. 50.

Ameka, F.K. 1992a. Interjections – the universal yet neglected part of speech. *Journal of Pragmatics*, 18: 101-118.

Ameka, F.K. 1992b. The meaning of phatic and conative interjections. *Journal of Pragmatics*, 18: 245-271.

Büyükkantarcioğlu**, N. 2006. An Analysis of Turkish Interjections in the Context of Reactive Idea Framing. Hacettepe University. 1/5s: 19-32.

Corver, N. 2010. "Interjections as Structured Root Expressions."Retrived from: Norbert. Abelcorver.com/…/

Eastman, C. M. 1983. Exclamations in Standard Swahili as Cultural Communication. *Journal of African Languages and Linguistics*, 5: 157-180.

Eastman, C. M. 1992. Swahili Interjections: Blurring Language-use/ Gesture-use Boundaries. *Journal of Pragmatics*, 18:273-287. doi:10.1016/0378-2166(92) 90055-G

Fairclough, N. 1989. *Language and Power*. London: Longman.

Fairclough, N. 1995. *Critical Discourse Analysis*: *The Critical Study of Language (Language in Social Life Series).*London: Longman.

Habwe, J. & P. Karanja. 2004. *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. A. K. 1985. *An Introduction to Functional Grammar.* London: Arnold.

Halliday, M. A. K. 1994. *An Introduction to Functional Grammar*. *(2nd edition).* London: Arnold.

Halliday, M. A. K. & C. Matthiessen. 2004. *An Intoduction to Functional Grammar (3rd Edition)*. London: Arnold.

Huang, Y. 2007. *Pragmatics.* UK: Oxford University Press.

Jovanovic, V. Z. 2004. The Form, Position and Meaning of Interjection in English. *Facta Universitatis. Series: Linguistics and Literature*, 3(1): 17-28.

Kariuki, J. G. 2012. Makosa ya Kisintaksia Katika Uandishi wa Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Shule za Upili. Unpublished MA Thesis. Kenyatta University.

Kihore, Y. M., D. P. B. Massamba, & Y. P. Msanjila. 2003. *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

KIE. 2002a. *Ministry of Education Primary Education Syllabus.*Vol.1. Nairobi: KIE.

KIE. 2002b. *Ministry of Education Secondary Education Syllabus.* Vol.1.Nairobi: KIE.

Kindija, K. A. 2012. *Taaluma ya Fonetiki Matamshi*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

KLB. 2009. *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 2 Kitabu cha Wanafunzi.* Nairobi: KLB.

King'ei, K. 2010. *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kockleman, P. 2003. The Meaning of Interjections in Q'eqch Maya from Emotive Reaction to Social and Discursive Action. *Current Anthropology,* 44 (4): 467 – 490. WWW. Colombia edu/… Article% PDFs/ interjections…2003.

Kothari, C. R. 2004. *Research Methodology. Methods & Techniques.* New Delhi: New Internatinal (P) Limited Publishers.

Leech, G. 1983. *Principles of Pragmatics.* England & New York: Longman Group Limited.

Levinson, C. S. 1983. *Pragmatics*. London: Cambridge University Press

Lyons, J. 1968. *Introduction to Theoretical Linguistics*. UK: Cambridge University Press.

Matei, K. A. 2008. *Darubini ya Sarufi. Ufafanuzi wa Sarufi.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Matrood, B. S. 2010. Interjections in English: An Interlingual Pragmatic Study. Thesis. University of Al-Qadisiyia.

Mbaabu, I. 1992. *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Moore, A. 2001. *Phonology*. http/www.shunsley.eril.net/amoore/

Mugenda, A.G. 2013. *Qualitative Research Methods Introduction.* Nairobi: ARTS Press.

Mugenda, O. M. and A. G. Mugenda. 1999. *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: African Centre for Technology Press.

Mumbo, C. K., O.Ngamia. F. Maneno & H. Mogambi. 2004. *Johari ya Kiswahili Kidato cha pili*. Nairobi: EAEP.

Ndalu, A. 1997. *Mwangaza wa Kiswahili.* Nairobi, Kampala: EAEP.

Nerlich, B. & D.D. Clarke. 1997. "Language, Action and Context. The Early History of Pragmatics in Europe and America, 1780-1930." *Studies in the Theory and History of Linguistic Science*, Volume 80, xii + 497pp.

Ngugi, B. 2014. Umilisi wa Stadi za Maamkizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Unpublished Ph. D Thesis. Kenyatta University.

Nguyen, T. K. P. 2011. A Study of Lingustic Features of Interjections in English and Vietnamese. M.A Thesis: University of Danang.

Njogu, K., A. Mwihaki, &A. Buliba. 2006. *Sarufi ya Kiswahili*: *Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: JKF.

Noel, W. 1989. *Language and Communication: An Introduction.* New Zealand: Dunmore Press.

Ohly, R. 1985. The Exclamation Mark in Kiswahili. *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi*

*wa Kiswahili*. Juzuu 52/1 & 52/2: 93-105.

TUKI, 1990. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI, 2013. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3)* Nairobi: Oxford University Press.

Waihiga, G. 1999. *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.

Waihiga, G. and Y. P. Wamitila. 2003. *Chemichemi za Kiswahili*. *Kidato cha Pili* . Nairobi: Longhorn Publishers.

Wierzbicka, A. 1992. The Semantics of Interjections. *Journal of Pragmatics,* 18:159-192.

Wodak, R. 2002. Aspects of Critical Discourse Analysis. *ZfAL*, 36: 5-31.

Yahya-Othamn, S. 1998. Kiswahili Interjections Revisited. *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Juzuu 61: 53-71.

Yule, G. 1996. *Pragmatics.* UK: Oxford University Press.

(www.reference.com/ browse/ interjection.) Downloaded on 10/1/2015.

www.alhidaaya.com/sw/node/1799. Downloaded on 21/8/2015.

## KIAMBATISHO A: DATA YA UTAFITI

Data ya utafiti ilikusanywa kutoka kwa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na nyanjani. Data hii imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imeshughulikia data msingi kutoka kwenye kamusi na sehemu ya pili inaorodhesha data kutoka nyanjani. Data imepangwa kwa njia ya majedwali.

### 1. Data kutoka kwenye Kamusi ya Kiswahili Sanifu

Data iliyokusanywa kutoka kwenye kamusi imegawanywa kwenye kategoria nne kwa kutumia kigezo cha etimolojia. Kategoria hizi zimejumuisha msingi, upili, mkopo na mkopo upili.

#### i. Vihisishi Msingi

Vihisishi msingi ni maneno ambayo kiasili ni vihisishi, hayajaundwa kutokana na maneno mengine (Ameka 1992a, Wierzbicka 1992). Maneno haya yanaweza kujisimamia kama semi na kwa kawaida hayaingii katika miundo na kategoria zingine za maneno.

| | Kihisishi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Aa! | Neno la kuonyesha mshangao, furaha au kukubali. |
| | | Neno la kuonyesha uchungu. |
| 2 | A-a! | Neno la kuonyesha kukataa |
| 3 | Abaa! | Neno la kumwita rafiki |
| 4 | Abee! | Neno la kuitika mtu, hasa mwanamke anapoitwa |
| 5 | Abwe! | Tamko la kushangilia jambo lisilo la kawaida. |
| 6 | Ache! | Neno la kumtakia mtu furaha na ufanisi hasa katika sherehe kama vile harusi au jando. |
| 7 | Ah! | Neno la kuonyesha kukerwa na kitu au jambo. |
| 8 | Ahaa! | Huonyesha furaha, mshangao au kukubali. |
| 9 | Alaa! | Neno lionyeshalo kuelewa kwa jambo. |
| 10 | Ati/ eti! | Neno la kufanya mtu asikilize. |
| | | Neno la kuonyesha shaka juu ya jambo fulani. |
| | | Neno la kuonyesha dharau |
| 11 | Chup! | Neno la kumwambia mtu anyamaze hasa kwa dharau/ hasira. |
| 12 | Do! | Tamko la mshangao |
| 13 | Ee! | Neno la kumwita mtu kwa dharau. |
| | | Hutumiwa na wakristo katika sala kumwita Mwenyezi Mungu. |
| 14 | Ehaa! | Neno la kuitana kwa watu walio mbalimbali hasa wavuvi. |
| 15 | Ehee/ enhee! | Huonyesha ukubaliano au hamu ya kuendelea kusikiliza |
| 16 | Enyi! | Ufupisho wa ee nyinyi. |
| 17 | Epuu! | Tamko litumiwalo kuainisha kutompa mtu nguvu ya kufanya aliloambiwa afanye au ya kumtaka asiamini analoambiwa. |
| 18 | Ewaa! | Kukubali au kuafiki jambo. |

| | | |
|---|---|---|
| 19 | Ewe! | Mshangao.<br>Ufupisho wa ee wewe. |
| 20 | Fyoto! | Tamko la kuonyesha uhodari linaloweza kusababisha hasira kubwa; tamko la kumjaribu mtu kama anaweza kukabili tendo. |
| 21 | Ha! | Huonyesha mshangao. |
| 22 | Habi! | Neno aambiwalo mtu aliyepandwa na shetani na akawa mkali sana na kujipigapiga huko na huko; kupunguza hasira. |
| 23 | Hae! | Tamko litumiwalo kuonyesha huzuni na kulia au kusikitika. |
| | | Tamko litumikalo katika kuitikia nyimbo au ngano |
| 24 | Haika! | Neno la kukubaliana na maneno ya shetani anayesema na watu kwa utulivu. |
| 25 | Hainehaine! | Tamko litumikalo kuelezea uchukuaji wa kitu juu kwa juu na kutumia nguvu. |
| 26 | Halumbe! | Neno linalotumiwa kutilia mkazo katika kupiga halambe. |
| 27 | Halwoho! /ho! Waho! | Tamko l kuonyesha mshangao |
| 28 | Hario! | Tamko la kushangilia. |
| 29 | Harioe! | Tamko la furaha wakati meli inapoonekana baharini ikielekea bandarini. |
| 30 | Hasha! | Hapana. |
| 31 | He! | Neno la kumhadharia mtu. |
| | | Neno la kudhihirisha chuki au kutopendezwa na jambo. Neno la kuonyesha dharau. |
| 32 | Hebu/ ebu! | Neno linalotumiwa kuvuta usikivu wa mtu. |
| | | Nipe nafasi. |
| 33 | Heko! | Shangilio la kumpongeza mtu. |
| 34 | Hewaa/ ewaa! | Neno linalotumiwa kwa maana ya kukubali au kuafiki jambo. |
| 35 | Hewala! | Tamko la kuridhia. |

| | | |
|---|---|---|
| 36 | Hobe! | Neno lionyeshalo matakwa ya msemaji kwa wema au kwa ubaya. |
| 37 | Hodi! | Neno la kubishia mlango.<br>Uombaji ruhusa ya kuingia. |
| 38 | Huree! | Neno la kushangilia. |
| 39 | Jamani/ jama | Neno la kutaka usikivu wa watu.<br>Neno la kuonyesha mshangao. |
| 40 | Jabwe! | Tamko la kejeli. |
| 41 | Ka! | Tamko la kuonyesha mshangao. |
| 42 | Kambirani! | Potelea mbali; lolote na liwe. |
| 43 | Kamwe! | Hutumiwa kwa kutilia nguvu pamoja na kukanusha jambo.<br>Hutumiwa kutilia mkazo au mshangao. |
| 44 | Keba! | Tamko la shangwe katika sherehe za harusi. |
| 45 | Kefle/ kefule | Neno la kutukana lenye kueleza hasira ya msemaji kwa anayemlaani.<br>Hutumika kuonyesha mshangao. |
| 46 | Khaa! | Neno la kuonyesha kukasirika. |
| 47 | Kulikoni! | Kulikuwa nini. |
| 48 | Kunani! | Kuna nini. |
| 49 | Kwaheri! | Tamko la kuagana na kumtakia mtu heri na salama. |
| 50 | Labeka! | Tamko la unyenyekevu la kuitikia. |
| 51 | Lo! | Neno la kuonyesha mshangao, furaha au hofu. |
| 52 | Mashalla! | Tamko la furaha la kumwombea mtu Baraka au mema kwa kitu ulichokiona au kukisikia kutoka kwake. |
| 53 | Mmh! | Tamko la kukubali. |
| 54 | Nambo! | Neno linalotumika kumwashiria mtu kuwa asifanye jambo fulani. |
| 55 | Ndiyo! | Neno linalotumika katika kukubali. |

| | | |
|---|---|---|
| 56 | Ng'o! | Neno litumikalo kusisitiza kukataa. |
| 57 | Nobe! | Hutumika kuonyesha hali ya kudharau mtu. |
| 58 | Nyoo! | Neno la kuonyesha dharau. |
| 59 | Nyungwa! | Neno linaloonyesha kutaka kuwatanabahisha wenzio ambao unazungumza nao. |
| 60 | Ohaa! | Aisee |
| 61 | Ole! | Neno litumiwalo kuelezea majuto au masikitiko. |
| 62 | Oyee! | Tamko la kushangilia. |
| 63 | Pakawa | Neno linalotumiwa kumwitikia mtambaji hadithi anapotaka kuanza kutamba. Swali lake ni paukwa. |
| 64 | Po! | Neno linalotumika kwenye michezo ya watoto ili kuonyesha dharau |
| 65 | Poko! | Neno litumikalo kuonyesha dharau. |
| 66 | Pukachaka! | Neno linalotumiwa kubeza au kudharau kitu kwa kutokithamini kabisa. |
| 67 | Ripuripu! | Tamko la furaha au la pongezi ambalo, aghalabu hutumiwa baada ya kumalizika au kufaulu kwa jambo fulani. |
| 68 | Salalaa/ Salalee! | Tamko la kuonyesha mshangao. |
| 69 | Twaibu! | Kiitikio cha kuthibitisha kuwa kisemwacho ni sawa, ndivyo na kinakubalika. |
| 70 | Wee! | Neno linalotumika kumwita mtu aghalabu kwa dharau au kumwonya. |
| 71 | Zii! | Tamko linalotumiwa kuzomea au kutoafikiana na mtu au jambo. |

**ii. Vihisishi Upili**

Vihisishi upili ni maneno ambayo huzalishwa kutokana na kategoria zingine za maneno kama vile nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi na viwakilishi.

| | **Kihisishi** | **Maelezo** |
|---|---|---|
| 1 | Acha! | Huonyesha mshangao. |
| 2 | Aka! | Tamko la kuonyesha mshangao.<br>Tamko la kukanusha. |
| 3 | Ala! | Neno linaloonyesha mshangao au mshtuko. |
| 4 | Ama! | Huonyesha mshangao. |
| 5 | Amba! | Neno la kukubali jambo |
| 6 | Anza! | Thubutu. |
| 7 | Babu! | Hutumiwa na wanawake kuitana. |
| 8 | Basi! | Neno la kuonyesha kikomo au mwisho wa jambo. |
| 9 | Biri! | Neno litumikalo kupa mtu changamoto kuwa hawezi kufanya jambo fulani na kama anaweza na ajaribu. |
| 10 | Buu! | Kaa kimya. |
| 11 | Bwana! | Neno la kumgutusha mtu au kumfanya asikilize. |
| 12 | Dole! | Sawa. |
| 13 | Hadithi! Hadithi! | Mwito wa mtu anayedhamiria kuanza kusimulia hadithi. |
| 14 | Hadithi njoo! | Kiitikio cha mwito wa ‘hadithi! Hadithi! |
| 15 | Hai! | Neno lionyeshalo nia ya kutaka kupoza jambo lisiendelee |
| 16 | Halambe/ harambee | Mwito wa kutia moyo watu ili kuweza kusukuma au kuvuta kitu kizito kwa pamoja.<br>Mwito wa kuwahamazisha wananchi kushirikiana kuchangia mendeleo yao. |

| | | |
|---|---|---|
| 17 | Hasa! | Ndio! |
| 18 | Hata! | Sivyo |
| 19 | Haya! | Sawa. |
| | | Neno la kuhimiza au kutayarisha watu kufanya jambo. |
| 20 | Hivyo! | Kama ilivyoelezwa. |
| 21 | Hongera! | Neno linalotumiwa kumpongeza mtu kwa mafanikio aliyopata. |
| 22 | Kabisa! | Hata kidogo. |
| 23 | Karibu! | Neno litumiwalo kumwitikia mtu aliyebisha hodi au wakati wa kukaribisha mtu. |
| | | Neno litumiwalo kumuaga mtu anayeondoka. |
| 24 | Katu! | Hata kidogo. |
| 25 | Kelele! | Tamko la kutaka kumnyamazisha mtu anaposema. |
| 26 | Kongoni! | Tamko litumikalo kwa kumkaribisha mtu. |
| 27 | Makiwa! | Tamko la kumpa pole mtu aliyefikwa na msiba mkubwa. |
| 28 | Mbwedu! | Tamko linalotumika kudharau kitu au mtu. |
| 29 | Pole! | Tamko la kumliwaza mtu aliyefikwa na jambo baya. |
| | | Neno la kumpoza mtu anayefanya kazi au aliyetoka safarini au kazini. |
| 30 | Riboribo! | Tamko la kuonyesha furaha na shangwe. |
| 31 | Saa! | Neno linaloonesha kushangaa au kuhimiza afanye jambo. |
| 32 | Sefule! | Tamko la kuonyesha dharau au kuchukiwa na yule anayeambiwa, hasa mtoto. |

### iii. Vihisishi Mkopo

Vihisishi mkopo ni maneno ambayo huundwa kupitia mbinu ya kuazima maneno kutoka kwa lugha zingine. Vihisishi mkopo vya Kiswahili vimeazimwa kutoka kwa lugha zifuatazo: Kiarabu, Kiingereza, Kituruki, Kiibrania, Kiajemi, Kijerumani, Kihindi na Kireno.

**Vihisishi Vilivyokopwa kutoka kwa Kiarabu**

| | Kihisishi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Abadan! | Neno linalotumika kusisitiza jambo linalokanushwa; hata kidogo. |
| 2 | Afanalek! | Hutumika kuonyesha mshangao. |
| 3 | Alamsiki! | Neno la kuagana wakati wa jioni na usiku. |
| 4 | Aleikum salaam! | Mwitikio wa salamu za amani |
| 5 | Alhamdulillahi! | Sifa zote ni za mwenyezi Mungu tu (hutumika kuonyesa shukrani) |
| 6 | Allahuma! | Neno linalotumika kumwomba Mwenyezi Mungu dua |
| 7 | Amin/ amina! | Kiitikio cha dua /sala (na iwe hivyo) |
| 8 | Bilahi! | Neno linalotumika kuapa katika jina la Mwenyezi Mungu. |
| 9 | Binuru! | Kiitiko cha alamsiki. |
| 10 | Bismillahi! | Husemwa kabla ya kufanya jambo lolote jema au mwanzo wa jambo (kwa jina la Mwenyezi Mungu) |
| 11 | Ebo! | Huonyesha mshangao na hasa hutumiwa kwa watoto au kwa walio chini ya mtu kwa umri au cheo. |
| 12 | Hamadi! | Neno la kutakia kitu kipone au kinusurike. |
| | | Hutumika kwa maana ya shtukia, tahamaki, juta. |
| 13 | Hashakum/ ashakum! | Neno ambalo hutumika katika kuombea msamaha kabla ya mtu kusema jambo ambalo linaweza kumkirihi mtu aliyepo |

| | | |
|---|---|---|
| | | mahali hapo; niwie radhi kwa jambo nitakalolisema. |
| 14 | Inshallah! | Mwenyezi Mungu akipenda. |
| 15 | Katu! | Hata kidogo. |
| 16 | Kunradhi/ kumradhi | Tamko la kumwomba mtu haja au msamaha. |
| 17 | La! | Hapana. |
| 18 | Lahaula! | Tamko la kuonyesha mshangao. |
| 19 | Masalaale! | Tamko la kuonyesha mshangao. |
| 20 | Msalheri/ Masalkheri | Tamko linalotumiwa kumwamkia mtu aghalabu wakati wa jioni. |
| 21 | Sabalkheri!/ Sabahalkheri | Salamu ya kumjulia mtu hali wakati wa asubuhi. |
| 22 | Sadakta! | Neno analotumia mtu kuonyesha kuafiki wazo au jambo fulani. |
| 23 | Salaam aleikum! | Salamu ya kutakiana heri na amani, itolewayo wakati wowote na jibu lake ni Aleikum salaam. |
| 24 | Samahani! | Tamko linalotumika kuomba radhi au kumtafadhalisha mtu. |
| 25 | Shabash! | Neno linalotumika kuelezea furaha au mshangao wa mtu anayelitamka kutokana na jambo au kitendo kilichotukia. |
| 26 | Shashimamishi! | Tamko lielezalo hali ya kudharaulika. |
| 27 | Simile! | Tamko linalotumiwa na mtu ili kutaka nafasi apite; tamko la kutahadharisha |
| 28 | Sini! | Kamwe. |
| 29 | Tafadhali! | Neno la heshima la kumwomba mtu afanye jambo kwa hisani yake. |
| 30 | Taibu | Tamko la kuonyesha kukubaliana au kupendezwa na jambo. |
| 31 | Taire! | Tamko linalotumiwa na mganga kilingeni ili kuwafanya watu wamsikilize. |
| | | Tamko la kuonyesha kukubaliana na maneno ya mganga. |
| 32 | Talahi | Hutumika katika kuapa. |
| 33 | Thubutu! | Haiwezekani. |
| 34 | Toba! | Neno linaloonyesha mshtuko kwa jambo lililotokea. |

| | | |
|---|---|---|
| 35 | Wallahi! | Neno linalotumika kuapa au kuthibitisha kuwa linalosemwa ni la kweli. |

**Vihisishi Vilivyokopwa kutoka kwa Lugha Zingine**

| | Lugha Changizi | Kihisishi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Kiingereza | Aisee! | Neno la kumfanya mtu asikilize habari unayotaka kumwambia. |
| 2 | Kiibrania | Aleluya/ haleluya! | Neno la kuonyesha shangwe au furaha |
| 3 | Kihindi | Bilikuli! | Hata kidogo. |
| | | | Kwa kila hali. |
| 4 | Kiajemi | Habedari! | Neno la kuhadharisha, hasa hutumiwa na makuli au mahamali wanapotaka kupita au kuteremsha mizigo. |
| 5 | Kiajemi | Hosanna! | Neno linalotumika kumsifu Mungu. |
| 6 | Kireno | Heria! | Neno linalotumiwa hasa na makuli ili kuhadharisha mtu. |

**iv. Mkopo- Upili**

Kategoria ya mkopo- upili ina vihisishi ambavyo vinaingia katika kategoria ya mkopo na mara hiyo hiyo katika kategoria ya upili. Sababu kuu ya kuwa katika kategoria mbili ni kuwa, kihisishi hicho kimeazimwa kutoka lugha nyingine na pia chaweza kuwakilisha kategoria zingine za maneno kama vile nomino na vivumishi.

**Vihisishi Mkopo- Upili Vilivyokopwa kutoka kwa Kiarabu**

| | **Kategoria zingine** | **Kihisishi** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 1 | Nomino | Afya! | Neno litumikalo kumtakia uzima mtu anapopiga chafya. |
| | | | Hutumiwa na watoto kushawishiana kufanya jambo. |
| 2 | Nomino | Ahsante/ asante! | Neno la kuonyesha shukrani kwa alilotendewa mtu. |
| 3 | Nomino | Hela! | Neno la kumtahadharisha mtu. |
| 4 | Nomino | Maskini! | Tamko la kumhurumia mtu aliyepatwa na maafa. |
| 5 | Kivumishi | Sawa! | Ndiyo, barabara, naam |
| 6 | Kitenzi | Shughulika! | Amri katika jeshi ya kuangalia upande wa kulia, kwenda hatua moja mbele na kasha kurudi nyuma kwa kupigapiga miguu ili kurudi katika mstari na kuhakikisha kuwa mstari umenyoka sawasawa, wakati wa mafunzo ya gwaride. |

Kategoria hii ya mkopo- upili pia ina kihisishi <*afande*> kwa maana ya mwitiko wa heshima wa askari kwa mkubwa wake kilichokopwa kutoka lugha ya Kituruki (TUKI 2013).

**2. Data kutoka Nyanjani**

Vihisishi kutoka nyanjani vimeainishwa katika kategoria mbalimbali kwa kutumia kigezo cha matumizi. Ifuatayo ni orodha ya kategoria kutokana dhima za kimatumizi: mshangao, kukubali, kukataa, dharau, kuitika, kutuliza, kuridhia, mshtuko, kuita, salamu, kushangilia, dua, maagano, shukrani, kusihi, amri, viapo, kuhimiza, kuomba msamaha,

kuomba nafasi, pongezi, kusifu, kubisha, kutaka usikivu, huruma, kufariji, mshtuko, majuto, na vihisishi tata.

**I.Vihisishi vya Mshangao**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Ala! | *Ala!* Kwa nini wanichokoza? |
| 2 | Auuu! | *Auuu!* Lo! Kwa nini alifanya hivyo? Hahaha! |
| 3 | Do! | *Do!* Mtoto wewe kumbe husikii eeeh!<br>*Do! Do!* Huyo? Mwache huyo.<br>*Do!* Nyanyuka mtoto wewe, waangushwa na nini?<br>Sonko mdogo yuko Mombasa *dooo.*<br>*Do!* Ni wewe? |
| 4 | Ha! | *Hahaha!* Nani alisema alienda mbinguni, hiyo ni kati yake na Mungu. |
| | | Auuu! Lo! Kwa nini alifanya hivyo? *Hahaha!* |
| 5 | He! | *He!* Hawa warabu vipi? |
| | | He! Niko mbali kidogo, mpaka kesho jioni. |
| | | *Heeeee! Heeeee!* |
| | | *Heee!* Mashindano! Tushindane leo. |
| 6 | Hei! | *Hei!* Afurahisha huyo. |
| 7 | Kumbe! | *Kumbe!* Nilisahau, wajua alama ya mwalimu ni chaki, samahani. |
| | | Mbona wanidanganya bwana, *kumbe* wewe mwongo, mimi nataka kahawa chungu. |
| 8 | Lahaula! | *Lahaula!* Izoo zimerudi, twende kwetu tukaangalie sinema. Twendeni. |
| | | *Lahaula!* We wala uzee, wala ujana! |
| | | *Lahaula* chakula kimeungua. |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Lo! | *Lo*, kwa nini? |
| | | *Lo!* Nastahili kuwa mkutanoni mie!<br>*Lo!* Leo kuna tope kweli.<br>*Auuu!Lo!* Kwa nini alifanya hivyo? Hahaha! |
| 10 | O! | *O!* Jamani! Jamu yamenda mpaka 'airport.' |
| 11 | Salaale! | Aa! *Salaale!* Wawili? Alhamdulillahi. |
| | | *Salaala!* Mwangale yule! |
| 12 | Wa! | *Wa!* Umeningoja sana? Maskini! Nilikuwa kwa mkutano.<br>*Wa! Wa! Wa!* Umejipodoa kweli, e! Umeng'ara wewe! |

**II.Vihisishi vya Kukubali**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ahaa! | *Ahaa!* Imekupendeza. Mashalla! |
| 2 | Alaa! | *Alaa!* Wewe ndiye Martin? |
| 3 | Ee! | Ooh! Yako ni Samsung? *Ee!* |
| | | *Ee!* Wacha aje ajue mambo ya nauli. |
| | | *Ee* Mungu Mwenyezi twakuomba uwakumbuke wagonjwa wote, wanyoshee mkono wako wapate kupona. |
| | | Wa! Wa! Wa! Umejipodoa kweli, *e!* Umeng'ara wewe! |
| 4 | Eee! | Wacha! *Eee!*<br>Do! Mtoto wewe kumbe hasikii *eeeh!* |
| 5 | Hewaa! | *Hewaa!* Twende mwanzo tumalizie ile ya juzi. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Ndiyo! | *Ndiyo!* Sawa asante. |
| | | *Ndiyo!* Inamanufaa kemkem. |
| | | *Ndiyo!* Nishaweka au wataka niongeze, nikiongeza itachoma boksi. |
| | | *Ndiyo* jamani, ksha watu washangae. |
| | | *Ndiyo* mama. |
| 7 | Sadakta! | *Sadakta! Sadakta!* Naona twaendelea vizuri, wale wakutuma salamu tafadhali tujongenii mbele. |
| 8 | Sawa! | *Sawa* baba naja.<br><br>*Sawasawa!* Nitaleta kesho. |
| 9 | Taibu! | *Taibu* kaka. |
| 10 | Hewala! | Hewala! Nenda. |

**III.Vihisishi vya Kukataa**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | A-a! | *A-a*, Jamani, mimi sijui. |
| | | *A-a*, nabarizi tu. |
| | | *A-a*, Bado, hata nampigia simu hapokei. |
| | | *A-a*, mimi sikuwenda, mama mimi sikwenda huko. |
| 2 | Abadan! | Mimi sikufika kwao *Abadan katan.* |
| 3 | Hapana! | *Hapana*, Chagua nguo ambayo unaweza kuvaa siku nyingi. Wajua wakua wewe. |
| | | *Hapana!* Huyo hakushika simu jana. |
| | | *Hapana!* Usimshike, nwache aende pekee yake. |
| | | Mimi? *Hapana!* |
| | | *Hapana*, usivae hivyo. |
| | | *Hapana! Hapana!* Pia wewe mwenyewe wajua siwezi fanya hivyo. |

| | | |
|---|---|---|
| | | *Hapana*, mama nakumbuka tena vizuri sana. Hukunilipa. We nipe pesa niende zangu. |
| 4 | Hasha! | *La hasha!* Siye aliyeiba. |
| 5 | Hata! | *Hata!* Hatujakutana. |
| | | *Hata*, mimi nipo tu, shughuli ndio nyingi. |
| | | *Hataa!* Amesema atachelewa. |
| | | *Ataa*, usinifanyie ubwete hapa kwangu. Utafanya toka hutaki mpaka utake. |
| | | *Hata!* Sijamwona tangu juzi. Hajakuja huko? |
| 6 | Kamwe! | Basi kwangu hutoshi! Nakwambia. *Kamwe!* Nasema *kamwe* sitoi pesa mara mbili |
| 7 | Katu! | Wallahi mimi sikuamini *katu* ulivyosema. |
| 8 | La! | *La!* Alisafiri leo kwenda kwa nyanya. |
| | | Redio yatangaza askari ishirini wafariki Garrisa, serikali yasema *la*, ni mmoja. |
| | | *La!* Kuna mtu namsubiri hapa. |
| | | A! *La-la-la!* |
| | | *La hasha!* Siye aliyeiba. |
| 9 | Ng’o! | Hata mwaka huu na hata mwaka kesho hutapata *ng’o.* |
| | | Vanga hukuendeki *ng’o!* Itabidi mgeuze gari. Barabara zimesombwa. |
| 10 | Zii! | *Ziii!* Sema mimi siko. |

**IV. Vihisishi vya Dharau**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Aaaa! | *Aaaa*, pengine nimwite anti tu. |
| | | *Aaaaa!*Mpe basi |
| 2 | Ebo! | *Ebo* mtoto wewe, wafanya nini? |
| 3 | Kefule! | *Kefule!* Yaani wanidanganya mimi? |
| 4 | Khaa! | *Khaa!* Nini wewe! |
| 5 | Mavi | *Mavi!* Kwani yeye ni nani? |
| 6 | Mmm! | *Mmm*, ni mlevi yule, achana naye. |
| | | *Mmm!* Hebuwe! (Kwa mtu wa maji) yaani mi ni wazimu. Si pesa ulipewa jana asubuhi. |
| | | *Mm!* wallahi billahi sitawahi waletea maji tena |
| 7 | Po! | *Po!* Abdi wewe kila mara wawaachia kina Nuru mpira, wataka watushinde?<br>Hufaulu *po!* |
| 8 | Poko! | Sitakwambia kitu *poko!* (akitema mate) |

**V. Vihisishi vya Kuitika**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Abee! | *Abee* mama. |
| 2 | Eeh! | *Eeh!* |
| 3 | Labeka! | *Labeka* mwalimu. |

### VI. Vihisishi vya Kutuliza

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Afya | Afya! Kulia juu chini kuna moto. |
| 2 | Chup! | *Chup!* (na ishara ya kidole kwenye mdomo) |
| 3 | Kelele! | *Kelele!* (Shule ya msingi) |
| 4 | Sss! | Sssss! |

### VII. Vihisishi vya Mshtuko

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Mama we! | *Mama we!* Niache na unikome kama ulivyokoma la mamako. |
| | | *Mama we!* Mtamumiza, mwacheni jamani! |
| | | *Mama we!* Mtu yule atazama! |
| 2 | Mungu wangu! | *Mungu wangu!* Nitamwambia nini mama? |
| 3 | Toba! | Yarabi! *Toba!* Roho yangu. Taratibu! |
| | | *Toba* ya ilahi. |
| 4 | Wacha! | Ndiyo! Ina manufaa kemkem.<br>*Wacha!* |
| 5 | Woi! | *Woi!* Nitaanguka kwa maji. |
| 6 | Yarabi! | *Yarabi*! Toba! Roho yangu. Taratibu! |

**VIII. Vihisishi vya Kuita**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Aisee! | *Aisee*, mwanangu mimi nimeyasikia, nimeyaona na sasa hivi wallahi naamini ndiye. <br><br> *Aisee bwana!* Wacha kelele, huku ni Mombasa. |
| 2 | Bwana! | i.Brian! Vipi *bwana*? Umepotea sana. |
| | | ii. *Bwana*, njoounisaidie. |
| | | iii.Aha! Uko wapi *bwana*. |
| 3 | Enyi! | *Enyi!* Mwaja ama hamji nijipange. |
| 4 | Njoo! | *Njoo!*(mama akimwashiria mtoto) |
| | | *Njoo* baba. |
| | | *Njoo! Njoo* hapa haraka. |
| | | *Njoo* bwana unisaidie. |
| | | *Njoo* kesho mapema, kuna nguo za kufua na pasi pia. |
| | | *Njooni! Njooni* nyote, watu washuka. |
| | | Mtume! Naumia jamani, *njooni* mnisaidie |
| | | We! *Njoo* twende, twaitwa. |
| | | *Njoo* basiii… |
| 5 | Taire! | *Taire! Taire! Taire!* |

**IX. Vihisishi vya Kuapa**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Bilahi! | Wallahi *bilahi* mama si zamu yangu, mbona nilifanya jana? |
| | | Lakini kaka wallahi *bilahi* mimi mwenyewe nimeyaona. |
| | | Mm! Wallahi *wabilahi* sitawahi waletea maji tena. |
| | | *Bilahi* watallahi nikipata pesa nitakusaidia. |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Haki ya Mungu | *Haki ya Mungu* si mimi. |
| 3 | Talahi! | Bilahi *watalahi* nikipata pesa nitakusaidia. |
| 4 | Wallahi! | *Wallahi* billahi mama si zamu yangu, mbona nilifanya jana? |
| | | Lakini *wallahi* wazidi kweli. |
| | | *Wallahi* Ali, nilikuwa naye jana. |
| | | *Wallahi!* Sisi hatuna wasiwasi. Maji yakijaa. Sisi ni samaki. |
| | | *Wallahi* mimi sirudi huko. Wale watu wametutenda. |
| | | *Wallahi* mimi sikuamini katu ulivyosema.<br>Lakini kaka *wallahi* billahi mimi mwenyewe nimeyaona.<br>*Wallahi!* Nimefunga.<br>Mm! *wallahi* bilahi sitawahi waletea maji tena |

**X. Vihisishi vya Salamu**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Aleikum salaam! | *Aleikum salaam!* |
| 2 | Hujambo! | *Hujambo!*<br>Sijambo! |
| 3 | Marahaba! | *Marahaba* mwanangu. |
| 4 | Masalheri! | *Masalheri!* |
| 5 | Masalnuru! | *Masalnuru.* |
| 6 | Sabalheri! | *Sabalheri!* |
| 7 | Sabalnuru! | *Sabalnuru.* |
| 8 | Salaam aleikum! | Haloo, *salaam aleikum?* |
| 9 | Shikamoo! | *Shikamoo* baba? |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Sijambo! | Hujambo!<br>*Sijambo!* |
| 11 | Waleikum salaam! | *Waleikum msalaam.* |

**XI. Vihisishi vya Pongezi**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Heko! | *Heko!* Ametoa shilingi elfu kumi, hebu tumpigie mgeni wetu makofi. Tena! Tena... |
| 2 | Hongera! | *Hongera! Hongera* kwa kupata mchumba. |

**XII. Vihisishi vya Kushangilia**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Alleluya! | *Alleluiya! Alleluiya!* Bwana amefufuka. Tuimbe hosana tulitukuze jina la bwana mfufuka. |
| 2 | Huree! | *Hureeee!* Tumeshinda!<br>Ripuripu *huree!* |
| 3 | Oyee! | *Oyeee!* (wakipiga makofi) |
| 4 | Ripuripu! | *Ripuripu* hureee |
| 5 | Shabash! | Mwanangu amefaulu? *Shabash!* |

**XIII. Vihisishi vya Dua**

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Allahuma! | *Allahuma* barikilau. |
| 2 | Amina! | Mungu na amuneemeshe. *Amina!* |
| | | Jina la bwana liinuliwe. *Amina!* |
| | | Asifiwe bwana. *Amina!* |
| | | *Amina* inshalla. |
| | | Basi, mimi naenda, tutaonana wakati mwingine. *Amina!* |
| 3 | Audhubilahi! | *Audhubilahi* wee! Kidogo tungechotwa, leo ni Mungu tu. |
| 4 | Bismilahi! | *Bismilahi* rahaman rahim. |
| | | *Bismilahi!* |
| 5 | Inshallah! | *Amina inshallah* |
| | | *Inshallahkheri*, tutafika Mombasa. |
| | | Mwenyeji: kwaheri tutaonana wakati mwingi<br>Mgeni: *Inshallah!* Nyinyi mbaki salama. |
| | | *Inshallah* nitajitahidi mara nyingine. |
| 6 | Jazakalla! | *Jazakalla* kheri. |
| 7 | Mashalla! | *Mashalla!* Kunani bwana, jionee mwenyewe! |
| | | *Mashalla* tabia yake nzuri sana. |
| | | *Mashalla* ana nywele ndefu. |
| | | Mimi nashukuru *mashalla* yule wangu yuajua kupika. |
| 8 | Mtume! | *Mtume!* Naumia jamani, njooni mnisaidie |
| | | Mswalie *mtume!* Mswalie *mtume!* Mama wewe. |

**XIV. Vihisishi vya Maagano**

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Alamsiki! | *Alamsiki* – binuru. |
| 2 | Kwaheri | *Kwaheri* mwenzangu tutaonana wakati mwingine. |

**XV. Vihisishi vya Shukrani**

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Asante! | *Asante*. Nauliza kama mzee Gitau yuko? |
| | | *Asante,* tushapoa. |
| | | *Asante,* mzee wangu *asante.* |
| | | Shukrani sana Liz kwa kuongea nasi. *Asante sana!* |
| | | Sawa *asante.* |
| 2 | Shukrani | *Shukrani* sana Liz kwa kuongea nasi. Asante sana! |
| | | *Shukrani!* Karibuni tena. |
| | | Nina afadhali*, shukrani.* |
| | | *Shukrani* kwa mwaliko ndugu. |

**XVI. Vihisishi vya Kusihi**

| | Kihisishi | Vishazi |
|---|---|---|
| 1 | Ewe! | *Ewe*! Mwenyezi Mungu, tuhurumie haya mafuriko yamezidi. |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Tafadhali! | Naam, ishirini, nitafutie *tafadhali*. |
| | | *Tafadhali!* Tujibidiishe ili tuyape magari nafasi. |
| | | Nipe chapati na kukuna unipashie moto *tafadhali!* |
| | | Tangazo la afya kwa watu wa Kwale, Kilifi na Mombasa Juni. Dawa za minyooo kwa watoto wa kati ya miaka miwili na kumi na minne. *Tafadhali* mjulishejirani. |
| | | Sadakta! Sadakta! Naona twaendelea vizuri, wale wakutuma salamu *tafadhali* tujongenii mbele.<br><br>Sasa bwana nataka uniwekee nyingi kuliko jana, *tafadhali* niwekee miraa mizuri. |

**XVII.Vihisishi vya Huruma**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Maskini! | Wa! Umeningoja sana? *Maskini.*Nilikuwa kwa mkutano. |
| | | *Maskini!* Poleni! Hiyo ni gharama kweli.<br><br>*Maskini!* Si angempa tu waachane salama. |

**XVIII. Vihisishi vya Samahani**

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | Hashakum! | *Hashakum* ndugu. |
| 2 | Kidogo! | *Kidogo!*<br><br>*Kidogoo!* Naja. |
| 3 | Kumradhi | *Kumradhi* mwalimu, naomba kwenda msalani. |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Samahani! | Babake Fatuma tumekuweka. *Samahani,* mambo ndo yamekuwa mengi. |
| | | *Samahani* ndugu kwa kukosa kuhudhuria arusi yako, siku hiyo nilipatwa na dharura. |
| 5 | Simile! | *Simile!* Dada |

**XIX. Vihisishi Tata**

Vihisishi tata vinawakilisha kategoria ambayo kihisishi kimoja kina dhima zaidi ya moja ambazo zaweza kueleweka vizuri kutegemea muktadha wa matumizi.

| | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|
| 1 | A! | *A!* We chukua pesa bwana.<br>*A*, Vuka basi<br>*A!* Acha kutoka nje, tulia twaenda.<br>*A!* Njoo dada.<br>*A!* Dada tuyaache hayo.<br>*A!* Mambo ya nyuma sipendi mimi.<br>*A* vipi? Rafiki. Karibu! Huendi?<br>*A!* La-la-la! |
| 2 | Aa! | *Aa!* Salaale! Wawili? Alhamdulillahi<br>*Aa!* Basi mimi sina habari.<br>*Aa*, nina matatizo tu ya hapa na pale lakini nipo.<br>*Aa!* Waniumiza!.<br>Oooh! *Aa!* Nilikuwa nadhani ni upande huu mwingine.<br>Wewe ndio Saimo? *Aa.* |
| 3 | Aaa! | Wewe ndo Saimoni? Aaa!<br>*Aaa*, ama tujifanye tunanunua viatu. |

| | | |
|---|---|---|
| | | *Aaa!* Za Mji Mkuu ziko mbali wewe!<br><br>*Aaa.*Pole!<br><br>Umemwona Rajan karibuni? Amenenepa! *Aaa*<br><br>*Aaa!* Kongoni anti.<br><br>Aaa! Umeyasikia ati, Zainabu kapewa talaka |
| 4 | Afande! | 1. *Afande!* (pamoja na saluti)<br>2. *Afande!* Na yule mzee wa jana anahitaji msaada wetu.<br>3. *Afande!* |
| 4 | Aha! | *Aha!* Kumbe wajua shairi, wewe ni mtoto mzuri, kesho nitakununulia zawadi.<br><br>.*Aha!* Uko wapi bwana. |
| 5 | Ai! | *Ai! Ai!* Ni jumamosi, mimi nilifikiri jumapili.<br><br>*Aiiii!* Kweli! Siamini.<br><br>*Ai!* Wee! Ati mzee Gitau.<br><br>Kuombaomba kumezidi, *ai?* Kwanikera roho kweli, si watoto, si kina mama si kina baba. |
| 6 | Aka! | Wee! Mama yuko? *Aka.*<br><br>*Aka!* Langu li chachu.<br><br>*Aka!* Kumbe ni mwizi? |
| 7 | Alahamdulillahi! | Twashukuru,*alhamdulillahi!*<br><br>*Alhamdulillahi* nimefaulu.<br><br>Aa! Salaale! Watoto wawili? *Alhamdulillahi!* |

| | | |
|---|---|---|
| 8 | Ati! / Eti! | *Eti* mara daktari mkubwa hayuko, mara sijui nini.<br><br>*Ati* wataka nipigie kina nani simu?<br><br>*Eti*! Abubakari amefariki?<br><br>*Ati*, wasema nini?<br><br>*Ati* waringa, waringa nini na hata kuoga mwenyewe hujui hapo ulipo.<br><br>*Ati* alisema tunamaliza pesa na hata 'credit' hatoi?<br><br>*Eti* watu wanunua, kuna moja yuapeleka, hiyo ni nini sasa?<br><br>Eti? Ana wazimu huyu? Si pesa yake alipewa na Mwanakombo iyo hiyo jana?<br><br>Ai! Wee! *Ati* mzee Gitau? |
| 9 | Basi! | *Basi!* Nimeangusha.<br><br>*Basibasi* Nimesikia!<br><br>*Basi! Basi! Basi!*<br><br>*Basi* nipe pesa.<br><br>*Basi* kwangu hutoshi! Nakwambia.<br><br>Nikaenda kununua kadi, nikienda kununua, mwenzangu naye akanipigia, nikajua *basi!*<br><br>Njoo *basiii…*<br><br>*Basi* tosha! |
| 10 | Ei! | *Ei!* Nyinyi watu si mmezunguka?<br><br>*Ei?* Mamake, mbona wakaa nje? Waumwa? |
| 11 | Enhee! | Ni elfu mbili tu?<br><br>*Enhee.*<br><br>*Eheee!* Kumbe! Umezoea kuibia watu pesa, wafikiri watu wajinga *eh!*<br><br>*Enhee?* |
| 12 | Haya! | *Hayahaya!* Sukuma mbele.<br><br>*Haya,* mama acha tuanie gari. Gari litakuja hapa hapa.<br><br>*Haya Haya!* Bwana utatugonga. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Wasalimie. *Haya!*<br><br>*Haya! Haya! Haya!* Tuharakishe, chunga begi lako, wanaoshuka kutoka juu *hayahaya*! Njia ni moja, tupande vidatu, chunga mzigo, soko limehamishwa, baada ya vidatu nunua vitu.<br><br>*Haya!* Wafanya nini?<br><br>*Haya!* Nishasikia.<br><br>*Haya* kwaheri.<br><br>*Haya* sawa.<br><br>*Haya!* Ameanguka majini!<br><br>*Haya!* Baki nayo, si wajidai hukumbuki wewe tena, basi nishukishe…njooo mwanangu tushuke.<br><br>*Haya!* 'Credit' lazima mnunue?<br><br>*Haya*, baadaye tutazungumza. |
| 13 | Hebu! | *Hebu*, nipeshe tafadhali<br><br>*Hebu* mkariri nisikize. Mjue jioni ni mashairi.<br><br>*Hebu* ingia.<br><br>*Hebu* rudi huko wewe!<br><br>Mmm! *Hebu* we! (Kwa mtu wa maji) yaani mi ni wazimu. Si pesa ulipewa jana asubuhi? |
| 14 | Jamani! | *Jamani!* Hivi vitu vitaenda.<br><br>*Jamani!* Mpeni nafasi awahutubie.<br><br>*Jamani!* Huyo mtu ametufuata sana.<br><br>O! *Jamani!* Jamu yamenda mpaka 'airport'<br><br>Sista Stefani alienda mbinguni lini? *Jamani*, tuongee ukweli. Nilifikiri Yesu atakapokuja atawachukua waliokufa.<br><br>Si anirahisishie kazi *jamani!*<br><br>*Jamani*, twende tukanywe chai.<br><br>Ndiyo *jamani*, kisha watu washangae.<br><br>Poleni! *Jamani*! Poleni!<br><br>Mama we! Mtamuumiza, mwacheni *jamani!* |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mtume! Naumia *jamani, jamani* njooni mnisaidie.<br><br>Huku Majengo hakupitiki, lazima uvushwe na bodaboda, jamani tutaenda wapi?<br><br>*Jamaniii!* Nisaidieni! Naumia. |
| 15 | Karibu! | *Karibu! Karibu* mume wangu napole kwa safari.<br><br>*Karibu* shangazi, tumekukosa kweli.<br><br>Nashukuru! *Karibuni* tena.<br><br>A! Vipi? Rafiki. *Karibu!* Huendi?<br><br>*Karibu!* Mlango uko wazi. |
| 16 | Mmh! | *Mmh*, ndivyo ilivyo.<br><br>*Mmh.* |
| 17 | Naam! | *Naam!* Mwambie aliyekutuma zimeisha.<br><br>*Naam*, ishirini, nitafutie tafadhali.<br><br>*Naam!* Wasemaje wewe? |
| 18 | Oh! | *Oh*! Mama Rahab.<br><br>O*ohoo!* Nilikuwa nataka umri wako.<br><br>*Ooh!* Yako ni Samsung.<br><br>O*ooh!* Ndo maana wafungua ile akaunti?<br><br>*Ooh!* Pole! Sasa umepona? |
| 19 | Pole! | *Poleni*! Jamani! *Poleni!*<br><br>*Pole, pole* kwa kukuweka. We nenda, nikiwa tayari nitakuita.<br><br>*Pole* bwana kwa kukusumbua wikendi.<br><br>Nzuri *Pole* uko ‘prayer?’ Twahitaji devera, ni dharura, mafuriko.Maskini! *Pole*<br><br>Maskini! *Poleni*, hiyo ni gharama kweli.<br><br>Ooh! *Pole!* Sasa umepona?<br><br>*Pole! Pole* sana mama, sikuwa nakuona.<br><br>*Poleni!* Haki *poleni*. Sikujua, nilikuwa mfanyikazi wake miaka mitano iliyopita na nikarudi bara.<br><br>Karibu! Karibumume wangu na *pole* kwa safari. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ulidhani nitafutwa kazi, *Pole! Pole* dada! |
| 20 | We! | *We!* Siwezi mimi. Huko ni mbali sana.<br><br>*We!* Leo huo upepo umezidi.<br><br>Billget anatoa paunti bilioni ishirini na tano! *We!* Pesa hizo hata tukishikana Afrika nzima hatuwezi kutoa.<br><br>*Wee!* Acha mchezo.<br><br>*Wee!* Hayo ni mageni kwangu, ndo leo nayasikia.<br><br>*We!* Mtaanguka, hapa kwateleza.<br><br>Audhubillahi *wee!* Kidogo tungechotwa, leo ni Mungu tu. *We!* Njoo twende, twaitwa.<br><br>*Wee!* Huoni wanikanyaga mguu?<br><br>*Wee!* Mama yuko?<br><br>Ai! *Wee!* Ati mzee Gitau. |

**XX. Kategoria Zingine**

| | **Kategoria** | **Kihisishi** | **Vishazi** |
|---|---|---|---|
| 1 | Kitangulizi cha hadithi | Hadithi hadithi!<br><br>Paukwa | 1. *Hadithi hadithi!* – Hadithi njoo.<br><br>2. *Paukwa- Pakawa.* |
| 2 | Kuhimiza | Halambe/ Harambee | *Harambee harambee* tuvute pamoja tujenge nchi yetu. |
| 3 | Kubisha | Hodi! | *Hodi!* |
| 4 | Kusifu | Hosana! | Alleluiya! Alleluiya! Bwana amefufuka. Tuimbe *hosana* tulitukuze jina la bwana mfufuka. |
| 5 | Kusisitiza | Kabisa! | Watu huenda mahali kwa chemichemi, siyo mahali pasipo na kitu. *Kabisaa!* |
| 6 | Kukaribisha | Kongoni! | Aaa! *Kongoni* anti. |
| 7 | Kutaka taarifa | Kulikoni! | Maeneo ya Mombasa, Mwembe Tayari, Miritini, tufahamisheni *kulikoni* barabarani. |
| | Kutaka taarifa | Kunani! | Mashalla! *Kunani* bwana, jionee mwenyewe! |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8 | Kufariji | Makiwa! | *Makiwa,* yashapita. |
| 9 | Majuto | Ole! | *Ole wenu* tu mama amesema. |
| 10 | Kitangulizi cha Hadithi | Paukwa! | *Paukwa! - Pakawa.* |
| 11 | Amri | Shughulika! | *Shughulika!* Waniangalia kama hunijui, sinimekwambia ukimbie Marikiti. |

## KIAMBATISHO B: KIONGOZI CHA MAHOJIANO

1. Taja njia mbalimbali ambazo waweza kumshukuru mtu.
2. Tafadhali eleza njia tofauti tofauti za salamu.
3. Ikiwa unashurutishwa na mtu kufanya jambo ambalo hulitaki, utakataa kwa kutumia maneno yepi?
4. Eleza njia tofauti ambazo watu hutumia kuelezea pole zao kwa familia ambayo imempoteza mmoja wao.
5. Ukiitwa na mtu wewe huitika vipi?
6. Watu huonyesha mshangao vipi?
7. Ni maneno yepi ambayo mtu hutumia kuomba msamaha?
8. Ikiwa hufurahishwi na kinachosemwa au kinachotendwa na mtu, utatumia maneno yepi kumdharau au kumkejeli?
9. Hasira huonyeshwa kupitia kwa maneno yepi?
10. Umeombwa kuzungumza na maarusi baada ya harusi, utatumia njia zipi kuwapongeza?
11. Taja njia ambazo waweza kumtakia mwenzako heri.

## KIAMBATISHO C: VIBALI VYA UTAFITI

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/23538/2013

DATE: 3rd August, 2015

Director General,
National Commission for Science, Technology,
& Innovation
P.O. Box 30623-00100,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION KHAVAI ADELAIDE– REG. NO. C50/23538/2013

I write to introduce Mr. Khavai Adelaide who is a Postgraduate Student of this University. He is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili.**

Mr. Khavai intends to conduct research for a M.A proposal entitled, **"Pragmatiki ya Kihisishi cha Kiswahili".**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

MRS. LUCY N. MBAABU
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

EO/ee

REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY
STATE DEPARTMENT OF EDUCATION

Telephone Mombasa 2315327/
2230052
When replying please quote
Email:pdecoast@yahoo.com

COUNTY DIRECTOR OF
MOMBASA COUNTY
P. O. BOX 90204-8010
MOMBASA

Ref. No.MC/ED/GEN/23/5/13

20th May 2015

Principal s & Head teachers
**MOMBASA COUNTY**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION KHAVAI ADELAIDE MBOVA REGISTRATION NO.P/15/8192/5801**

The above named who is a postgraduate student pursing Masters degree in Kiswahili in the Department of Kiswahili at Kenyatta University has been authorized to carry out a research on "**Pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili**" for a period ending 30th June 2015.

She is expected to furnish this Office with a copy of the research work upon completion.

Please accord her the necessary co-operation.

FOR:-
COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
P. O. Box 90204 - 80100

Newton E. Okwatsa
**FOR: COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION**
**MOMBASA COUNTY**

Copy to: Said Hussein
Kenyatta University
P. O. Box 43844-00100
**NAIROBI**

Khavai Adelaide Mboya

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION

Telephone: +254-20-2213471, 2241349, 310571, 2219420
Fax: +254-20-318245, 318249
Email: secretary@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No.

Date:

**13th May, 2015**

**NACOSTI/P/15/8192/5801**

Khavai Adelaide Mboya
Kenyatta University
P.O. Box 43844-00100
**NAIROBI.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Pragmatiki ya kihisishi cha kiswahili,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Mombasa County** for a period ending **30th September, 2015.**

You are advised to report to the **County Commissioner and the County Director of Education, Mombasa County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are required to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**SAID HUSSEIN**
**FOR: DIRECTOR GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Mombasa County.

The County Director of Education
Mombasa County.

National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO 9001: 2008 Certified

**CONDITIONS**

1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit
2. Government Officers will not be interviewed without prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one(1) soft copy of your final report.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice

**REPUBLIC OF KENYA**

NACOSTI

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEARCH CLEARANCE PERMIT**

Serial No. A 5105

**CONDITIONS: see back page**

THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MS. KHAVAI ADELAIDE MBOYA*
of KENYATTA UNIVERSITY, 151-90129
ngwata,has been permitted to conduct
research in *Mombasa County*

on the topic: *PRAGMATIKI YA KIHISISHI CHA KISWAHILI*

for the period ending:
*30th September,2015*

Permit No : NACOSTI/P/15/8192/5801
Date Of Issue : 13th May,2015
Fee Recieved :Ksh 1,000




...............................
*Applicant's Signature*

...............................
*Director General*
**National Commission for Science, Technology & Innovation**

OFFICE OF THE PRESIDENT

*MINISTRY OF INTERIOR AND CO-ORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT*

Telephone: Mombasa 2311201
Fax No.041-2013846
Tel.0722371400
Email: msacountycommissioner@yahoo.com
*When Replying please quote:*

COUNTY COMMISSIONER'S OFFICE
MOMBASA COUNTY
P.O. BOX 90424-80100
**MOMBASA**

Ref. No.**MCC/ADM.25/72**

**20th May, 2015**

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**
**KHAVAI ADELAIDE MBOYA**

This is to confirm that Khavai Adelaide Mboya, a student at Kenyatta University has been authorized to carry out research on **"Pragmatiki ya kihisishi cha Kiswahili"** in Mombasa County for a period ending 30th September, 2015.

Any assistance given to him will be highly appreciated.

Thank you.

(APP) for Nelson Marwa Sospeter
COUNTY COMMISSIONER
**MOMBASA COUNTY**